SUPA JACKPOT
TZS. 1,059,844,733
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**RIPOTI MAALUM**
Kilichojificha machinga wagumu kuondoka masoko ya barabarani

UKURASA 8



Nipashe TESA
Jumanne Desemba 20, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

UWEZO AWARD
Kisima kinachoibua wajasiriamali wabunifu na wagunduzi shuleni
Ukurasa 15

MWISHO KUSOMA KINADHARIA
Uwekezaji mafunzo kwa vitendo mpango mpya maendeleo ya jamii
Ukurasa 14

SAYANSI
NA MWANDISHI WETU

Ufugaji kuku Dar unavyozidi kuwa pasua kichwa, magonjwa, vifo balaa
• Mtaalamu: Wazoefu wasaidie, dawa asili zitumike

"NIMEKATA tamaa. Nasikitika mdondo umevamia banda langu nimebakia na kazi moja kuangalia kuku wangu wanavyosinzia na kuanguka nyakati za mchana ambazo walitakiwa kula, badala ya kuwalisha ninawachinja.

"Kwa vile siwezi kukesha nao bandani, nikiamka asubuhi ninapofungua mlango naanza kutupa vibudu vya kuku waliouawa na mdondo na mafua usiku." Anasema Anastazia Mrosso mkazi wa Madale, Dar es Salaam, anayefuga kuku.

Mama huyo analalamika kuwa magonjwa ya ndui ya kuku, mdondo na mafua yamezidi na kwamba kila kifaranga kinachofugwa mtaani ili familia ijipatie mayai ya watoto...

...kuwekwa kwenye maji ili kuku wale na kunywa. Magonjwa mengi ya virusi hivi vinavyoshambulia kuku na kusababisha vifo vya maelfu kwa wakati mmoja na kuongeza hasara kwa wafugaji hasa huku mijini japo na vijijini shida hiyo," anasema.

Mfugaji huyo anaamini kuwa ni lazima kuwe na njia nyepesi ya kuwapa kuku tiba kuliko ilivyo sasa ili kupunguza ugumu wa ufugaji mijini.

"Tunasikia ndui inachanjwa kwenye bawa zipo nyingine kwenye jicho inakuwa vigumu kuchanja. Hata kama kuna ugunduzi wa chanjo kuwakinga kuku na ugonjwa wa mdondo, ndui na mafua bado kuna ugumu. Nina wasiwasi kuwa huenda maradhi hayo yamekuwa sugu ndiyo maana kila mwaka yanaibuka na kusababisha maafa zaidi," anasema Joan.

Anaongeza kuwa dawa madukani zinawachanganya wataalamu...

# Nipashe

Jumanne Desemba 20, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581165

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 13



Ofisa Mkuu Rasilimali Watu wa Benki ya NMB, Emmanuel Akonaay (wa pili kushoto), akikabidhi Tuzo ya Mwajiri Bora Afrika kutoka Taasisi ya Employer Branding kwa Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Filbert Mponzi, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Ofisa Mwandamizi Rasilimali Watu wa NMB, Pamela Deteba na kulia ni Mkuu wa Idara ya Masoko, Rahma Mwapachu. **Habari UK. 9. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sita jela miaka 50 kwa njama ya kupindua serikali

**WAPATA** mafunzo nje ya nchi, wamo ndugu watatu...*Endelea Uk. 2*

## Ghorofa laanguka, laua watano



UKURASA 2

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Sembeti, Kata ya Marangu Mashariki, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wakishirikiana na askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kufukua kifusi kutafuta miili ya watu walioangukiwa na jengo la ghorofa mbili lililokuwa likiendelea kujengwa jana. **PICHA: MARY MOSHA**

## Korti yaagiza uchunguzi wa mwili aliyefia kituoni polisi

UKURASA 7




MICHEZO YANGA, COASTAL MTIHANI MZITO LEO UK. 32
KATUNI UK. 6



Baadhi ya washiriki wa mkutano wa siku mbili wa wadau wa Sekta ya Mifugo wakimsikiliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati alipofungua mkutano huo kwenye ukumbi wa PSSSF jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Jela miaka 50 kwa jinai kutaka kuipindua Serikali ya Tanzania

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imewatia hatiani watu sita, wakiwamo watatu wa familia moja na kuwahukumu kwenda jela miaka 50 kwa kosa la kula njama kutaka kuipindua Serikali ya Tanzania.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki mbele ya Jaji Dk. Yose Mlyambina kwenye Masijala Ndogo ya Songea.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Seif Chombo, Abdallah Chombo, Mohamed Kamala, Athumani Chombo, Omary Mbonani na Rashidi Ally.

Akisoma hukumu hiyo, Jaji Yose alisema washtakiwa wanatuhumiwa kati ya Januari Mosi 2014 na Julai 13, 2020, kwenye maeneo tofauti wilayani Tunduru mkoani Ruvuma na maeneo mengine nchini, kwa pamoja walikula njama ya kufanya ugaidi.

Wanadaiwa kula njama kuanzisha vita ya kidini vijulikanavyo Jihad na kuwashawishi vijana kuongeza nguvu kuipindua Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuanzisha Taifa la Kiislamu kwa kutumia nguvu na machafuko.

Alisema malengo yalikuwa kuongoza kwa kutumia sheria za Kiislamu, washtakiwa walipekelekwa nchi mbalimbali zenye uongozi wa Kiislamu kwa ajili ya mafunzo zaidi ya Jihad kinyume cha sheria na taratibu za Jamhuri Muungano wa Tanzania.

"Kitendo hicho hakihatarishi tu maisha ya watu wengine, bali hata wao wenyewe, ni hatari kwa maisha yao, " alisema Jaji Yose.

Washtakiwa walifikishwa mahakamani kwa makosa mawili ya kula njama kufanya ugaidi na kushiriki vikao vya kufanya ugaidi.

Washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo kwenye Kijiji cha Lumbukule na maeneo mengine wilayani Tunduru, Mkoa wa Ruvuma ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ilidaiwa mahakamani huko kuwa washtakiwa kwa pamoja na wengine ambao hawakuwapo mahakamani, walishiriki kufanya kikao kinachohusiana na masuala ya ugaidi, kula njama ya kutaka kuanzisha Serikali ya Kiislamu kwa kutumia nguvu kwa malengo ya kuvuruga mfumo wa kisiasa, kiuchumi na kijamii wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Washtakiwa hao walikana mashtaka hayo, lakini walikiri kukamatwa na waliposomewa hoja za awali, walizikana isipokuwa majina yao, wakazi wa Lukumbule, walikubali kwamba walikamatwa na kupelekwa kituo cha polisi na kwamba wanaujua msikiti wa Al Malidi na wanaishi kwenye kijiji hicho tangu mwaka 2017 mpaka 2020.

Katika kesi hiyo, Jamhuri iliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Hebel Kihaka aliyesaidiana na Tulimanywa Majigo na Edgar Bantilaki.

Washtakiwa walikuwa wakiwakilishwa na Mawakili Naomi John, Nestory Nyoni Rafael Matola, Alex Nyoni, Razaro Simba na Denis Razaro.

Katika kesi hiyo, upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi wanne na vielelezo vitano.

Washtakiwa walijitetea wenyewe kwa kiapo na hakuna aliyekuwa na kielelezo chochote.

Miongoni mwa ushahidi uliotolewa ni kwamba serikali iliharibu kambi yao maeneo ya Lukumbule, Tunduru maeneo ya Magazini, Nanyumbu, Ntamba Swala mpakani mwa Msumbuji, Tandahimba, Newala na Masasi na Mtwara.

Ushahidi ulidai malengo ya washtakiwa yalikuwa uamuzi wote ufanyike chini ya misingi ya Quran Tukufu.

Inadaiwa viongozi wao wanaishi Ruvuma, Lindi, Mtwara na Pwani na kwamba viongozi wachache walikamatwa huku wengine wakifanikiwa kukimbilia Msumbiji.

Pia ilidaiwa wahalifu hao waliua na kuharibu vijiji ambavyo viligoma kuungana nao, walichukua mali za watu zikiwamo fedha na kuharibu mali zisizohamishika.

Hata hivyo, washtakiwa wakati wa utetezi walikana kuhusika kufanya matukio hayo.

Mahakama baada ya kusikiliza shauri hilo, ilijiridhisha kwamba upande wa Jamhuri umeweza kuthibitisha makosa dhidi ya washtakiwa bila kuacha shaka.

"Mahakama ilijiridhisha kuwa washtakiwa wote walikula njama kutaka kuipindua serikali iliyoko madarakani na walipata mafunzo.

"Kutokana na ushahidi ulioko, mahakama ilizingatia maombi ya washtakiwa kupunguziwa adhabu lakini kutokana na makosa waliyotenda, mahakama inawatia hatiani na kuwapa adhabu ya kutumikia kifungo cha miaka 20 kwa kosa la kwanza na miaka 30 kwa kosa la pili, adhabu zote zinakwenda kwa pamoja," alisema Jaji.

Mahakama iliwapa haki yao ya msingi kama hawakubaliani na adhabu wanaruhusiwa kukata rufani.

# Jengo lilivyoporomoka na kuua watu watano

**Na Waandishi Wetu,** MOSHI

WATU watano wamefariki dunia kwa kuporomokewa na jengo la ghorofa mbili la makazi lililokuwa likijengwa na mmoja wa wafanyabiashara katika Kijiji cha Sembeti, Kata ya Marangu Mashariki, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Watu wengine tisa waliokuwa wakifanya kazi za ujenzi katika jengo hilo, wamejeruhiwa na hali zao ni mbaya, huku mmoja akiendelea kutafutwa chini ya vifusi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Simon Maigwa, akizungumza na Nipashe kwenye eneo la tukio la ajali hiyo, alisema liliporomoka na kusababisha ajali hiyo usiku wa Desemba 18.

Jengo hilo lililokuwa kwenye hatua ya kumwaga zege silabu ya ghorofa ya pili, linalodaiwa kuporomoka na kuanguka, kati ya saa tatu na saa nne usiku.

"Mpaka jana usiku (juzi) tulikuwa tumetoa maiti watatu, lakini mwingine alikuwa analalamika anasikia baridi na majira ya usiku akawa amefariki na kufanya waliofariki kufikia wanne. Jana tuliendelea na uokozi na tukaopoa mwili mwingine wa tano.

"Mtu mwingine ambaye hali yake ni mbaya zaidi, amehamishiwa KCMC (Hospitali ya Rufani ya Kanda) na Hospitali ya Marangu, wako majeruhi wanane. Wale wengine (vibarua) ambao wamebaki hawakuwa na jeraha lolote. Ila mmoja bado tunamtafuta hatujampata, tunaendelea na uokozi.

Alipoulizwa kuhusu chanzo cha tukio hilo, alisema umma utataarifiwa kuhusu chanzo chake baada ya uchunguzi, kwa sababu mmiliki wa jengo hilo hayupo na inasemekana ni mkandarasi yuko jijini Dar es Salaam.

"Mmiliki naye tunamhitaji tuendelee kumhoji, kwa sababu sisi pia tumefungua jalada la uchunguzi, ambalo tunaendelea nalo. Tumeandika maelezo ya vibarua mbalimbali ambao walikuwa wanafanya kazi pale ili tuweze kujua nani ni foremen (msimamizi wa ujenzi).

"Je, ni nani aliyekuwa anahusika na ujenzi? Je, taratibu zilifuatwa? Kujua chanzo ni baada ya ile tume iliyoundwa, ambayo itahusisha wataalamu ambao watatoa majibu yaliyo sahihi," alisema Kamanda Maigwa.

Kwa mujibu wa ACP Maigwa, ripoti ya uchunguzi huo itakapokamilika na kuonyesha watu hao walipelekwa kujenga jengo hilo bila ya kufanya maandalizi mazuri, sheria itachukua mkondo wake, baada ya kuonekana uzembe uko upande gani.

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000, inaelekeza kuwa Mamlaka ya Serikali ya Mitaa (halmashauri), ina jukumu la kutoa kibali cha ujenzi ndani ya siku 30 kwa mwombaji aliyekubaliwa.

**SERIKALI YAUNDA TUME**

Kutokana na ajali hiyo, serikali imetangaza kuunda timu maalum ya wataalamu wa kada mbalimbali, kuchunguza chanzo cha kuanguka kwa jengo hilo na kusababisha vifo hivyo.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Abbas Kayanda, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Moshi akitoa taarifa ya awali kuhusu tukio hilo alisema: "Serikali, tutaunda timu ya kuchunguza sababu kubwa iliyosababisha jengo hilo kuanguka na kusababisha hao wenzetu watano kupoteza maisha.

"Kwenye hilo jengo kulikuwa na wafanyakazi 30 ambao ni vibarua na mafundi ujenzi, ambapo wafanyakazi 16 kati yao ndio wamesalimika."

**MHANDISI AELEZA SABABU**

Mhandisi wa Ujenzi Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Lameck Bernard, aliyekuwa katika eneo la tukio, alisema kwa sasa wamechukua baadhi ya malighafi zilizokuwamo kwenye eneo linalotekelezwa mradi huo kuona nini chanzo cha kuporomoka kwa jengo hilo.

"Tumefika hapa tumejionea hali halisi, lakini uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa jengo hilo limejengwa mfululizo na halikupata muda wa kupumua na kuruhusu taratibu nyingine za kiujenzi," alisema.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi na Mary Mosha**

## TANGAZO




# Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

## Zoezi la kuanza ujazaji wa maji kwenye Bwawa la Julius Nyerere

# 22/12/2022

**BWAWA LANGU | BWAWA LAKO | BWAWA LETU**

Tutakuwa Mubashara TBC UHAI TV ITV TANZANIA millardayo Clouds MAELEZO TV

www.tanesco.co.tz

#TupoKazini

17201202

# Ilivyo mikataba ya bodaboda inavyowaachia vilio na simanzi

**Na Halfani Chusi**

**KATIKA sehemu ya kwanza ya ripoti hii jana, madereva wa pikipiki za kubeba abiria, maarufu bodaboda, walibainisha kinachowasibu kutokana na dosari zilizomo kwenye mikataba wanayoingia na mabosi wao wanaowanunulia pikipiki kwa ajili ya kuendesha biashara hiyo.**

**Vilevile, uongozi wa bodaboda Mkoa wa Dar es Salaam ulibainisha hatua mbalimbali zinazochukuliwa kukabiliana na tatizo hilo. Endelea na sehemu ya mwisho kujua hatua zaidi zinazochukuliwa na wadau pamoja na serikali.**

---

**JICHO LA KISHERIA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga anasema mikataba mingi ya madereva bodaboda huwa inaegemea kwa tajiri kwa kuwa wengi wao hawana utaratibu wa kutumia wanasheria wakati wa kutia saini makubaliano hayo kwa kuogopa gharama.

"Mikataba mingi ya bodaboda haisemi 'mpaka siku fulani usipoleta fedha, ninapokonya chombo'. Mfano kama mkataba unasema fedha iletwe kila Jumapili, lakini haisemi kwamba isipoletwa Jumapili moja, mmiliki ananyang'anya pikipiki. Mkataba ukiwa hivyo, unakuwa mkataba lakini ni kandamizi.

"Mikataba yote inatakiwa iwe na pande mbili, iwe na usawa, iwe na muda maalum, uwe mkataba wa mtu kuingia kwa hiari, hapo kwenye hiari mtu anaweza kuingia kwa shida lakini hajakubali kutokana na masharti ya mkataba, mkataba hautakiwi kuwa kandamizi.

"Kwa kesi ya bodaboda kusema lazima fedha ziletwe siku fulani na asipoleta siku hiyo, atapokonywa chombo. Inatakiwa ifahamike kuwa dereva anaweza kupata matatizo ya mkwamisha kupata fedha, kwenye udereva kuna mengi, hivyo mikataba ya aina hiyo inakuwa haitendi haki na inapingana na sheria za mikataba zinavyotaka," anafafanua.

Mkurugenzi Mtendaji huyo anasema kuwa hata kama bosi anaamua kumpokonya chombo dereva, kuna vitu vya kufuata ikiwa ni pamoja na kumpa kwanza onyo.

"Huyo anayepokonywa, kama ana ushahidi anaweza kwenda mahakamani kufungua shauri la madai," Anna anashauri.

Mbobezi huyo wa sheria anakirejea Kifungu cha 15 cha Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini ya Mwaka 2004 kinachomtaka kila mwajiri na mwajiriwa kuhakikisha kabla ya kuanza kazi, kuwe na mkataba wa maandishi uliotiwa saini na pande zote mbili.

"Pamoja na uwezekano wa kuwapo makubaliano kati ya mwajiri na mfanyakazi, makubaliano hayo yanapaswa yafanyike kwa sababu za msingi na si kwa lengo la kujaribu kumnyima mfanyakazi baadhi ya haki zake zilizoko kisheria," Anna anatoa angalizo.


Anna Henga


Patrobas Katambi

**KAULI YA SERIKALI**

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, anabainisha hatua zinazochukuliwa akitoa agizo lililokwenda sambamba na onyo.

"Kwa sehemu kubwa ukiingalia Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, inamlinda sana mfanyakazi japo inalinda pia maslahi ya mwajiri. Kwa mfumo wa sheria zetu, kama mkataba utatengenezwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania, hauna tatizo.

"Sheria pia inamruhusu mfanyakazi kuingia makubaliano ya awali na mwajiri kabla ya kutia saini mkataba wa kufanya kazi ili kama kuna sehemu haipo sawa kati ya mwajiri na mwajiriwa wanaweza kuangalia namna ya kuurekebisha.

"Kwa hiyo kama utakutana na mkataba kandamizi, labda tu huyo mtu ameingia bila kuwahusisha wanasheria lakini hilo suala la utoaji wa mikataba kandamizi tumekuwa tukilipigia kelele mara kwa mara.

"Kama kuna malalamiko, ofisi yangu ipo wazi muda na saa yoyote, mimi nikiona shida, ninakwenda kuchukua hatua kama kuna watu wanafanya ovyo.

"Nitoe rai kwa waajiri wote nchini walinde maslahi ya waajiriwa, itakapobainika mwajiri amekiuka masharti, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake. Kwa sasa tupo macho katika hili, hatulali!" Katambi anaonya.

Kuhusu hoja mahususi ya ukandamizaji katika mikataba ya bodaboda, Naibu Waziri Katambi anasema wameweka mikakati endelevu ya kulilinda kundi la vijana waliojiajiri na kuajiriwa kwenye biashara hiyo.

"Tatizo la mikataba kandamizi kwa bodaboda lipo. Kikubwa, wanapaswa kuwa makini, wasiingie mikataba kandamizi, mkataba hautakiwi kumbana mtu, unatakiwa kuwa na mizani sawa.

"Na ikitokea amevunjiwa mkataba kinyume cha makubaliano, anaweza kwenda mahakamani kwa ajili ya kufungua kesi ya madai. Baada ya hapo, hatua zitachukuliwa na ikibainika bosi ana kosa, atalazimika kumlipa fidia mfanyakazi wake.

"Kingine, mkataba ukiwa haufai unaweza kuukataa. Na kama ukiukubali ukagundua ni mkataba kandamizi, kuna hatua za kuchukua. Tunazo ofisi za maofisa kazi mkoa, zipo kila mkoa, tuna Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), vyama vya wafanyakazi vinavyosimamiwa na chama cha wafanyakazi wa viwanda, biashara, taasisi za fedha, huduma na ushauri (TUCTA).

"Unaweza ukaenda na mkataba wako kutoa malalamiko pale na utasaidiwa kwa sababu hizo ofisi zinashughulikia hiyo mikataba, unakwenda unauonyesha, unawaambia huu ninaona ni mkataba kandamizi, wao watajua namna ya kukusaidia," anasema.

Katambi pia anasema vyama vya wafanyakazi, kikiwamo cha bodaboda wenyewe, vinaweza kutumika kama maeneo mahususi ya kuwasilisha malalamiko ya aina hiyo.

"Serikali ina mpango wa kuangalia namna ya kuwakopesha bodaboda kwa riba nafuu ili kumaliza utata unaojitokeza kila siku kati yao na mabosi wao," Katambi anawasilisha mikakati ya serikali.

**USULI**

Inaporejewa historia ya bodaboda nchini, inaanzia mwanzoni mwa miaka ya 2000 pale aliyekuwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Wilfred Lwakatare alipowasilisha hoja mahusus bungeni kuitaka serikali kuruhusu matumizi ya pikipiki za kubeba abiria kibiashara.

Ikumbukwe kwamba kipindi hicho, ubebaji abiria kwa pikipiki haukuwapo, bali utaratibu huo ulikuwa ukishuhudiwa zaidi Uganda, hasa mpakani mwa Kenya na Uganda.

Katika mazungumzo na Nipashe hivi karibuni mkoani Dar es Salaam, Lwakatare alikumbusha kuwa kwenye Mpaka wa Tanzania na Uganda (Mutukula), usafiri huo wa pikipiki ulikuwa zaidi ukiwavusha wafanyabiashara wa magendo ya bidhaa mbalimbali kutoka pande zote mbili.

"Kwa kuwa usafiri huu uliwasafirisha abiria wao toka upande mmoja wa nchi (border) na kuvuka kwenda upande wa nchi nyingine (other boarder), usafiri huo wa pikipiki ukapewa jina la bodaboda, yaani 'border to border'.

"Jina hilo limekuwa maarufu na kutumika hivyo hivyo hata kwa maeneo yasiyo na mpaka kati ya nchi na nchi. Limechukuliwa kama jina linaloakisi usafiri wa kukodi pikipiki.

"Biashara hii ya usafiri wa pikipiki ilichangamkiwa sana na vijana wa upande wa Tanzania pale Mutukula na kwa kasi wakaingiza aina hiyo ya usafiri wa pikipiki kibiashara mpaka mjini Bukoba ambako ni jimbo nililolokuwa nikiliwakilisha bungeni.

"Biashara hiyo ilikumbwa na tatizo la kuzuiliwa na vyombo vya dola (polisi) na Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa kutokuwapo sheria ya kuruhusu pikipiki kubeba abiria kibiashara na pia malalamiko makubwa ya wafanyabiashara wa Taxi ambao waliona wameingiliwa kibiashara.

"Vijana wengi waliojitosa katika biashara hiyo ya bodaboda, walipigwa na polisi barabarani, kumizwa na kuangushwa barabarani na kuumia vibaya sana kwa kufukuzwa na magari ya polisi.

"Wengi walinyang'anywa pikipiki zao na kurundikwa kwa mamia kwenye Kituo cha Polisi Bukoba. Hospitali ya Mkoa Kagera kuna wodi ilijaa vijana walioumizwa au kuvunjika kwa kuanguka na pikipiki zao pindi walipokuwa wakifukuzana na polisi barabarani.

"Kama mbunge, niliona kuna haja kuingilia kati jambo hilo. Kwanza, pamoja na vurugu zote hizo, vijana hawakutaka kuiacha biashara hiyo kwani ilikuwa ikiwaingizia kipato.

"Hata walipokuwa wakinyang'anywa pikipiki hizo, haraka sana walikuwa wakiingiza pikipiki nyingine toka Uganda, zikijulikana kama bomba mbili.

"Usafiri huo ulionekana kupendwa na kuwavutia watu wengi kwa kuwa ulikuwa wa bei rahisi na uliweza kuwafikisha abiria mpaka milangoni mwa makazi yao.

"Niliwasilisha hoja bungeni nikiambatanisha na picha nyingi za majeruhi hospitalini na rundo la pikipiki kituo cha polisi. Na kwa kuwa kilikuwa kipindi cha bajeti, nikaishikilia shilingi ya mshahara wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi (wakati huo alikuwa Omar Mapuri).

"Nikaitaka serikali itoe maelezo juu ya unyanyasaji huo wa raia na pia kuitaka kuleta marekebisho ya sheria na kanuni kuhusu vyombo vya kubeba abiria barabarani na pia Sheria za Usalama Barabarani.

"Nimshukuru Spika (Pius) Msekwa alikuwa 'very much concerned' (aliguswa) na hoja yangu na kiti chake kikaungana nami kuibana serikali juu ya hoja hiyo. Bila ajizi, wizara husika ikiwamo ile ya Mawasiliano na Uchukuzi iliyokuwa ikiongozwa na Profesa (Mark) Mwandosya na ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya Mheshimiwa Mapuri, wakakubali kwenda kukaa na kufanya marekebisho ya sheria na kanuni.

"Huo ukawa mwanzo wa mfumuko wa uingizwaji nchini maelfu ya kontena za pikipiki toka China na biashara ya usafiri wa bodaboda ikashamiri nchi nzima, vijijini, vitongojini na mitaani.

"Hoja yangu moja tu ikatoa fursa ya kimapato kwa mamilioni ya watu; China hadi Tanzania. Ndani ya Bunge, ilifikia mahali kila nikisimama kuchangia hoja yoyote ninaitwa 'Mheshimiwa wa Bodaboda, ni muda wako wa kuchangia'.

"Ukweli ninajivunia kitu hiki hadi leo. Nikiona vijana nchi nzima wakikata mitaa barabarani wakisaka riziki, wao wanasema 'kula vichwa', bila bughudha, ninajisikia fahari na furaha kubwa," Lwakatare anasimulia kilichojiri.

# Mpango kuwachukulia hatua viongozi waharibifu mazingira

**Na Elizabeth Zaya,** IRINGA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema serikali inafanyia kazi taarifa za baadhi ya viongozi kudaiwa kuhujumu hifadhi za mazingira na vyanzo vya maji kwa maslahi binafsi na kuwachukulia hatua kwa kuzingatia misingi ya haki.

Pia amewaagiza viongozi wote wa mamlaka za mabonde nchini, kuwabomolea wote waliojenga na kuziba Mto Ruaha Mkuu bila kibali kwa gharama zao wenyewe huku akiagiza kupatiwa majina ya wote waliopewa vibali vya kujenga katika hifadhi hiyo.

Dk. Mpango alitoa kauli hiyo jana mkoani hapo wakati akifungua kongamano la wahariri na wadau wa uhifadhi, mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji lililoandaliwa na Kituo cha Wanahabari Watetezi wa Rasilimali na Taarifa (MECIRA).

Awali, akiwasilisha taarifa ya hali ilivyo katika vyanzo vya hifadhi za maji na mazingira, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Ruaha, Godwell Ole Meing'ataki, alisema hali ni mbaya katika vyanzo vya hifadhi za maji na mazingira na baadhi ya wawekezaji wakubwa waliojenga katika Mto Ruaha na kuziba na haijulikani waliowapatia kibali cha ujenzi huo.

Meing'ataki alisema baadhi yao hata wanapokamatwa kutokana na kufanya uharibifu huo, huwa wako tayari kutoa fedha nyingi kwa mara moja kwa ajili ya faini na bila 'kukoma' hurudia tena ikiwamo kuingiza mifugo hifadhini.

"Tumekuwa tukipata fedha nyingi kwa kuwatoza faini wanaoharibu vyanzo vyetu ikiwamo kilimo na kuingiza mifugo, lakini kinachoshangaza wako tayari kulipa faini kwa wakati mmoja na kurudia tena kosa."

"Siku moja tena ilikuwa mwisho wa juma, mtu mmoja akakamatwa anaingiza mifugo ndani ya hifadhi, alipigwa faini Sh. milioni 80, lakini alizilipa ndani ya muda mfupi siku hiyo hiyo, hii inashangaza, tunaona suluhisho sio hiyo faini kwa sababu ni kweli tunakusanya fedha, lakini hifadhi zetu zinaharibiwa vibaya."

Makamu wa Rais alisema haamini kama wanaofanya uharibifu huo ni watu wa kawaida na endapo serikali itabaini kuna viongozi walio nyuma ya hilo, watachukuliwa hatua kali.

"Mengine mliyoniambia mniachie, nimeyachukua, serikali nayo inasimamia haki, tutayafanyia kazi haya na tutachukua hatua, hii vita ni kubwa lakini tutashinda. Hatuwezi kukubali na kuvumilia viongozi wa namna hii."

"Hata hao wakubwa watatu wanaodaiwa kuchepusha maji kwenye vyanzo vya maji, tutashughulikia, kwa hiyo viongozi wa namna hii, wa maslahi ambao wanaweka maisha na maendeleo ya Watanzania rehani hawafai."

Dk. Mpango aliagiza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na mikoa inayohusika kuweka mpaka katika Mto Ruaha kukamilika mara moja.

Pia aliomba mamlaka zinazohusika na hifadhi za maji, kumpelekea ripoti inayoonyesha matumizi halisi ya maji.

Aliomba waandishi wa habari kufanya uchunguzi za kufichua mambo mazuri au mabaya yanayohusiana na utunzaji na uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji ili kunisaidia serikali kuchukua hatua.

Awali Mwenyekiti wa MECIRA, Habib Mchange, alisema tayari baadhi ya timu ya waandishi wa habari waliotembelea baadhi ya vyanzo vya maji ikiwamo Mto Ruaha Mkuu, wamefanya uchunguzi na kubaini namna watu wanavyoharibu vyanzo hivyo katika sekta za kilimo, uvuvi na ukataji miti.

Mchange alisema waandishi wa habari watashirikiana na serikali kufichua hujuma zote zinazofanywa na baadhi ya watu kwa maslahi yao binafsi kuharibu hifadhi za mazingira na vyanzo vya maji kwa kuwa athari zake zinamgusa kila Mtanzania.



Mtaro uliojengwa kwa ajili ya kupitisha maji ya mvua eneo la Kilimani Manzese Dar es Salaam ukiwa umejaa majitaka baada ya wakazi wa eneo hilo kudaiwa kuchepusha maji ya vyooni kwenye mtaro huo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Familia ya marehemu Balali yalalamika uvamizi shamba la uwekezaji

**Na Idda Mushi,** MLIMBA

FAMILIA ya aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), marehemu Daudi Balali imeiomba serikali kuingilia kati kuwazuia watu waliovamia shamba lao la ekari 2,000 wanalolimiliki kihalali kwa kulima na kujenga nyumba za kuishi.

Familia ya Balali ilinunua shamba hilo kwa ajili ya uwekezaji katika Kijiji cha Merela, Kata ya Chita, Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba mkoani Morogoro na imeshindwa kuendelea na shughuli za uwekezaji ikiwamo kilimo cha mpunga kwa miaka minne sasa kutokana na kikundi cha watu kuvamia na kuanzisha mashamba na hata kujenga nyumba za kuishi.

Akizungumza kwa niaba ya familia ya mwekezaji huyo ambaye ni mke wa marehemu Daudi Balali, Anna Muganda Balali, msimamizi wa shamba hilo, Mussa Christopher, alisema wanamiliki shamba hilo la ekari 2000 kihalali, licha ya kesi mbalimbali zilizofunguliwa na baadhi ya wavamizi katika mamlaka mbalimbali na familia hiyo kushinda.

Msemaji huyo wa familia ya Balali aliiomba serikali kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wa ndani dhidi ya wanaowakwamisha kwenye shughuli za uwekezaji kwa sababu wakiwekeza wananufaisha wananchi wanaowazunguka kwa ajira na fursa zingine, kulipa kodi na kukuza uchumi wa nchi.

Alisema licha ya vurugu zinazoendeleaa mara kwa mara, mwaka jana waliamua kutoa ekari 500 katika shamba hilo serikali ilipime na kuwapa wananchi kupitia serikali ya kijiji, lakini kundi lingine la watu takribani 20 wakiwamo wavamizi kutoka nje ya kijiji walizuia kwa kufanya vurugu.

Agosti 6, mwaka jana, walidaiwa kuchoma moto gari aina ya Land Cruizer mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, pikipiki nne za viongozi wa vijiji walioambatana kwenda kwenye upimaji huo akiwamo Mwenyekiti wa kijiji, Felician Lisakagu, Mwenyekiti wa kitongoji, Evarist Lilonoka, Kaimu Mtendaji wa kijiji na Mwakilishi wa familia ya Balali, walioongozana na watendaji wa halmashauri akiwamo Ofisa Mipango Miji na vijiji wa halmashauri, Remigi Lipiki, maofisa ardhi na mgambo watatu. Watu hao pia walichoma vifaa vya upimaji wa ardhi, simu na fedha zilizokuwa kwenye gari kwa ajili ya kuwalipa posho watu waliokuwa wakipima pamoja na mali zingine na kumjeruhi dereva wa gari hilo la halmashauri lililochomwa moto ambaye alitibiwa na kuruhusiwa.

Kikundi hicho pia, kimedaiwa kuchochea vurugu, kunyang'anya bunduki ya mlinzi wa shamba na kutoa taarifa za uongo za madai kwamba shamba hilo wanalimiliki kihalali bila kuwa na hati za umiliki.

Sakata hilo lilisababisha kufikishana mahakamani na kufunguliwa kwa kesi namba 3 ya mwaka 2022 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kanda ya Morogoro, mbele ya Jaji Kalunde dhidi ya mwekezaji huyo na mahakama ilitupilia mbali shauri hilo na kutaka mwekezaji aendelee na uzalishaji baada ya kukosekana ushahidi.

"Baada ya kutupiliwa mbali kwa shtaka la awali, walifungua shauri jingine namba 10 la madai la mwaka 2022 mbele ya jaji Kwembe wakiwa watu 52 ambapo shauri hilo liliendelea mpaka tarehe 6 mwezi 10 na mahakama ilisema mwekezaji hana kesi yoyote ya kujibu wala kushtakiwa, kualalamikiwa wala ya kudaiwa na mahakama haiwezi kumhoji chochote na mtu yeyote nje ya mahakama haruhusiwi kumhoji chochote," alisema Mussa.

Hata hivyo, alidai mawakili wa upande wa washtaki waliomba marekebisho na wakati yakiendelea mawakili hao walikuja na malalamiko kwamba wateja wao wananyanyaswa kwa kufanyiwa vitendo vya kikatili na Jeshi la Polisi, mahakama iliwaambia kuwa Jeshi la Polisi ni lazima liendelee na kazi yake kwa kuwa kuna mali za umma zimefanyiwa uharibifu.

Alisema vurugu hizo za mara kwa mara zimefanya mwekezaji kushindwa kuwekeza kwa wakati na kuikosesha serikali mapato kutokana na kodi mbalimbali walizotakiwa walipe katika kipindi chote cha uzalishaji.

Mwenyekiti mstaafu wa kijiji cha Merela, Dionis Ondole, aliyeshiriki utoaji wa eneo hilo kwa aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu Marehemu Balali, alisema wavamizi hao ni wabishi kwa kuwa serikali imekuwa ikiwafahamisha kwa muda mrefu kwamba eneo hilo ni la mwekezaji bila mafanikio. Mjumbe wa serikali ya kijiji hicho, Simon Nicholaus, alisema hali kwa sasa ni mbaya kutokana na fujo kwenye shamba hilo wakidai ni mali yao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, SACP Fortunatus Musilimu, alikiri kukamatwa na kushikiliwa kwa watuhumiwa watano wakiongozwa na Nkumbi Malashi Holela, wanaodaiwa kuhusika na uchomaji moto gari ya halmashauri, pikipiki, vifaa vya upimaji ardhi na mali zingine wakati wa upimaji wa ardhi iliyotaka kumegwa kupewa wananchi.

Pia wanatuhumiwa kupora silaha ya mlinzi wa shamba la Balali, ambayo ilikamatwa, pamoja na kutoroka dhamana katika kesi ya awali.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bwawa la Umeme la Julius Nyerere litimize ndoto ya TZ

**WAGENI** 2,300 wanatarajiwa keshokutwa kushuhudia ufunguzi wa lango la handaki mchepuko katika Bwawa la Umeme la Julius Nyerere kuruhusu maji yaanze kuingia.

Hatua hiyo imeanza kuleta matumaini ya mradi huo kutimiza ndoto ya Tanzania kuondokana na tatizo la umeme.

Mradi huo unaotarajiwa kukamilika Aprili 2024 utakuwa na thamani ya Sh. trilioni 6.65.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ndiye anayetarajiwa kufungua lango la handaki mchepuko katika bwawa hilo Desemba 22, mwaka huu, ili kuruhusu maji kujaa.

Kati ya wageni watakaoshuhudia tukio hilo ni 300 kutoka Serikali ya Misri ambao wataambatana na Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo.

Kwa mujibu wa Waziri wa Nishati, January Makamba, ujenzi wa bwawa hilo umefikia asilimia 78.68 ambayo ni hatua ya awali ya kuanza kujaza maji na inategemewa kuchukua misimu miwili ya mvua. Kwa hakika Watanzania wengi wanausubiri kwa hamu mradi huo uanze kufanyakazi ili nchi yao iondokane na adha ya kukatika umeme mara kwa mara na mgawo ambao hurudisha nyuma shughuli za maendeleo.

Nchi yoyote iliyosonga mbele kimaendeleo lazima inakuwa na nishati ya umeme na maji ya uhakika.

Mwekezaji yeyote anayetaka kuwekeza katika nchi anayotaka kufanya biashara lazima kwanza awe na uhakika wa umeme na maji kwa sababu hivyo vyote vina umuhimu katika uendeshaji wa viwanda. Alipokuwa akiwaelezea wahariri na waandishi wa habari waliotembelea mradi huo hivi karibuni, Waziri Makamba, alisema mageti ya kuziba mchepusho yameshawasili na yameshafungwa ikiwa ni hatua tatu muhimu zilizofanyika katika utekelezaji wa mradi huo.

Rais Samia akifika kwenye mradi huo atabonyeza kitufe ambacho kitashusha geti la kuziba handaki lililokuwa linachepusha maji na kwa tukio hilo maji yataanza kujaa kwenye bwawa.

Hatua hiyo inakwenda kujibu mijadala ya baadhi ya watu waliokuwa na wasiwasi kwamba mradi huo hautokamilika kwa muda uliopangwa na pia uwezekano wa kujaza maji kama utawezekana kutokana hali ya ukame inayoendelea.

"Kuna watu walikuwa wanauliza ninyi watu wa serikali, tena wengine wakasema ninyi watu wa CCM, kuna ukame ambao kila siku mnalalamika ambao ndio chanzo cha upungufu wa umeme inakuwaje tena mnajenga bwawa kuzalisha umeme kwa maji ambayo kila siku mnalalamika ukame, kwanini msiache na kufanya mambo mengine," alinukuu Makamba baadhi ya watu waliokuwa wakihoji kuhusu mradi huo.

Alisema kuna aina mbili za kuzalisha umeme kwa kutumia maji, hatua ya kwanza maji yanakuja kwenye mto na yanatiririka moja kwa moja kwenye mitambo na kujengewa eneo la kukusanywa halafu yanaendesha mitambo.

Hatua nyingine ni kujenga bwawa na kuyakusanya maji mengi na kuyaingiza kwenye mitambo halafu yanazungushwa na kuzalisha umeme kama inavyofanyika katika Bwawa la Mtera.

Linapojengwa bwawa na kujazwa kama la Nyerere, mvua hata isiponyesha kwa miaka mitatu na lisitokee tone hata moja, bado kutakuwa na uwezo wa kuzalisha umeme kwa sababu maji yamehifadhiwa.

Bwawa hilo lina uwezo wa kuhifadhi lita bilioni 33.2 za maji na kama zikitumika na mitambo yote itaweza kuendesha kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Ujazaji wa bwawa hilo unakadiriwa kuwa wa misimu miwili ya mvua. Mwezi Desemba mvua ndogo za vuli na za masika mwezi Machi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Marufuku hii ipunguze ukatili

**VITENDO** vya ukatili shuleni kama ulawiti, ni miongoni mwa matukio ambayo yamechangia kuumiza kisaikolojia na kimwili baadhi ya wanafunzi na mara kwa mara yanatajwa na kupigiwa kelele na wanaharakati kuwa ni kitisho, safari hii serikali imetoa angalizo.

Kuwapo kwa ukatili kulishawahi kumwibua Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima na kutaka mashirika yasiyo ya serikali kutembelea shule kupata maoni ya wanafunzi.

Ukatili huo unashamiri kwenye taasisi za elimu kuanzia msingi na hata vyuo vikuu na hilo ni jambo linaloelekea kuharibu hatima zao kiafya, kisaikolojia na mwenendo wa maisha iwapo watakutana na unyanyapaa na unyanyasaji.

Miongoni mwa ukatili ambao umekuwa ukitajwa kufanyika kwenye baadhi ya shule, ni wanafunzi kulawitiwa na wenzao wanaodaiwa kuwa ni wababe wenye nguvu wanaotumia misuli yao kuwanyanyasa wenzao.

Lakini waziri akawageukia baadhi ya wazazi na walezi kwamba wanawaachia watoto wanatazama vitu vibaya na kusababisha waende kujaribu kwa wenzao bila kujua kama wanafanya ukatili unaoweza kuwatupa jela kwa miongo kadhaa.

Kutokana na kauli hiyo, ninadhani jambo lingine la kuangalia zaidi ili kupunguza ukatili huo, ni mtindo wa wanafunzi wa bweni kulala wawili kitanda kimoja kitendo ambacho kinaweza kusababisha kuwapo ukatili huo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amepiga marufuku mtindo huo katika Mkutano Mkuu wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSA) jijini Dodoma na kuahidi kufuatilia hilo.

Hata hivyo, hakufafanua sababu za kupiga marufuku hiyo, lakini ni muhimu pia jamii kujiongeza na kutambua kuwa dunia ya sasa imebadilika, wanafunzi wamekuwa wafanyiwa na kufanyiana ukatili huo.

Kwa maana hiyo kuendelea kuwalaza wawili kwenye kitanda kimoja, kunaweza kuchochea vitendo vya ukatili vikiwamo vya kulawitiana ambavyo

**Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amepiga marufuku mtindo huo katika Mkutano Mkuu wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSA) jijini Dodoma na kuahidi kufuatilia hilo.**

kimsingi ni hatari kwa afya zao na hata maendeleo yao kielimu.

Waziri anawataka wakurugenzi wa halmashauri kuhakikisha shule zote zinakuwa na vitanda vya kutosha, na kwamba wasithubutu kutumia fedha katika maeneo mengine na kulaza wanafunzi kitenda kimoja.

Ninaunga mkono marufuku ya Prof. Mkenda, kwani inaweza kupunguza ukatili shuleni au vishawishi vya wanafunzi kufanyiana vitendo hivyo, hasa kutokana na ukweli kwamba mazingira hayo ni salama kwao.

Hivyo, wakati wazazi na walezi wanapowapeleka watoto wao katika shule za bweni, ni vyema nao wakafuatilia ili kujua mazingira wanayolala kwani mategemeo yao ni kuona maisha ya watoto yao yanakuwa mema.

Kwa maana hiyo, nidhani ni muhimu shule zitoe huduma za bweni kwa wanafunzi, huku kukiwa na tahadhari kama alivyofanya Waziri wa Elimu, ili kuhakikisha kwamba hawawezi kufanyiana vitendo vya ukatili.

Kama ambavyo imekuwa ikihimizwa kwamba wazazi na walezi wasiruhusu watoto wao walale na wageni nyumbani, ni vyema hilo pia lifanyike katika shule za bweni kwa wanafunzi wawili kutolala kitanda kimoja.

Siyo vibaya wazazi na walezi wakafuatilia kwa karibu maendeleo ya watoto wao shuleni lakini kujua mazingira wanayolala badala ya kuridhika tu kwamba wako bweni na kumbe wanafanyiana vitendo vya ukatili.

Pamoja na hayo, ni vyema kuimarisha klabu za wanafunzi za kupinga ukatili shuleni, ili wawe wanaelimishana na kupeana mbinu zitakazowawezesha kuepuka kufanyiana ukatili au kufanyia wengine vitendo hivyo.

Ni vyema wanafunzi waelewe umuhimu wa kuheshimiana na pia kuheshimu walimu na jamii inayowazunguka, lakini kikubwa wasilazwe kitanda kimoja wawili, kwani mazingira hayo si salama kwao.

## Kesi ya Kocha wa Makipa wa Simba yapigwa kalenda

**Na Kulwa Mzee**

KESI ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroine kilogramu 34.89 inayomkabili aliyekuwa Kocha wa Makipa wa Klabu ya Simba, Muharami Seltani na wenzake, imeahirishwa hadi Januari 2 mwakani kutokana na upelelezi kutokamilika.

Shauri hilo liliahirishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mario baada ya Wakili wa Serikali Carolina Matemu kudai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na akaomba tarehe nyingine.

Mahakama ilikubali maombi hayo na kuahirisha kesi hiyo hadi Januari 2, mwakani.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mmiliki wa Kituo cha Cambiasso Sports Academy kilichoko Tuangoma wilayani Kigamboni kinachojihusisha na ukuzaji wa vipaji kimichezo, Kambi Seif.

Wengine ni Maulid Zungu, maarufu Mbonde, Said Abeid ambaye ni fundi Selemala, John Andrew, maarufu Chipanda, mfanyakazi wa Kituo cha Cambiasso na Sara Joseph.

Washtakiwa wanadaiwa kuwa Oktoba 27, mwaka huu, eneo la Kivule, Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, walikutwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya heroine kilogramu 27.1.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Novemba 4, mwaka huu, eneo la Kamegele Mkuranga mkoani Pwani, kwa pamoja walikutwa wakisafirisha kilogramu 7.79 za dawa za kulevya aina ya heroine.



Wafanyabiashara wa soko kuu la mboga wilayani Muheza mkoani Tanga wakiendelea na biashara zao jana kuwauzia wateja bidhaa kuelekea Sikukuu ya Krismasi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Korti yaagiza uchunguzi mwili aliyekufa mikononi mwa polisi

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam imetoa amri ufanyike uchunguzi wa kifo cha Stella Moses aliyefia kwenye Kituo cha Polisi Mburahati kwa madai kuwa alijinyonga, baada ya kubaini kifo chake kilitokea katika mazingira ya kutatanisha.

Machi 22, mwaka huu, shemeji wa marehemu, Emmanuel Kagongo alifungua shauri dhidi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni na Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kipolisi Mburahati.

Wajibu maombi wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), akiomba ufanyike uchunguzi huru ili kujua ukweli wa mazingira ya kifo cha shemeji yake Stella.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Franco Kiswaga wa mahakama hiyo baada ya kupitia maombi yaliyowasilishwa na Kagongo pamoja na viapo vya wajibu maombi watatu kati ya sita.

Hakimu Kiswaga alisema alipitia kiapo cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hospitali ya Taifa Muhimbili na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni na kubaini kuwa kulikuwa hakuna ubishi kama Stella Desemba 20, 2020 alifia kwenye Kituo cha Polisi Mburahati.

Pia alisema kibali cha mazishi kinaonyesha tarehe hiyo na ni eneo gani ambalo Stella alifia, hivyo mahakama inalo jukumu la kutoa amri ya kufanyika uchunguzi wa mwili.

"Kwa sababu sheria inasema kama mahakama itaona shaka, basi itatakiwa itoe amri ya kufanyika kwa uchunguzi," alisema Kiswaga.

Alisema hakuna ripoti yoyote iliyotolewa ya polisi au ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuonyesha kuwa kuna sampuli zilichukuliwa kwa ajili ya uchunguzi wa mwili wa marehemu Stella.

Pia alisema mahakama haijapata ripoti ya taarifa ya kidaktari ya chanzo cha kifo cha marehemu Stella, hivyo maombi ya mleta maombi yana mashiko kisheria ya kutaka ufanyike uchunguzi huru kujua ukweli wa mazingira ya kifo hicho.

"Mahakama inaamuru ufanyike uchunguzi kuhusiana na kifo cha Stella kilichotokea katika mazingira ya kutatanisha akiwa chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi Desemba 20, 2020 katika Kituo cha Polisi Mburahati.

"Na taarifa hiyo itolewe kwa mahakama na sehemu husika na yeyote aliyehusika achukuliwe hatua za kisheria. Kwa hiyo, maombi ya mleta maombi yamekubaliwa," alisema Hakimu Kiswaga.

Hakimu huyo alisema pande zote mbili zilikubaliana kwamba shauri hilo litaendeshwa kwa njia ya maandishi, lakini hadi anatoa uamuzi huo hakuna hata mjibu maombi aliyewasilisha hoja za maandishi mahakamani huko.

Kwa mujibu wa hati ya kiapo chake, Kagongo anadai kuwa Desemba 28, 2020 Idara ya Vizazi na Vifo kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili ilitoa kibali cha mazishi kwa Eliud Ernest Kagongo chenye namba 1097179 kuridhia mazishi ya mwili wa Stella Moses.

Hata hivyo, anadai kibali hicho cha mazishi hakikubainisha sababu za kifo cha shemeji yake, bali kilieleza tu kuwa uchunguzi wa kimaabara ulikuwa unasubiriwa na kwamba mpaka anafungua maombi hayo, hakuna taarifa ambayo ilishatolewa.

Awali Wakili wa familia hiyo, Peter Madeleka alipinga kiapo kinzani cha Mkuu wa Jeshi la Polisi na wenzake katika shauri la maombi namba 3/2020 ya uchunguzi wa kifo cha mwanamke huyo, akidai kuwa kimewasilishwa mahakamani kinyume cha utaratibu.

Ilidaiwa kuwa Stella alikwenda kwenye kituo hicho cha polisi alikojisalimisha baada ya kupata taarifa kuwa alikuwa anahitajika na polisi walidai alijinyonga akiwa mahabusu, lakini ndugu wa marehemu waliopinga taarifa hiyo, walidai kuna utata wa kifo hicho.

**NJE YA MAHAKAMA**

Wakili Peter Madeleka alidai waliwasilisha maombi mahakamani ili mwili wa marehemu ufukuliwe na kufanyiwa uchunguzi huru na wa wazi kama sheria ya uchunguzi wa vifo vyenye shaka inavyoelekeza.

Alisema uamuzi huo unakwenda kuleta sura mpya katika haki jinai hasa zinazowahusu mahabusu wanaokamatwa na kuwekwa kwenye vituo mbalimbal vya polisi na baadaye kuripotiwa kwamba wamefariki dunia kwa mazingira ambayo yanaacha maswali mengi

"Tunaamini uamuzi huu utakuwa ni funzo kwa Jeshi la Polisi na kwa wengine wote wanaohusika kwenye mfumo wa haki jinai kuhakikisha wanaheshimu haki jinai hasa wale waliyokuwa wametuhumiwa na wapo kwenye vyombo vya dola, jamii imechoshwa na tabia ya kuambiwa waliokuwa wamekamatwa wamekutwa wamekufa," alidai.

Alidai wanatarajia uamuzi huo wa mahakama utaheshimiwa na utakwenda kutekelezwa kama ilivyotolewa ili wajue ukweli wa kifo cha Stella na ili uchunguzi huo ufanyike, mwili huo uliozikwa Goba, utafukuliwa ili ufanyiwe uchunguzi.

## KABWELA

Fadhili Mohamed



RIPOTI MAALUM



Machinga wakiendelea na biashara kwenye Soko la Mwenge, Dar es Salaam juzi. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Kilichojificha machinga wagumu kuondoka masoko ya barabarani

## • Pande zote za wadau zaanika kinachoendelea

**Na Romana Mallya**

"SKETI ya kuombea msamaha kwa mpenzi uliyemkosea, gauni la kwenda nalo kwa mama mkwe akaruhusu kijana wake akuoe siku hiyo hiyo, blauzi ya kumshawishi mkuu wa chuo asikuadhibu kwa kufeli mtihani wake". Ni sauti ya machinga akinadi bidhaa zake.

Hapo ni Soko la Mwenge wilayani Kinondoni, ulingo mmojawapo uliopigwa marufuku kwa biashara hiyo, huku sura ya pili pana mwaka na miezi miwili pako kwenye marufuku ya biashara hiyo, wateja wakuu ni jinsia ya kike.

Ghafla mgambo wanatokea, nao machinga wanaudaka mkasa wakipeana ishara ya miluzi ya hatari, kila mmoja anajitwisha furushi lake na kukimbilia uchochoroni. Hali ya hewa ikitulia, wanarejea kwenye biashara kwa kasi ileile.

Biashara ya machinga iko katika marufuku kitaifa kwenye maeneo yasiyo rasmi ili kukabili uholela katika huduma za miji na athari zake.

Ni majira ya 12 jioni, hivi karibuni, Nipashe ikiangaza mahali hapo, inashuhudia ng'ambo mbili za barabara zinazokatiza eneo la sokoni Mwenge, wenye magari wahangaika kupata maegesho kutokana na pande hizo mbili za barabara kuwa na msongamano mkubwa wa machinga.

Jumanne Ally, mmoja wa machinga hao anayeuza nguo za mitumba karibu na bango linalopiga marufuku kufanya biashara kwenye maeneo hayo, anasema amekuwa hapo kwa muda mrefu kwa kuwa eneo hilo lina wateja wengi.

"Sijaja mjini kuuza sura, nimekuja kufanya biashara ili nihudumie wazazi wangu na wadogo zangu niliowaacha kijijini.

"Nipo hapa kwa kuwa kuna mzunguko wa biashara, ninafungua mzigo wa nguo kila jioni wateja wanamiminika, ninapata riziki, sasa ukiniambia nichague kubaki au kuondoa, nitabaki hapa, siyo kule kusiko na wateja," Ally anasema.

Anawasilisha kilio cha machinga ni mgambo kuchangia kupoteza na hata kuharibu bidhaa zao wanapowaondoa kwa nguvu.

Machinga huyo anarejea uzoefu wake wa miezi mitano sokoni hapo, akisema wanaokamatwa, hurejea kwenye biashara baada ya kulipa faini katika Ofisi ya Kata ya Kijitonyama.

"Shughuli zetu tunafanyia barabarani, kero kubwa ni vumbi, binafsi mara kwa mara nimekuwa nikiumwa mafua, hatuna shida ya choo, wapo wanaotoa huduma hiyo na kuna vyoo vina huduma ya kuoga.

"Hatari nyingine kwa kuwa tunapanga bidhaa pembezoni mwa barabara, kama unavyoona magari yanapita, nyakati za usiku wakati madereva wanapishana wapo wanaokanyaga bidhaa zetu, huwezi kumkoromea maana hujui ni nani, unamwacha tu aende maisha yanasonga," anasema.

Elizabeth Lema aliyekutwa na Nipashe sokoni hapo akinunua nguo za mtumba, anasema kinachosababisha kukimbilia maeneo hayo ni bei ya bidhaa kuwa chini kulinganisha na wauzaji walioko kwenye masoko na maduka rasmi.

Mfanyabiashara wa nguo mwenye fremu sokoni hapo, Joseph Haule anasema: "Kuna wakati mgambo wanapowaondoa walio maeneo yasiyo rasmi, wateja huja huku kwa wingi, shida haipiti muda machinga wanarejea tena."

**UONGOZI SOKONI**

Kiongozi wa Machinga sokoni hapo, Samata Matelephone anasema: "Baada ya bomoabomoa, tulikuja hapa Mwenge kwenye eneo rasmi (barabara ya kwenda kiwanda cha Coca-Cola) machinga zaidi ya 1,000, kwa sasa tuliobaki ni 100, wengine wamerudi barabarani.

"Hii haimaanishi hapa hakuna biashara, hapana! Walioshika maeneo wameyaacha na wengine kudaiwa kuyauza na wao kurejea barabarani," anasema huku Nipashe ikishuhudia baadhi ya fremu na meza sokoni hapo zikiwa wazi.

Anasema tayari walishaliwasilisha suala hilo kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ili kuwaondoa machinga waliobaki kwenye maeneo yasiyo rasmi lakini utekelezaji wake umekumbwa na anachokiita kigugumizi cha watendaji.

"Ukweli ni kwamba operesheni hazifanyiki kwa sababu hakuna vitendea kazi, mgambo wanaofanya kazi, uwezo wa kuwalipa hatuna, lazima serikali itusaidie. Kiongozi huyo ana angalizo lingine kwa mamlaka, akibainisha kuwa baadhi ya vizimba vilivyotolewa sokoni kwa ajili ya machinga, vimekuwa vikitumiwa na watu wasio waaminifu kuuza dawa za kulevya aina ya bangi na suala hilo wameshalifikishwa kwa Jeshi la Polisi kwa hatua zaidi za kisheria.

Pia anakumbusha tukio la miezi miwili iliyopita la mgambo kushambuliwa kwa kupigwa na baadhi ya machinga walio maeneo yasiyo rasmi sokoni Mwenge na kusababisha kulazwa hospitalini.

Halfani Misilei ni miongoni mwa askari wa Jeshi la Akiba (Mgambo) walioshambuliwa na machinga sokoni huko, akipigwa kwa kipande cha tofali kichwani na kulazwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) kwa siku saba.

Anasema madhila hayo yalimpata Septemba 28, mwaka huu, majira ya jioni walipokwenda kuwaondoa machinga sokoni hapo.

"Tuliwakamata na vitu vyao, baadhi walipelekwa Manispaa na wale wakorofi tuliwapeleka Kituo cha Polisi Oysterbay na wengine walipelekwa ofisini kwa Ofisa Mtendaji na kulipishwa faini.

"Kazi hii tuliifanya hadi saa 10 jioni, tulikuwa kama 15 hivi, wakiwamo wanawake wawili kutoka manispaa. Wakati tunataka kubadilisha sare tuondoke, mwenyekiti wa wafanyabiashara akatupigia simu kututaarifu machinga wanarejea, hivyo twende.

"Eneo hilo lilikuwa na jengo limevunjwa, hivyo kulikuwa na matofali yaliyovunjika, nilipoona machinga wameanza kurusha mawe na sisi tulikuwa tumevaa sare za mgambo na hatuna silaha yoyote, tukakimbilia upande wa pili wa barabara kujiokoa.

"Niliongozana na dada wa manispaa, yule dada akapata bahati akafunguliwa geti la kiwanda kimoja kipo pale Mwenge kwenye mataa akaingia, ila mimi walikataa kunifungulia kwa sababu nilikuwa na sare, machinga wangerusha mawe ndani ya kiwanda.

"Kwa kuwa walikuwa wengi wananifuata wakiwa wamebeba vipande vya matofali, nikakimbilia uelekeo wa Coca-Cola, ghafla nilipigwa na kipande cha tofali kichwani upande wa kushoto nikaanguka na sikujua kilichoendelea hadi siku iliyofuata (Septemba 29) nilipojikuta Hospitali ya Taifa Muhimbili, nikaona ndugu zangu pamoja na Ofisa Mtendaji Mazanda ambaye baada ya hapo hakurudi tena," anasema.

Anasimulia kuwa akiwa hospitalini huko, ndugu aliyekuwa akimuuguza, alimweleza kuwa Ofisa Mtendaji huyo alipofika hospitalini kumwona, alituma Sh. 40,000 kama malipo ya kazi aliyofanya siku ya tukio.

"Nimekaa hospitalini kwa siku saba, nikaruhusiwa na kwa sasa ninahudhuria kliniki, mpaka sasa ninagharamia mwenyewe matibabu, nimeshatumia zaidi ya Sh. 300,000 na ninatakiwa kurejea hospitalini Desemba 23," anasema.

Msemaji wa kikundi kingine cha ulinzi ambacho kati yao wamo polisi jamii na itifaki, Amina Maganga anataja ulipo ugumu wa kuwaondoa machinga kwenye maeneo yasiyo rasmi, akitamka:

"Tunapanga kuwaondoa halafu ghafla unasikia kiongozi wa soko hayupo au tunaambiwa gari la manipsaa lililotolewa kwa kazi hii halipo, tunajikuta tunapoteza muda.

"Jukumu kubwa tulilopewa ni kuwaondoa, cha ajabu ukiwaondoa leo, ikifika kesho au siku hiyo hiyo wamerejea.

"Tukiwadodosa wanakwambia kuna baadhi ya viongozi wanajuana nao, mwingine anakwambia 'siwezi kwenda soko rasmi, hapa mnajisumbua' wapo wanaodiriki kutaka kutoa rushwa ili tuwaache."

Anabainisha shida nyingine kwamba licha ya kazi hiyo kuwa hatarishi kwao, hawajalipwa tangu mwezi Septemba mwaka huu kwa kazi walizofanya, akiwataja askari 20 wanaoidai manispaa.

Desemba 14, mwaka huu, Nipashe ilifika kwenye Ofisi ya Mtendaji wa Kata ya Kijitonyama, Boniphace Barnabas kupata ufafanuzi wa madai hayo, naye akirusha lawama kwa baadhi ya wafanyabiashara wenye fremu sokoni hapo kuwa wamekuwa wakichangia kundi hilo kurejea kwa kuwa huwahifadhia mizigo yao.

"Haiwezekani machinga anaishi Goba au Mbagala halafu kila siku aje na mzigo wake, wanahifadhiwa ndiyo maana wanarudi, tumeendelea kutoa elimu kwa wenye fremu wasiendelee kufanya hivyo," anasema.

Uchunguzi wa Nipashe sokoni hapo umebaini mizigo ya wafanyabiashara hao inahifadhiwa kwenye stoo mahususi ambapo kila mzigo hutozwa Sh. 500 kwa siku.

***ITAENDELEA KESHO**

HABARI KITAIFA

# Dawa ya migogoro wafugaji na wakulima yapatikana

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ana mapenzi ya dhati na Sekta ya Mifugo na anatamani kuona inaleta mapinduzi ya kiuchumi kwa kukuza zaidi pato la wananchi, kutoa ajira na kuchangia Pato la Taifa bila kuathiri mazingira na maendeleo ya sekta nyingine.

Kutokana na dhamira hiyo, Waziri Mkuu ameielekeza Wizara ya Mifugo na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya tathmini ya maeneo ya ufugaji yaliyoko kwenye maeneo yao na kiasi cha mifugo kinachoweza kufugwa na endapo mifugo itazidi uwezo wa eneo husika, wafugaji waelekezwe kuvuna mifugo yao.

Majaliwa alitoa maelekezo hayo jana alipofungua mkutano wa siku mbili wa wadau wa Sekta ya Mifugo unaofanyika jijini hapo.

"Wafugaji wahamasishwe kuvuna mifugo yao kwa wakati ili kuwawezesha kupata bei nzuri sokoni pamoja na kupunguza changamoto za malisho hususan wakati wa ukame. Kwa ujumla kasi ya uvunaji wa mifugo nchini bado ipo chini ya asilimia 10 kulinganishwa na viwango bora vya uvunaji wa mifugo kitaifa ambavyo ni kati ya asilimia 20 na 25," alisema.

Waziri Mkuu alizielekeza Wizara ya Ardhi na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe zinashirikiana na wadau wa Sekta ya Mifugo katika kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya vijiji na kutenga maeneo ya malisho ya pamoja, ranchi za vijiji na vitalu kwa ajili ya wafugaji binafsi.

Majaliwa alisema kwa vijiji vyenye ardhi ya kutosha, vitenge maeneo ya ranchi za vijiji zenye ukubwa wa kati ya hekta 200 na 500 zitakazotumika kwa utaratibu wa kuwapanga wafugaji kutoka ndani ya kijiji husika.

"Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo inamiliki Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), ihakikishe maeneo yote ya NARCO yaliyoko kwenye mikoa yetu, wakuu wa mikoa kwanza mtambue maeneo hayo yanamilikiwa na nani na mjue yapo kwenye wilaya gani na yana ukubwa upi na je, matumizi ni sahihi kama serikali inavyotaka?

"Kwa sababu tuna watu binafsi wamechukua ardhi hiyo, kazi yao ni kukodisha watu wengine, tumewaacha wafugaji wenye ng'ombe na tunawajua huyu ana ng'ombe wake 200, huyu ana ng'ombe wake 300 na tuna eneo la NARCO zuri tu badala ya kumpa huyu mwenye ng'ombe tumempa mtu ambaye hana ng'ombe, tumempa mtu ambaye hana ng'ombe halafu anakuja kumpangisha mwenye ng'ombe. Hii wakuu wa mikoa tuikatae wazi," aliagiza.

Pia aliiagiza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na wadau na wafugaji kushiriki kikamilifu katika kuhamasisha mabadiliko ya mfumo wa ufugaji ikiwamo ufugaji wa kukaa kwenye eneo moja bila kuhamahama na wafugaji kulima malisho badala ya kutegemea malisho ya asili peke yake.

Waziri Mkuu pia aliagiza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za mifugo uimarishwe ili kuongeza tija katika sekta hiyo na kuwahamasisha wafugaji kutumia mifugo bora iliyofanyiwa utafiti na kuonyesha kuwa na tija zaidi. Vilevile, Waziri Mkuu aliiagiza Wizara ya Mifugo na Uvuvi ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kutatua migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema lengo la mkutano huo ni pamoja na kuwaleta pamoja wadau wa Sekta ya Mifugo kujadili kwa kina na uwazi kuhusu mwelekeo mpya wa sekta ya mifugo nchini na kuwajengea uwezo wafugaji ili wafuge kwa tija na kibiashara kama wawekezaji kwenye sekta ya mifugo.

Waziri Ndaki alisema Sekta ya Mifugo inakabiliwa na vikwazo mbalimbali, hivyo watatumia mkutano huo kujadili namna ya ufugaji bora pamoja na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Tumepanga namna ya kuwafikia wafugaji na kuwaelimisha juu ya matokeo ya athari hizo kwani sehemu kubwa ya mifugo imeathirika," alisema.




Waziri wa Wizara ya Nishati, January Makamba, akizungumza katika hafla ya utiaji saini wa mikataba ya utekelezaji mradi wa kupeleka umeme maeneo ya pembezoni mwa miji, Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# NMB yatwaa tuzo ya Mwajiri Bora Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

KWA mara nyingine Benki ya NMB imedhihirisha umahiri na ukubwa wake kiundeshaji baada ya kunyakuwa tuzo ya Mwajiri Bora barani Afrika.

Ushindi huo ulitangazwa wiki iliyopita mjini Port Louis, Maurituis ambako NMB ilitunukiwa tuzo hiyo inayotambua umakini katika kuzingatia maslahi na maendeleo ya wafanyakazi na waandaaji wake ambao ni Taasisi ya Ajira ya Employer Branding Institute.

Akipokea nishani hiyo jana makao makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam, Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Filbert Mponzi, alisema tuzo hiyo ya nne ya mwajiri bora mwaka huu, ni ushahidi mwingine wa jinsi taasisi hiyo kubwa ya fedha nchini inavyothamini wafanyakazi wake.

"Thamani ya wafanyakazi kwetu sisi NMB ni kubwa sana kwani wao ndiyo rasilimali inayoongoza na chanzo cha mafanikio yetu yote na tuzo mbalimbali ambazo tumekuwa tunazipata," Mpozi alisema baada ya kukabidhiwa tuzo hiyo na Ofisa Mkuu Rasilimali Watu, Emmanuel Akonaay.

Kiongozi huyo ambaye ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB alisema kuwa baada ya kuongoza karibu kwa kila kitu nchini, sasa wameanza kupata mafanikio barani Afrika.

Alisema kuwa hilo linatokana na NMB kuzingatia matakwa ya msingi ya uongozi na uendeshaji taasisi hasa zile za fedha.

Alisema ushindi wa mwajiri bora unatokana na NMB kutambua umuhimu wa rasilimali watu na kuwekeza katika maendeleo yake. "Rasilimali watu ndiyo mtaji wetu mkubwa na ushindi huu unadhihirisha jinsi tunavyothamini rasilimali hii. Mafanikio haya yanawafanya wafanyakazi wa NMB kujivunia kufanya kazi na mwajiri bora nchini na Afrika," Mponzi alisema kwenye hafla fupi ya kupokea tuzo hiyo.

Aliongeza: "Maana kubwa ya ushindi huu ni kuwa matokeo na mafanikio yote makubwa ambayo NMB inayapata yanatokana na kuzingatia maslahi na maendeleo ya wafanyakazi."

Mbali ya kuwa mwajiri bora, katika miaka miwili iliyopita, NMB imekusanyia zaidi ya tuzo 20 za kimataifa ilizotunukiwa na majarida yanayoheshimika duniani kama vile World Economic Magazine, Global Brands Magazine, International Banker Awards na International Business Magazine.

Kwa mwaka huu, tuzo hiyo ni tuzo ya 21 kwa benki hiyo kuipata ndani na nje ya nchi. Mwezi uliopita, NMB ilinyakua tuzo tatu za mwajiri mahiri kutoka kwa Chama cha Waajiri nchini (ATE), ikiwamo ya Mwajiri Bora wa Mwaka 2022.

Jana Akonaay ambaye ndiye aliipokea tuzo ya Best Employer Brand - Africa huko Mauritius, alisema tuzo hiyo ni mwendelezo wa mambo makubwa ya NMB kwa mwaka huu.

Akizungumza kabla ya kuikabidhi rasmi kwa Mponzi, mtaalamu huyo wa ajira na wafanyakazi alisema heshima waliyopata inazidi kuifanya NMB kutambulika barani Afrika na duniani kote kwa ujumla.

"Mafanikio haya yanafuatia yale yaliyopatikana kutokana na ushindi wa Jasiri Bond na EDGE Certification (cheti maalumu cha kutambulika rasmi duniani kama kinara katika mgawanyo wa kiuchumi kwenye suala la kijinsia)," Akonaay alisema.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa ushindi walioupata unatokana na juhudi za Bodi na Menejimenti ya NMB lakini zaidi wafanyakazi wa benki hiyo.

Alisema NMB imeonyesha kuwa si tu taasisi inayoongoza kwa huduma za kifedha, bali pia ni kinara wa kujali maslahi ya wafanyakazi wake.

"Sisi tunaongoza si tu kwa biashara na huduma bora, bali pia linapokuja suala la rasilimali watu," alisema.

# RUWASA yaokoa mil. 100/- utekelezaji wa mradi wa maji

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

WAKALA wa Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Singida umeokoa Sh. milioni 100 katika ujenzi wa mradi wa maji kwenye Kijiji cha Senene wilayani Mkalama kutokana na kutumia mkandarasi wa ndani.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alibainisha hayo juzi wakati wa uzinduzi wa mradi huo kwenye kijiji hicho ambao makadirio ilikuwa ugharimu zaidi ya Sh. milioni 570 lakini zimetumika chini ya hizo na kuokoa Sh. milioni 100.

Alisema namna bora ya kuishukuru serikali ni kuutunza mradi huo ili udumu kwa zaidi ya miaka 25 na jukumu la kulinda ili usiharibike ni la kila mwananchi.

Serukamba aliagiza RUWASA wahakikishe maeneo yote yanayotoa huduma kwa wananchi wilayani Mkalama kama vile shule, vituo vya afya na polisi, yanapata maji ili kuondoa changamoto ya ukosefu wa maji kwenye maeneo hayo.

Pia aliwataka wazazi na walezi wenye watoto waliofikisha umri wa kwenda shuleni wawaandikishe kabla ya Desemba 30, mwaka huu, ili waanze darasa la kwanza mwakani.

"Ninawaomba wazazi pelekeni watoto wenu wakaandikishwe shuleni, hadi sasa ni asilimia 49 tu ya watoto waliofikia umri wa kuanza shule Mkoa wa Singida ndiyo wameandikishwa," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Sophia Kizigo, alisema kati ya vijiji 70 vilivyoko wilayani hapa, 63 vinapata huduma ya majisafi na salama na hivyo kufanya upatikanaji wa maji kufikia asilimia 80.

Meneja wa RUWASA Wilaya ya Mkalama, Antidius Mchunguzi, alisema mradi huo ulikuwa ugharimu zaidi ya Sh. milioni 569 lakini kutokana na kutumia mkandarasi wa ndani, hadi kukamilika umegharimu Sh. milioni 475.

Mchunguzi alisema kukamilika kwa mradi huo kumeongeza kiwango cha asilimia 1.5 cha upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Mkalama na hivyo utapunguza muda wa upatikanaji wa majisafi na salama kwa wananchi wa Kijiji cha Senene.

Alisema faida nyingine za mradi huo ni kwamba utapunguza migogoro kwenye familia na kuongeza uchumi kwa wananchi.




Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini, Mhandisi Hassan Saidy (kulia), akipokea mkataba kwa Meneja wa Kampuni ya O.K & Electronics Services (katikati), katika hafla ya utiaji saini wa mikataba ya utekelezaji mradi wa kupeleka umeme kwenye maeneo ya pembezoni mwa miji, Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Ufundi, Mhandisi Novatus Lyimo. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Mkuu wa Mkoa apewa tuzo kwa utendaji bora

**Na Mwandishi Wetu** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amepokea hati ya pongezi kutoka kwa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Geita kwa kutambua mchango wake na kuleta mageuzi wakati wa uongozi wake akiwa Mkuu wa Mkoa huo.

Hati hiyo iliwasilishwa jana na Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari wa Mkoa wa Geita, Renatus Masuguliko, aliyefuatana na Katibu wake, Novatus Lyaruu.

Masuguliko alisema kwa takribani mwaka mmoja ambao Senyamule amekuwa mkoani Geita, amefanikiwa kuleta mabadiliko chanya kwenye sekta zote na kumpongeza kwa kusimamia kwa vitendo kaulimbiu aliyoianzisha ya 'Geita ya dhahabu, utajiri wa heshima'.

"Mkuu wetu wa Mkoa, Mheshimiwa Senyamule alivyokuja na hii kaulimbiu, mwanzoni hatukumwelewa, lakini kwa kipindi kifupi amefanya mengi katika sekta za elimu, afya, miundombinu, maji, uchumi na uzalishaji, hivyo watu wa Dodoma mna bahati ya kupata kiongozi mahiri," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary alikishukuru Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Geita kwa kumpa tuzo ya heshima kwa kutambua mchango alioutoa akiwa Geita.

Aliupongeza uongozi wa chama hicho kwa kuwa mstari wa mbele katika kufanya kazi kwa weledi na maarifa na kusisitiza kuwa kazi hiyo iwe endelevu ili jamii inufaike na kufahamu mambo ambayo serikali imekuwa ikitekeleza katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Dodoma, Mussa Yusuph na Katibu wake, Ben Bago walifuatana na ugeni huo kutoka Geita, wakisema jitahada zinaendelea ili Makao Makuu ya Muungano wa Vyama vya Waandishi wa Habari Tanzania yahamie kwenye Mkoa wa Dodoma.

# Wahariri wawaangukia wabunge mabadiliko ya Sheria ya Habari

**Na Mwandishi Wetu**

WAJUMBE wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) wamewaomba wabunge waondoe tofauti zao bungeni ili wafanikiwe kupitisha sheria nzuri baada ya kuifanyia marekebisho Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 pindi muswada wa mabadiliko ya sheria hiyo utakapowasilishwa bungeni.

Wamesema kama wabunge watatimiza wajibu wao ipasavyo kwa kujadili kwa kina sheria hiyo, Tanzania itafanikiwa kuwa na sheria nzuri itakayowafanya waandishi wa habari watimize wajibu wao bila hofu.

Wahariri hao waliyasema hayo mwishoni mwa wiki walipozungumza na waandishi wa habari baada ya kauli ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, kwamba Januari mwakani, serikali itawasilisha bungeni muswada wa mabadiliko ya sheria hiyo.

Nape alitoa kauli hiyo alipozungumza jijini Dar es Salaam Jumamosi wakati wa Kongamano la Maendeleo ya Sekta ya Habari lililokutanisha waandishi wa habari pamoja na wadau wa habari zaidi ya 1,000.

Mhariri wa Gazeti la Raiamwema, Joseph Kulangwa, alisema wabunge wana nafasi kubwa katika kutunga sheria nzuri pindi watakapokuwa wakijadili muswada huo kwa kina na kwa ushirikiano wa hali ya juu.

"Sisi wahariri na waandishi wa habari kwa ujumla wetu, tumekuwa tukiichambua sheria hiyo kwa kipindi kirefu na kueleza kwa kina maeneo yenye utata na ambayo yanatakiwa kufanyiwa mabadiliko. "Tumefanikiwa kuyafanya hayo kwa sababu tuliisoma sheria hiyo na tuliichambua kwa ushirikiano kama mchwa wanavyofanya kazi.

"Kwa kuwa sasa serikali imesema itawasilisha bungeni muswada wa mabadiliko ya sheria hiyo, mpira sasa unatakiwa kuchezwa kwa umakini na waheshimiwa wabunge.

"Katika hilo, wabunge ambao tunaamini ni makini, ninawaomba waisome kwanza sheria tunayolalamikia kisha waelewe msingi wa malalamiko yetu ili watakapoanza kujadili muswada huo Januari, wawe na mwanga mpana wa ni kitu gani kinalalamikiwa na ni kipengele gani kinatakiwa kiondolewe.

"Binafsi ninaamini kama waheshimiwa wabunge watatimiza wajibu wao sawasawa kwa jinsi tunavyowafahamu na kuwaheshimu, basi watatuletea sheria bomba kabisa itakayokuwa ikisimamia waandishi wa habari nchini," alisema Kulangwa.

Mjumbe wa TEF ambaye ni mwandishi wa habari mzoefu, Revocatus Makaranga alisisitiza wabunge kuonyesha umuhimu wa pekee katika mjadala wa muswada wa mabadiliko ya sheria hiyo.

"Kwa kuwa sisi waandishi wa habari tumeshaona madhara ya sheria hiyo na tumeweza kuichambua na kuonyesha maeneo yanayokandamiza taaluma ya habari, ni wajibu wa wabunge sasa kuonyesha umuhimu wa pekee katika mjadala wa muswada wa sheria hiyo.

"Sina shaka na wabunge wetu, ninaamini muswada huo utakapowasilishwa bungeni Januri mwakani, wataitendea haki tasnia ya habari kwa kuitungia sheria nzuri kwa sababu hakuna maendeleo pasipokuwa na waandishi wa habari," alisema Makaranga.

TEF kwa kushirikiana na Umoja wa Wadau wa Kupata Habari (CORi) wamekuwa wakilalamikia sheria hiyo kwa kipindi kirefu kwa kile wanachodai inawakandamiza waandishi wa habari na kuna kila sababu kwa serikali kuifanyia mabadiliko.



# Watanzania wahimizwa kuendelea kutunza utamaduni

**Na Anjela Mhando,** MOSHI

NAIBU Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pauline Gekul, amewataka Watanzania kuendelea kutunza na kulinda utamaduni wao kwa maendeleo na maslahi ya Taifa.

Aliyasema hayo jana mkoani Kilimanjaro, wakati wa ugawaji zawadi kwa washindi walioshiriki tamasha la michezo la wanawake na watu wenye ulemavu lililoandaliwa na Taasisi ya Frorida Women Empowerment kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Wilaya ya Moshi.

Katika tamasha hilo wananchi wa eneo hilo walionyesha mambo mbalimbali yanayohusu utamaduni ikiwamo kupiga na kucheza ngoma, vyakula, vifaa vya asili, nyumba na michezo ikiwa ni pamoja na uwasilishaji wa mada mbalimbali zinazohusu tamaduni na maendeleo ya mkoa huo.

Alisema kupitia tamasha hilo, Watanzania wamepata fursa ya kujifunza utamaduni wa watu wa mikoa mingine na itasaidia kuendelea kuwafanya kuwa na mshikamano.

Akizungumzia suala la ukatili wa kijinsia unaoendelea katika jamii, aliwataka wazazi na walezi kukemea vitendo hivyo.

"Bado matukio ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto yanaendelea, UWT mnajukumu la kuendelea kulikemea kwa nguvu zote vitendo hivi vya ukatili," alisema.

Pia aliipongeza Taasisi ya Frorida Women Empowerment kwa kushirikiana na UWT kwa kuandaa bonanza hilo, lililowashirikisha vijana wa kike wenye umri mdogo.

Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Moshi, Theresia Komba, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuhamasisha michezo.

Mhandisi Komba alisema atahakikisha katika uongozi wake maslahi ya wanawake dhidi ya dhuluma, ukatili na ubaguzi wa aina yeyote unakomeshwa kwani lengo la serikali ni kumwona mtoto wa kike akipata haki yake.

# RC awaagiza wazazi kupeleka watoto waliofaulu shuleni

**Na Anjela Mhando,** MWANGA

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, amewaagiza wazazi na walezi mkoani humo kuhakikisha wanawapeleka shuleni watoto wao waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza mwakani.

Alitoa agizo hilo jana wilayani Mwanga wakati akikabidhiwa madarasa tisa katika Halmashauri ya Mwanga yaliyogharimu Sh. milioni 180.

"Serikali imetoa utaratibu wa elimu bila malipo kwa kila mwanafunzi ili kuhakikisha wanafunzi wote wanapata fursa ya kuendelea na masomo jambo ambalo litasaidia kuinua uchumi wa taifa kwa kuwa na wasomi wengi," alisema Babu.

Kadhalika aliwaonya wazazi na walezi ambao wamekuwa na tabia ya kuwaozesha watoto wa kike na kuchukua ng'ombe kama sehemu ya mahari ili watoto wasiendelee na masomo yao.

Awali akisoma taarifa ya makabidhiano ya madarasa hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, Mwajuma Nasombe, alisema kati ya vyumba tisa vya madarasa vilivyojengwa kwenye wilayani humo, ujenzi wa vyumba hivyo umekamilika kwa asilimia 100 na viko tayari.

"Mwaka 2022 wanafunzi wa darasa la saba waliofanya mitihani kwenye wilaya yetu walikuwa 3,300 kati yao wanafunzi 2,700 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023," alisema Nasombe.

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdallah Mwaipaya, alizishukuru kamati za ujenzi kwa namna zilivyoshiriki kukamilisha ujenzi wa vyumba hivyo.

Akizungumza kwa niaba ya madiwani wa halmashari hiyo, Diwani wa Kata ya Kileo, Kuria Msuya, aliishukuru serikali kwa kutoa fedha zilizotumika kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Alisema: "Katika kata yangu ya Kileo, tumepata darasa moja kwenye Shule ya Sekondari Kifaru, kwamba wanafunzi wa kidato cha kwanza wataingia darasani pasipo kuwasumbua wazazi kwa kutoa michango."

Katibu Tawala Mkoa wa Kilimanjaro, William Machum, aliwashukuru wananchi kwa michango yao jambo ambalo limewezesha ukamilishaji wa madarasa hayo.



Wakuu wa Taasisi ya Usanifu na Ubunifu Mitambo (TEMDO) na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DTI) wakibadilishana mikataba baada ya kutia saini makubaliano ya kufanya kazi kwa kushirikiana kwa lengo la kuendeleza na kuzalisha bunifu zilizobuniwa na taasisi hizo kibiashara, mkoani Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# SBT yatoa mbegu tani 70 kumaliza uhaba wa sukari

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

BODI ya Sukari Tanzania (SBT) imewapatia wakulima wa miwa mbegu za kisasa tani 70 ili waweze kuzalisha kwa tija na kuondoa uhaba wa sukari nchini.

Mbegu hizo zilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Ofisa Mwandamizi Mipango na Uratibu wa Bodi ya SBT, Grace Kabate, katika Bonde la Kiru lililoko wilayani Babati mkoani Manyara.

Akizungumza na wakulima wa zao hilo, alisema bodi hiyo ni kiungo muhimu, ndiyo maana wameamua kuwapelekea wakulima mbegu ambayo ni chanzo cha uhai.

Kabate alisema Machi mwaka huu bodi hiyo ilianzisha kitalu cha mbegu za kisasa cha miwa chenye ukubwa wa hekari tatu katika bonde hilo.

Aidha, alisema mbegu hizo zitasaidia kuongeza kipato cha wakulima wa miwa wilayani humo.

Alisema walishindwa kuanzisha maeneo ya Matufa na Gichameda kutokana na maeneo hayo kuwa na mazao mengine.

"Bodi ya Sukari inawashukuru wakulima ambao wametoa maeneo yao ili tuanzishe kitalu cha mbegu bora za miwa," alisema Kabate.

Alisema mbegu walizopatiwa wakulima wataanza kuzitumia kuzalisha miwa kuanzia Januari mwakani ili waweze kuongeza tija na kusaidia wakulima wengine kupata mbegu za kisasa.


Katibu Tawala wa Wilaya ya Babati, Halfani Matipula, alisema eneo la Kiru ni la mfano kwa kilimo cha miwa, kwamba mbegu hizo zitasaidia kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Alisema wataalamu hawatakiwi kukaa ofisini ni vizuri waende kwa wakulima na kuwapatia elimu juu ya mbegu bora.

Aliyekuwa Mbunge wa Babati Vijijini, Vrajil Jituson, aliiomba Bodi ya SBT kuwasaidia wakulima wapate vifaa vya kupima udongo na maji.

Jituson pia aliomba kuanzishwa kituo cha utafiti mkoani humo ili kisaidie kuongeza tija ya kilimo cha miwa na mazao mengine.

Mtafiti kutoka Taasisi ya Kilimo Tanzania (TARI), Kibaha Jeremiah Kabisa, alisema wakulima wanatakiwa kuzingatia matumizi ya dawa za kuua wadudu wanaoshambulia miwa.





# Watunga sheria kuwabana wazazi wasiochangia chakula

**Na Oscar Assenga,** PANGANI

WANANCHI wa Kata ya Kipumbwi wilayani Pangani mkoani Tanga, wametunga sheria ndogo ya kuwabana wazazi na walezi ambao hawachangii chakula cha wanafunzi shuleni.

Baada ya kukamilisha mchakato wa utungaji wa sheria hiyo, zitapelekwa katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Pangani kwa ajili ya kupitishwa.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kipumbwi, Akida Omari, alibainisha hayo jana wakati wa mkutano wa kuhamasisha uwajibikaji wa jamii na mamlaka husika katika uboreshaji wa elimu katika kata hiyo.

Lengo la kutungwa kwa sheria hiyo ilikuwa ni kuwachukulia hatua kali za kisheria wazazi na walezi ambao wamegoma kuchangia chakula cha wanafunzi.

Alisema uwapo wa sheria hizo, kutaongeza chachu ya wazazi na walezi kuona umuhimu wa kuchangia chakula shuleni pia itasaidia kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi jambo.

"Hatutanii tumekubaliana na wazazi mpango wa chakula Shule ya Msingi Kipumbwi uanze mwezi ujazo kwa kuwapa wanafunzi maziwa na karanga na baadaye chakula cha mchana.

"Tutapita kwenye nyumba za starehe kuweka katazo la watoto kuokingia kwenye maeneo hayo na watakaobainika watachukuliwa hatua," alisema. Awali akizungumza suala la umuhimu wa chakula shuleni, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ubangaa, Fatuma Mnyamisi, alisema wazazi na walezi ambao hawatachangia watachukua orodha yao na baadaye kuwashtaki.

Alisema wamelazimika kufikia hatua hiyo, ili kuhakikisha watoto wanapata chakula kwa ajili ya kuwawezesha kushika vizuri wanachofundishwa.

Mratibu wa mradi wa kuhamasisha uwajibikaji jamii na mamlaka husika kutoka Shirika la Tree of Hope, Goodluck Malilo, alisema kuna umuhimu wazazi na walezi kufuatilia maendeleo ya watoto wao wanapokuwa shuleni kujua maendeleo yao.

Alisema wanapaswa kuwalipia watoto wao chakula ili kuwawezesha kupata mlo kwa kuwa kuna faida kubwa na kwamba itamsaidia mwalimu anapofundisha darasani.

Alisema: "Mtoto anayepata chakula shuleni akili yake inachangamka tofauti na yule asiyekuwa na kitu tumboni kwa kuwa hakuna kitu ambacho anaweza kuingiza kwenye akili yake."



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Anna Mbogo (kushoto), akizungumza kwenye mdahalo wa maendeleo uliofanyika juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Vijana walalamika kucheleweshewa mikopo asilimia 10

**Na Allan Isack,** BABATI

VIJANA wilayani Babati, mkoani Manyara wamelalamikia kitendo cha ucheleweshwaji wa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Walitoa malalamiko hayo jana wakati wakizungumza kwenye kikao cha kutoa mrejesho wa ufuatiliaji na uwajibikaji wa jamii katika uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wilayani humo, Hamisi Hussein, alisema Halmashauri ya Babati, inapochelewa kutoa mkopo kwa kundi hilo muhimu kwenye jamii husababisha kuzorota kwa shughuli za uzalishaji kutokana na ukosefu wa mitaji.

"Kutokana na vijana kutokuwa na mitaji ya uhakika halmashauri inapochelewa kuwapatia mikopo inasababisha kusuasua na kuzorotesha shughuli za uzalishaji mali ambazo zingewasaidia kuongeza kipato na kukuza mitaji yao kutokana na biashara zinazofanya na kila mmoja wetu,"alisema Hussein.

Alisema mikopo hiyo, ikitolewa kwa wakati itachangia kukua kwa uchumi kwa mtu mmoja mmoja kwa kuwa kutakuwapo na mzunguko wa fedha kwenye eneo hilo kulingana na shughuli au biashara zinazofanyika.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Yahaya Loya, alisema halmashauri inapochelewesha kutoa mkopo kwa wakati inasababishwa na baadhi ya vijana waliopatiwa mikopo kuchelewa kuirejesha au kushindwa kabisa.

"Wako baadhi ya vijana wanapokopeshwa mikopo hii wanachelewa kuirejesha kwa wakati hivyo ni moja ya sababu inayochangia ucheleweshaji wa kuwakopesha wengine hadi tukusanye marejesho ndiyo tuweze kukopesha tena," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Civic Social Protection Foundation, Nemence Iria, alisema kuna umuhimu kwa halmashauri kuongeza kasi ya utoaji wa mikopo ili kuwakomboa vijana kiuchumi.

Ofisa Tawala Wilaya ya Babati, Khalfani Mathipula, alisema watahakikisha mikopo inaendelea kutolewa kwa makundi husika kwa kuwa ni maelekezo ya serikali kuu.

# Serikali yakamilisha ukarabati kivuko MV Tanga

**Na Hamida Kamchalla,** PANGANI

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kushirikiana na Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA), imekamilisha ukarabati wa kivuko cha Mv Tanga kinachohudumia wananchi wa Wilaya ya Pangani.

TEMESA walikabidhi kivuko hicho kilichokarabatiwa kwa muda wa miezi sita na kimegharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.1.

Kukarabatiwa kwa kivuko hicho kutapanua wigo wa usafirishaji kwa kuwa ni muhimu kwa ustawi wa maendeleo ya wakazi wa eneo hilo.

Akipokea kivuko hicho jana, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, alisema kukamilika kwa ukarabati wa huo kutasaidia kuboresha huduma za mawasiliano na usafirishaji wa bidhaa za wananchi pamoja na kuchochea maendeleo.

"Kivuko cha Mv Tanga kitainua na kuongeza uboreshaji wa huduma za mawasiliano na usafirishaji na kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa wananchi wetu, nitoe pongezi tena kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kuwezesha vivuko vipya kujengwa nchini," alisema Mgumba.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Sekta ya Ujenzi, Ludovick Nduhiye, alisema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 serikali imepanga kutanua vivuko nane ambavyo vitatoa huduma katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo kwenye Ziwa Victoria na maeneo yanayohitajika.

"Kwa mwaka wa fedha 2022/23 Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inatekeleza ujenzi wa vivuko vipya nane, katika vivuko hivyo vipo ambavyo vitakavyotoa huduma katika ukanda wa Ziwa Victoria," alifafanua.

Mtendaji Mkuu wa TEMESA, Lazaro Kihahala, alisema kivuko hicho kina uwezo wa kubeba abiria 100 sambamba na mizigo yenye uzito wa tani 50 yakiwamo magari madogo sita.

Aidha, alisema katika mwaka huu wa fedha serikali imepanga kufanya ukarabati kwa vivuko 14 ambavyo vitagharimu Sh. bilioni 22.99."Vivuko vitakavyo karabatiwa ni Mv Tanga, ambacho ndiyo hiki tunakikabidhi, Mv Misungwi, Mv Musoma, Mv Sabasaba, Mv Kazi, Mv Nyerere, Mv Kitunda, Mv Kilombero II,Mv Ruhuhu, Mv Old Ruvuvu, Mv Magogoni, Mv Ujenzi, Mv Kome II, Mv Mara,"alisema.

Waziri wa Maji ambaye ni Mbunge wa Pangani, Juma Aweso, aliishukuru serikali kwa ukarabati wa kivuko hicho.

"Tunaiomba serikali isaidie Wilaya ya Pangani kupata boti ya mwendo kasi ili kuwezesha kutoa huduma ya uhakika wa safari za Pangani na Zanzibar,"alisema Aweso.

Wakazi wa wilaya hiyo walipongeza serikali kwa kuwapatia kivuko hicho wakisema awali walikuwa wakipata shida ya usafiri kwa kuwa walitumia kivuko kimoja na kilikuwa ni kidogo.

Mmoja wa wakazi hao, Mariam Mohamed alisema: "Tunaishukuru serikali kwa kutatua kero ya kivuko kwa sasa tutaendelea kujituma na kufanya kazi kwa uhuru na kwa uhakika wa kivuko ambacho kitatoa huduma kwa muda wote."

Nipashe
TESA
Jumanne Desemba 20, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



UWEZO AWARD
Kisima kinachoibua wajasiriamali wabunifu na wagunduzi shuleni

Ukurasa 15



MWISHO KUSOMA KINADHARIA
Uwekezaji mafunzo kwa vitendo mpango mpya maendeleo ya jamii

Ukurasa 14

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# Ufugaji kuku Dar unavyozidi kuwa pasua kichwa, magonjwa, vifo balaa

• Mtaalamu: Wazoefu wasaidie, dawa asili zitumike

“NIMEKATA tamaa. Nasikitika mdondo umevamia banda langu nimebakia na kazi moja kuangalia kuku wangu wanavyosinzia na kuanguka nyakati za mchana ambazo walitakiwa kula, badala ya kuwalisha ninawachinja.

“Kwa vile siwezi kukesha nao bandani, nikiamka asubuhi ninapofungua mlango naanza kutupa vibudu vya kuku waliouawa na mdondo na mafua usiku.” Anasema Anastazia Mrosso mkazi wa Madale, Dar es Salaam, anayefuga kuku.

Mama huyo analalamika kuwa magonjwa ya ndui ya kuku, mdondo na mafua yamezidi na kwamba kila kifaranga kinachofugwa mtaani ili familia ijipatie mayai ya watoto inakabiliwa na tatizo hilo na husababisha vifo vingi.

Anasema maradhi haya yanayoitwa’fawl pox’ dalili zake ni pamoja na kuwa na vipele au vidonda sehemu zote zisizo na manyoya kuanzia miguuni, kikokoriko (upanga), mdomoni na machoni, lakini akifunguliwa midomoni na kooni kuna vidonda na kuku anakoroma wakati anahema, kukohoa na kupiga chafya na wengi hufa kwa muda mfupi kitu ambacho kinakatisha tamaa wafugaji wa kuku.

MAFUA NI KERO

Anastazia anasema mafua ya kuku nayo ni kero mno zama hizi akisema dalili zake ni pamoja na macho kuvimba, chafya muda wote, kushindwa kula, kuvimba macho na kutoa usaha.

“Kuku wetu wanakufa kwa muda mfupi mno. Wanaweza kufa banda zima kwa dakika chache. Inawezekana mfugaji ana kuku au vifaranga 100 wakafa wote kwa muda mfupi. Tunaomba wataalamu watusaidie.”

Anazungumzia mdondo, akisema nao zama hizi hauishi, akitaka wataalamu wajitokeze kusaidia. Anataja baadhi ya dalili kuwa ni pamoja na kukohoa, kuhara kinyesi cha kijani, kutokwa na udenda, kusinzia na wengine huvimba, midomo na macho na kikokoriko na kwamba kifo hutokea ndani ya muda mfupi.



Ufugaji wa kuku mijini. **PICHA:MTANDAO**

Joan Siriwa, anayefuga kuku na bata anatoa angalizo kuwa licha ya chanjo hizo kuwapo inakuwa vigumu wakulima na wafugaji kuwapa kuku kutokana na maelekezo kuwa wanyweshwe kuku zaidi ya 50.

“Tunataka tuchanganye na chakula kama pumba, mahindi au kuwekwa kwenye maji ili kuku wale na kunywa. Magonjwa mengi ya virusi hivi vinavyoshambulia kuku na kusababisha vifo vya maelfu kwa wakati mmoja na kuongeza hasara kwa wafugaji hasa huku mijini japo na vijijini shida hiyo,” anasema.

Mfugaji huyo anaamini kuwa ni lazima kuwe na njia nyepesi ya kuwapa kuku tiba kuliko ilivyo sasa ili kupunguza ugumu wa ufugaji mijini.

“Tunasikia ndui inachanjwa kwenye bawa zipo nyingine kwenye jicho inakuwa vigumu kuchanja. Hata kama kuna ugunduzi wa chanjo kuwakinga kuku na ugonjwa wa mdondo, ndui na mafua bado kuna ugumu. Nina wasiwasi kuwa huenda maradhi hayo yamekuwa sugu ndiyo maana kila mwaka yanaibuka na kusababisha maafa zaidi,” anasema Joan.

Anaongeza kuwa dawa madukani zinawachanganya wataalamu nao hawaeleweki na kushauri kuwe na makongamano na semina kwa wafugaji zinazotolewa mitaani hata na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) Taasisi za Utafiti wa Mifugo ili wakulima waelimike na kupata dawa zinazostahili.

Anaeleza kuwa zamani waliambiwa kuwa kuna chanjo yenye dawa tatu kwa pamoja na inapotolewa inatibu magonjwa ya njia za hewa, lakini mdondo na inaweza kutumiwa popote kwa sababu inastahimili joto japo haitakiwa kuwekwa juani au karibu na jiko au moto, lakini taarifa kama hizo siku hizi hazipo.

**DAWA ZA ASILI**

Joan anasema changamoto

INAENDELEA UK. 18

ELIMU

NA SABATO KASIKA

## MWISHO KUSOMA KINADHARIA

# Uwekezaji mafunzo kwa vitendo mpango mpya maendeleo ya jamii

MOJA ya vikwazo vinavyowakabili wahitimu wa vyuo vikuu mbalimbali ni kukosa ujuzi wa ziada ambao unaweza kuwasaidia katika ushindani wa soko la ajira.

Baadhi yao wamekuwa wakilalamikia ugumu wa kupata kazi huku wakiwamo wasio na ujuzi wa kujiajiri, licha ya kutumia muda mwingi hadi kuhitimu masomo yao ya vyuo vya kati na vya juu.

Pamoja na kikwazo hicho, viongozi wa serikali wakiwamo pia wanasiasa, wataalamu wa uchumi na wafanyabiashara wamekuwa wakiwahimiza wahitimu kutosubiri ajira, badala yake wawe tayari kufanya kazi yoyote, ili kujiingizia kipato.

Wakati kukiwa na mkazo huo wa kutaka wahitimu wasisubiri ajira rasmi, serikali ina nia ya kuweka mkazo katika elimu na ujuzi wa kada mbalimbali ikiwamo ya maendeleo ya jamii

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, anasema mwelekeo wa serikali kwa sasa ni kusisitiza utoaji elimu yenye ujuzi ili wahitimu hasa wa maendeleo ya jamii wanapata stadi za kazi.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alipotembelea majengo ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Kampasi ya Kisangara Mwanga mkoani Kilimanjaro. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

Anasema hayo maeneo mawili tofauti, kuanzia kwenye mahafali ya Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru Arusha na mahafali ya Taasisi ya tano ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Kampasi ya Kisangara, Mwanga, Kilimanjaro.

Wakati akiwatunuku wahitimu 1,604 wa fani ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi mbalimbali, katika mahafali ya 12 ya Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru mkoani Arusha wiki iliyopita anahitimiza elimu ya ujuzi.

"Serikali na hata sekta binafsi hazina uwezo wa kuajiri wahitimu wote wa elimu ya juu, hivyo dhana ya uanagenzi, ubunifu na ushirikishwaji jamii katika mitaala ni suluhisho la ukosefu wa ajira kwa kuwa wahitimu wanapata ujuzi wanaoweza kutumia kujiajiri na hata kuajiri wengine," anasema Dk. Dorothy.

Waziri pia anatoa rai kwa wadau wa mahali pa kazi ikiwamo mamlaka za serikali, asasi za kiraia, mashirika na kampuni kutenga nafasi za uanagenzi kwa wanafunzi wa taasisi, ili kutatua vikwazo vya ukosefu wa ajira kwa wahitimu.

"Taaluma ya Maendeleo ya Jamii ni muhimu, kwani inawezesha sekta nyingine kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa sababu inashughulika na watu moja kwa moja," anasema.

Anawataka wahitimu hao kuwa na fikra chanya na ubunifu kwa kuwa wamehitimu kipindi ambacho serikali imefanya kazi ya kuvutia wawekezaji wa ndani na nje, kujenga uchumi imara na kuongeza mzunguko wa fedha.

"Ninyi ni mawakala wa mabadiliko, kiuhalisia mnapaswa kusaidia kuleta fikra mpya na chanya kwa jamii yetu, kwa ajili ya kuleta mwamko na hamasa ya maendeleo," anasema.

**KINARA UKATILI**

Aidha, Taasisi hiyo ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imemtunuku Waziri Dk. Dorothy tuzo kwa kuwa kinara wa mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili vinavyotokea ndani ya jamii.

Mwenyekiti wa Bodi ya Uendeshaji wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Dk. Rosemarie Mwaipopo, anasema waziri huyo amekuwa na mchango mkubwa katika mapambano hayo.

"Tunatambua mchango wako, pia tunakuhakikishia kwamba Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru itaendelea kutatua vikwazo mbalimbali vinavyoikabili ikielekea kutimiza miaka 60 tangu kuanzisha kwake," anasema Dk. Rosemarie.

Anashukuru serikali kwa kutoa Shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ikiwamo ununuzi wa samani katika majengo ya hosteli ya wasichana na kumbi za mihadhara.

Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Dk. Bakari George, anasema taasisi hiyo kwa mwaka huu imeadhimisha Wiki ya Maendeleo ya Jamii kwa shughuli mbalimbali kwa lengo la kujikumbusha kwa vitendo shughuli za msingi za fani ya Maendeleo ya Jamii.

Anataja baadhi ya shughuli zilizofanywa katika maadhimisho hayo yaliyoambatana na kongamano la kitaaluma kuwa ni kubadilishana mawazo kuhusu mwelekeo wa maendeleo ya jamii.

"Mengine ni upandaji miti, matembezi ya kuhamasisha lishe bora, mashindano ya uandishi wa maandiko ya miradi, elimu juu ya mapambano ya vitendo vya ukatili na kuchangia damu salama," anasema Dk. George.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alipokuwa katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru Arusha.

Katika mahafali ya Kampasi ya Kisangara, iliyoko wilayani Mwanga mkoa wa Kilimanjaro, anasema wahitimu wana fursa ya kutatua changamoto za kijamii hasa za kisaikolojia zinazowakumba watu wengi, pamoja na vijana.

Anawataka wahitimu hao wakati wakisubiri ajira, wawe na maono ya kugeuza changamoto za kijamii kuwa fursa, kwamba dunia ya sasa inawahitaji wataalamu wa Ustawi wa Jamii, ili wasaidie kuzipatia ufumbuzi.

"Taaluma hii ya ustawi wa jamii ni kubwa na inayohitaji wenye moyo wa maadili na upendo kwa sababu inalenga kuwasikiliza wakiwamo wanaolia machozi na kukosa tumaini," anasema.

Anasema wanataaluma hao wanatakiwa kuangaliwa kwa jicho la pekee hasa kwenye zama hizi, na kwamba msingi mkuu wa wasomi kuelimika ni kuwa na uzalendo kwa nchi yao, huku akifafanua kuwa matumaini yake ni wahitimu hao kufanya vizuri kwa kusimamia misingi na maadili ya taaluma.

"Wizara imeweka miongozo na kanuni kuhusu suala la malezi ya watoto kuanzia ngazi ya familia na vituo vya kulelea watoto na anaipongeza Taasisi ya Ustawi wa Jamii kwa kuunda mitaala ya malezi na makuzi.

"Namwagiza Kamishna wa Ustawi wa Jamii kujadiliana na menejimenti ya taasisi kuona namna gani inaweza kuanza kutoa vyeti katika eneo la malezi na makuzi na saikolojia, ili kuimarisha ustawi," anasema.

Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Magavana wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Dk. Lulu Mahai, anatoa wito kwa wadau wa malezi na makuzi kutumia taasisi hiyo kupata taaluma ya malezi na makuzi bora.

ELIMU

NA GWAMAKA ALIPIPI

UWEZO AWARD

# Kisima kinachoibua wajasiriamali wabunifu na wagunduzi shuleni

KUTOA elimu ya ujasiriamali kuanzia shule ya msingi hadi ngazi za juu kunaweza kuwapa maisha bora watoto wengi wanaokwama kuendelea na masomo.

Ni kwa sababu wataweza kubuni na kupata cha kufanyakazi, badala ya kukaa vijiweni au kushiriki uhalifu mitaani, ndivyo, ni kwa mujibu wa Shirika lisilokuwa la kiserikali la Great Hope Foundation.

Katika kutatua changamoto ya ukosefu wa mafunzo ya ujasiriamali Great of Hope Foundation wana mkakati wa 'Uwezo Award', ambao ni fursa kwa wanafunzi wa sekondari kujifunza ujasiriamali wakiwa shuleni ili wanapoondoka, wana akiba ya ujuzi wanaokwenda kuufanyia kazi kubadili maisha.

Mkurugenzi wa shirika hilo na Mratibu wa Uwezo Award, Noelle Mahuvi, anaeleza kuwa mradi huo unajikita kuwapa nafasi wanafunzi kujifunza ujasiriamali kwa vitendo wakiwa darasani.

Mahuvi, anasema mradi huo unaendeshwa kwa njia ya mashindano na kwamba ushindani hufanya kupitia miradi mbalimbali ya kijasiriamali na ya kibunifu, inayoleta matokea chanya katika jamii inayowazunguka.

Anasema mradi wa Uwezo Award umekuwa kazini tangu mwaka 2016, ukiwa na lengo la kuwapa wanafunzi jukwaa la kujifunza ujasiriamali kwa vitendo wakiwa kabla ya kuondoka shuleni.

Mahuvi, anaongeza kuwa kupitia mradi huo wanafunzi wa sekondari wanabuni na kutekeleza miradi ya kijasiriamali na fedha wanazopata hutumia kufanya miradi ya kijamii kwenye maeneo wanayochagua.

"Kila mwaka Great Hope Foundation, hukusanya mawazo ya kibunifu na kijasiriamali kutoka kwa wanafunzi, na wanaofanya vizuri hupewa tuzo. Vigezo vikubwa ambavyo vinaangaliwa kwanza kuwapa nafasi wanafunzi kutambua uwezo wao, ambao mara nyingi hauonekani moja kwa moja darasani."

Jambo la pili anaongeza kuwa mradi huo unapaswa kuwajengea wanafunzi ujuzi na jingine ni kuleta mabadiliko chanya katika jamii ulikofanyika, anaongeza Mahuvi.



Washindi wa jumla wa Tuzo za Uwezo Award 2022, Sekondari za Kibaha na Benjamin Mkapa wakifurahia mafanikio pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Great Hope Foundation, Noelle Mahuvi (kushoto). **PICHA ZOTE: GHF**

### MAFANIKIO 2022

Akizungumzia mafanikio kwa mwaka huu, Mahuvi anabainisha kwamba wanafunzi kutoka shule zaidi ya 250 za sekondari za Dar es Salaam, Pwani na Morogoro zilifikiwa na sekondari 33 zimekidhi vigezo vya kupata tuzo.

Katika mashindano ya mwaka huu, Shule ya Sekondari Kibaha iliyoko mkoa wa Pwani imeibuka kidedea kwa kuwa mshindi wa kwanza na kujinyakulia tuzo ya dhahabu, zawadi ya Sh.500,000.

Nafasi ya pili ilishikwa na Sekondari Benjamin Mkapa ikipata zawadi ya Sh. 200,000.

Mahuvi anayataja kuwa ni pamoja na kutengeneza wanafunzi wenye ujuzi kiubunifu na ugunduzi ili kwenda kupambana katika changamoto za ajira na kwamba kwa mwaka huu wengi walioshinda wametengeneza miradi ya mboga.

Mratibu wa Tuzo Award anasema mwanafunzi anapomaliza elimu ya sekondari anakuwa na wazo la kufanya kitu kitakachomuingizia kipato wakati anaendelea kutafuta ajira.

"Miradi wanayoifanya inakuwa nje ya muda wa masomo, lakini malengo yetu tunataka miaka ya baadaye wafanye ndani ya mitaala ya shule," anasema Mahuwi.

### LAZIMA KUSHIRIKI

"Walimu na wazazi waruhusuni wanafunzi kushiriki katika tuzo hizo sambamba na kuwahimiza kufanya bidii darasani na kwenye ubunifu," anasema Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Dar es Salaam, Kheri James.

Anayasisitiza hayo katika tamasha la tuzo za uwezo kwa mwaka huu lililofanyika Dar es Salaam, akiwa ni mgeni rasmi.

Anatoa rai kwa wakuu wa shule akiwataka pia kuruhusu na kusaidia wanafunzi kushiriki ili kupata uzoefu na kujijenga kwenye ubunifu, ugunduzi na ujasiriamali ili yale wanayojifunza yawe mchango mkubwa katika kujenga vijana wenye ujuzi na maarifa yatakayowasaidia kupambana na umaskini, lakini kuingia katika soko la ajira.

"Shirika hili limeanza mazungumzo na Taasisi ya Elimu ya Tanzania pamoja na wizara, kuona ni kwa namna gani, mradi huu unaweza kuwa sehemu ya mtaala wetu. "Pia niwaombe walimu na wazazi, tuendelee kuwahimiza wanafunzi kushiriki mradi huu wa Uwezo Award kwa sababu una manufaa kwa wanafunzi, shule na hata walimu," anasema James.

### SAUTI ZA WASHINDI

Wanafunzi zaidi ya 20 wa Sekondari ya Kibaha, ndiyo washindi wa mwaka huu, akizungumza na gazeti hili, Folden Suleiman anasema wamebuni miradi mingi kama kutengeneza na kuuza vifutio vya ubao 10, na kupata Sh. 20,000.

Aidha, kuandaa mafunzo ya ubunifu na usanifu shuleni hapo na kuwafundisha wenzao namna ya kutengeneza nembo, vipeperushi, mabango, kadi za biashara, matangazo, makala za video kwa wanafunzi 39 na kupata Sh. 39,000.

Folden anasema pia wameendesha kampeni ya kutoa damu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila na kupata uniti 48.

Anabainisha kuwa wameshiriki usafi katika kituo cha kutoa ushauri nasaha cha waathirika wa VVU na UKIMWI cha Hospitali ya Tumbi-Kibaha kwa kukata nyasi. Aidha, wamenunua soketi za umeme na kuzifunga katika maeneo yalikuwa hayana vifaa hivyo ili kuzuia athari za shoti za umeme.

Anataja kutengeneza vitafunwa -maandazi na kuuza katika mashindano ya UMISETA yaliyofanyika shuleni kwao na kupata Sh.200,000.

Anasema pesa walizozipata walizitumia kwenye ziara ya mafunzo kwenye Sekondari ya Nyumbu kupitia mradi wao uitwao 'Kumthamini Mwanamke' na kutoa msaada wa taulo za kike maboksi 70 kwa wanafunzi wasichana.

"Pia tulikusanya chupa za maji zaidi ya 3,000 na kuzipamba katika eneo mojawapo la shule, na kuuza urembo katika mahafali ya kidato cha sita shuleni na kupata Sh. 300, 000," anasema Foden.

Mbali na hilo, wamekarabati kompyuta za walimu na kupata Sh. 20,000 na nyingine 104,000 kutoka kwa wanachama 52 wapya waliokuwa wakijiunga na umoja wao kama ada ya kiingilio.

Foden anataja ziara katika Sekondari ya Mkuza ambayo iliungua na kutoa msaada wa vifaa mbalimbali vya masomo kwa wanafunzi wenzao.

Anabainishwa kuwa pia walitengeneza vitambulisho kwa wanafunzi wenzao shuleni hapo na kupata Sh.178,000 pamoja na kubuni na kutengeneza nembo kwenye fulana na traki suti kwa wanafunzi wa kidato cha tano na kupata Sh. 630,000.

Anasema kupitia fedha hizo walinunua saruji na kufanya ukarabati wa vimbweta na uwanja wa mpira wa kikapu (basketball) ambao ulitumiwa katika mashindano ya UMISETA.

Na mshindi wa pili ni Sekondari ya Benjamin Mkapa, akizungumzia mafanikio Khadija Subra anayesoma kidato cha sita, anasema walifanya miradi mbalimbali kama kuchangishana fedha na kuanza kulima bustani ya matembele mekundu shuleni hapo lakini bustani yao ikatumiwa kujenga maabara, hivyo haukuendelea.

Aidha, walibuni mradi wa kufunga madumu ya maji juu ya miti ii kuwekea taka, pia walipika maandazi na kuyauza na kupata zaidi ya Sh. 300,000 pesa ambazo walizitumia kununua rangi na kupaka sehemu ya majengo ya shule yaliyochakaa akitaja ofisi za utawala na za skauti.

Anabainisha kuwa sehemu ya pesa hizo pia walinunua kilo 10 za mchele, mafuta ya petroli, chupi, mishumaa, biskuti, penseli, ufutio pamoja na mbegu na kwenda kutoa msaada katika jela ya watoto iliyoko Upanga Dar es Salaam.

"Pia tuliandaa na kuonyesha sinema shuleni, tuliuza tiketi na tulipata zaidi ya Sh.100, 000 kama kiingilio na pesa hizo tulikarabati mfereji wa maji taka," anasema.

Kupitia onyesho la sinema waliwashawishi wanafunzi kufanya utalii wa ndani na kuwapeleka kwenye Makumbusho ya Bagamoyo na pesa waliyoipata walinunua bidhaa muhimu na kutoa msaada katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road Dar es Salaam.



ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Makali tabianchi, ndivyo Afrika inavyobakia yatima



Barabara ya kitaifa namba 1 iliyoharibiwa na mafuriko jijini Kinshasa na kuua watu 169. **PICHA: RFI**

Wiki iliyopita Rais Felix Thisekedi wa DRC, akiwa kwenye mkutano wa Afrika na Marekani jijini Washington DC, anahusisha athari za mabadiliko ya tabianchi na mafuriko makubwa yaliyoikumba nchi yake na kuua takribani watu 100 katika mji mkuu, Kinshasa.

Barabara kuu zilifungwa kwa saa kadhaa baada ya kufunikwa na maji, wakati jiji hilo linalokadiriwa kuwa na watu milioni 15 likisimama kukabili mafuriko.

Kwa mujibu wa DW watu waliofariki kwenye mafuriko hayo ni takribani zaidi ya 120, huku Mkuu wa Jeshi la Polisi Sylvano Kasongo, akikaririwa na Shirika la Habari la AFP, akieleza kuwa waliofariki walikuwa wakiishi milimani ambayo iliporomoka na wengi kufunikwa na udongo.

Kwenye milima nyumba ziliporomoka baada mvua kubwa maeneo ya Binza Delvaux, yakitajwa kuwa na hali mbaya.

Rais Thisekedi, anasema:"Congo imekumbwa na mafuriko kutokana na mvua kubwa zilizochochewa na mabadiliko ya tabianchi na kusababisha vifo vya mamia ya watu pamoja na uharibifu mkubwa wa mali ambao ungeweza kuepukika kama makubaliano ya kuzuia uchafuzi yaliyofikiwa miaka ya nyuma yangetekelezwa."

Novemba, 2019, karibu watu 40 walikufa katika jiji hilo la Kinshasa kutokana na mafuriko na maporomoko ya udongo. Eneo la Mont-Ngafula liliathiriwa zaidi, ingawa wakazi wa eneo hilo wanasema hawajawahi kushuhudia mafuriko na athari kubwa kama za sasa.

AFRIKA YATIMA

Mwezi uliopita mataifa yaliondoka kwenye mkutano wa mabadiliko ya tabianchi huko Misri na kinachoonekana sasa ni upweke unaoikabili Afrika, katika suala la mabadiliko ya tabianchi, inasema makala ya DW.

Baada ya mazungumzo ya mabadiliko ya tabianchi ya COP27 mjini Sharm el-Sheikh, Misri viongozi wa Afrika lazima waanze mara moja kupanga upya mikakati yao.

Sasa tena zaidi ya hapo awali, Afrika inahitaji kufikiria jinsi mamilioni ya watu walio katika hatari ya kukabiliwa na athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi wanavyoweza kusaidiwa.

Ukweli wa mambo ni kwamba ufadhili kutoka kwa mataifa tajiri kusaidia kupunguza athari za ongezeko la joto duniani sio chanzo cha kutegemewa wanachopaswa kukiamini kwa asilimia zote.

Viongozi wajue kuwa idadi ya wanaokabiliwa na njaa inatarajiwa kuongezeka ikitokana na ukame na inatabiriwa kufikia kiwango cha hatari katika eneo la Pembe ya Afrika.

Umoja wa Mataifa unaonya kuwa kutokana na hali hiyo, mamilioni ya Waafrika walio katika mazingira magumu wanajiandaa kukabiliana na njaa kali katika kipindi cha miezi ijayo.

Mtazamo huu mbaya hauwezi kusubiri mazungumzo yasiyo na mwisho ya mabadiliko ya tabianchi ni lazima viongozi waanze na kuamka sasa.

Afrika lazima ikubali kuwa iko peke yake na ichukue hatua za haraka kusaidia watu wake wanaokabiliwa na njaa ya mara kwa mara.

**NI KUTOKUAMINIANA**

Mazungumzo juu ya mabadiliko ya tabinachi yamesababisha hofu na ongezeko la hali ya kutoaminiana kati ya mataifa ya Kusini na Kaskazini mwa dunia.

Haya yanatokea wakati mamilioni ya Waafrika wanaendelea kuathirika kila siku na joto kali ambalo limechochewa na nchi zilizoendelea ambazo zinachafua kwa asilimia 97 hali ya mazingira duniani.

Wale wanaoteseka wanangoja kwa subira hatua kabambe za kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi kufikiwa kupitia mazungumzo.

Wakati wa kuchukua hatua ni sasa, na viongozi wa Kiafrika hawawezi kudai kuwa wameishiwa na mawazo ya kuokoa watu wanaoteseka.

Hasa kuna wazo la kubadilisha hali hiyo ambayo viongozi wamekuwa wakilirejesha nyuma kwa miaka 20 sasa.

MATUMIZI YA KILIMO

Mwaka 2003, serikali za Afrika zilijitolea kutumia asilimia 10 ya bajeti yao ya kila mwaka kuendeleza sekta ya chakula na kilimo.

Ahadi hii kubwa ilijulikana kama Tamko la Maputo ambao nia yake ilikuwa ya kufikiwa na yenye maana. Wazo lilikuwa kupunguza uhaba wa chakula wa mara kwa mara kwa watu walio hatarini zaidi barani Afrika ifikapo mwaka 2030.

Kufikia sasa, nchi kadhaa za Kiafrika bado zinajikokota kutekeleza wazo hili, nyingi zimeweka kipaumbele kwenye sekta nyingine. Kenya, Uganda na Senegali zimeweka angalau asilimia nne.

Hofu ya mabadiliko ya tabianchi inalikumbusha bara hili kwamba utekelezaji wa Tamko la Maputo unahitajika sasa kuliko hapo awali.

Na huku pesa za wachafuzi wa mazingira ambao ni nchi matajiri zikisubiriwa Afrika inapaswa kuzingatia kilimo kama suala la kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi.

Kilimo ni uwezo mkubwa wa bara la Afrika usiotumika. Jukumu kuu la sekta ya kilimo kwa Afrika si la kutiliwa chumvi. Ndicho uti wa mgongo wa kila kitu.

Ni tegemeo la mamilioni ya watu katika masuala ya kazi na mapato. Kwa sasa, licha ya vikwazo vingi na kukandamizwa kwa mgao wa rasilimali, sekta hiyo bado ni chanzo cha mapato kinachotegemewa.

Viongozi wengi wanasisitiza dhamira ya serikali zao za kufufua sekta hiyo lakini yote haya yamegeuka kuwa maneno matupu.

**KWANINI KINAPUUZWA?**

Baadhi ya wachumi wanaeleza kuwa ni vigumu kwa sekta ya kilimo kuchangia asilimia 10 ya bajeti yote.

Hii ni kwa sababu uongozi wa Kiafrika una mzigo mkubwa wa madeni ambao yanatumia bajeti zao kwa kiasi kikubwa kuyalipa.

Baadhi ya mataifa pia yametoa kipaumbele katika sekta nyingine muhimu, kama vile usalama, utalii, miundombinu na elimu

Lakini kwa kuzingatia nyakati ngumu zinazokuja, ambazo kwa kiasi fulani zimesababishwa na mabadiliko ya tabianchi, je, ni jambo kubwa kuuliza kwamba ugawaji upya wa bajeti ya matumizi uelekezwe kwenye sekta ya kilimo?

Matumizi ya juu kwa kila mtu yanahusishwa na utendaji kazi bora wa sekta ya kilimo na kwa hivyo, ni hatua ya tahadhari inayostahili kuchukuliwa.

Iwapo yote yatafanyika kwa njia ipasayo, sekta ya kilimo inaweza kuwa chanzo kikubwa cha mapato na hata ikaweza kufadhili sekta nyingine.

Zaidi ya hayo, ongezeko la joto duniani limefanya iwe muhimu zaidi kuongeza utafiti katika eneo hilo, ambao pia utalazimika kufadhiliwa ipasavyo.

Bara la Afrika linahitaji kuendeleza na kutumia aina za mazao yanayostahimili hali tofauti za hewa, maghala yanayoweza kudhibiti wadudu na teknolojia za hali ya juu.

Msukumo huu wa mabadiliko unaweza kutekelezwa kwa ushirikiano na mazungumzo ya haki ya mabadiliko ya tabianchi. Na matokeo yake yanatarajiwa kuwa ushindi kwa bara zima.

ELIMU

NA PAUL MABEJA, MPWAPWA

# Wenye ulemavu bado wanafungiwa ndani

• Waelezwa hawasomi, wengi wamenyimwa elimu makusudi



Wakazi wa kata ya Mazae wilayani Mpwapwa wakifuatilia mafunzo ya umuhimu wa elimu kwa watoto wenye ulemavu kijijini Mazae.

NI ukweli kuwa katika kuzaliwa hakuna aliyejaza fomu au kutuma maombi. Unazaliwa popote na maumbile yako yawe na ukamilifu au yenye ulemavu hakuna aliyeweza kuamua. Kama huo ndiyo ukweli inakuwaje wenye ulemavu hawakubaliki? Mbona familia zinawatenga na hazitaki kuhusishwa nao?

Ni maswali yanayoibuka kutokana na ukweli kwamba maeneo mengi jamii zina mtazamo hasi kuwa watu wenye ulemavu hawana msaada wala faida kwa familia zao na kwao binafsi.

Kutokana na kutambua umuhimu wa watu wenye ulemavu kwenye jamii shirika lisilo la kiserikali la Foundation for Disabilities Hope, (FDH), linazindua mradi wa miezi nane utakaoboresha maisha ya watu wenye mahitaji maalumu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa mkoani FDH Dodoma.

FDH inasema pamoja na juhudi zinazofanyika serikali na wadau kuwakwamua wenye ulemavu bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazochangia kukwamisha kwenye nyanja nyingi.

Inataja moja ya changamoto hizo ni kunyimwa elimu kutokana na wazazi na walezi wengi kuwaficha ndani ili kuzuia wasionekane na jamii na watu wanaowazunguka.

Mradi huo unaodhaminiwa na The Foundation for Civil Society (FCS), unalenga kuhamasisha upatikanaji wa elimu bora kwa watoto wenye mahitaji maalumu wa kata za Mpwapwa Mjini na Mazae.

Akizungumza wakati wa uzinduzi hivi karibuni, msimamizi wa mradi huo Gabriel Muhuwa, anasema sababu za kupelekwa mradi huo katika wilaya ya Mpwampwa ni kuwaponya watoto wengi wenye ulemavu ambao hawajaandikishwa shule, wanaopatikana hapo.

Aidha, anasema baada ya kufika Shule ya Msingi Chazungwa wilayani hapo inayotumika kufundisha watoto wenye mahitaji maalum na kubaini changamoto mbalimbali kama uhaba wa walimu wenye taaluma ya kuwahudumia wenye mahitaji maalum.

"Tulikuta watoto wenye mahitaji maalum zaidi ya 70 lakini mwalimu ni mmoja tukaona ni jambo jema kama mradi huu utatekelezwa hapa ili kujenga uelewa kwa wazazi na jamii kwa ujumla kuhusu umuhimu wa elimu kwa watoto hawa," anasema Muhuwa.

Anataja lengo jingine kuwa ni kuongeza uelewa wa jamii kuhusu haki ya kupata elimu kwa watoto wenye ulemavu, mwitikio wa serikali katika kuboresha mazingira ya ujifunzaji kwa watoto hao.

Anaeleza kuwa mradi huo ulioanza Septemba mwaka huu unatarajiwa kumalizika Aprili 2023 na kwa miezi nane ya utekelezaji kazi zitakazofanyika ni pamoja na kukutana na wadau wa masuala wenye ulemavu.

"Mikutano ya hadhara kwa ajili ya kujenga uelewa wa jamii kuhusu haki ya kupata elimu kwa watoto wenye ulemavu, mingine ya kimkakati na wakuu wa shule na wajumbe wa kamati za shule itafnyika. Kadhalika, kujenga uwezo wa walimu katika utambuzi wa mapema na utunzaji wa watoto wenye ulemavu."

"Kuendesha mkutano wa kimkakati wa ngazi ya wilaya kwa ajili ya utetezi na mipango ya utekelezaji wa taarifa zilizobainishwa na kufanyiwa tathmini na ufuatiliaji," anasema.



Diwani wa Mazae, William Madanya, akitoa hoja wakati wa mafunzo kwa jamii kuhusu umuhimu wa elimu kwa watoto wenye mahitaji maalumu.**PICHA ZOTE: FDH.**

Vilevile, anazungumzia matarajio kuwa baada ya mradi huo kutekelezwa jamii itabadilika na kuacha kuwaficha watoto wenye ulemavu ndani na kuwapeleka shule na serikali kuboresha miundombinu yao ili wasome kwa furaha.

Anasema, mradi huo unatokana na uchambuzi wa hali ya watu wenye ulemavu uliofanywa mwaka 2020 na Shirika la DID, ambalo lilibaini kuwa wenye ulemavu wengi hawasomi na kushindwa kusoma, kuhesabu na kuandika katika maeneo mengi ya Tanzania.

"Hii inatokana na elimu kwa kundi hili kukumbana na changamoto mbalimbali kama vile mazingira ya shule yasiyo rafiki pamoja na uelewa mdogo wa jamii kuhusu haki ya kupata elimu kwa wenye mahitaji maalumu,"anasisitiza.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mpwapwa, George Fuime, anasema mradi huo umekuja wakati mwafaka kwa kuwa wilaya hiyo inakabiliwa na matatizo mbalimbali ya utoaji elimu kwa watoto wenye ulemavu.

Mwenyekiti wa Shirika la Foundation for Disabilities Hope (FDH), Michael Salali, anawataka wazazi, walezi wa watoto wenye ulemavu kuacha kuwaficha bali wawapeleke shule na kupata elimu itakayowasaidia kuondokana na utegemezi.

Salali, anabainisha hayo wakati akizungumza na wakazi wa Kata ya Mazae wilayani Mpwapwa ikiwa na sehemu ya utekelezaji wa mradi huo.

Anasema, watoto wenye ulemavu wanastahili elimu kama ilivyo kwa wengine hivyo siyo busara kuendelea kuwaficha ndani na kuwanyanyapaa.

"Mimi ni mlemavu ninaishi na ualbino lakini maisha yangu hayana ulemavu nikikupa leo 10,000 yangu haiwezi kuwa na ulemavu nilionao lakini hata haya maneno ninayoongea hayana ulemavu hivyo ni lazima wazazi tuwape watoto wetu haki ya kupata elimu badala ya kuwaficha ndani," anasisitiza.

Aidha, anasema kutokana na ulemavu huo, akiwa mdogo alinusurika kuuawa lakini wazazi wake hawakukubali walimtorosha ili kumlinda na wauaji na kuongeza: "Nawashukuru wazazi wangu kunitorosha labda leo ningekuwa nimekufa muda mrefu watu walitaka kunimaliza kwa milioni 300, na kuwapa nyumba na magari wazazi wangu."

"Kama wangekuwa wana tamaa za mali wangeniuza lakini leo niko hai. Huenda hata fedha walizopewa zingekuwa zimemalizika na mimi wasingeniona tena," anasema kwa uchungu.

Akizungumzia lengo la shirika hilo anasema nikuhamasisha jamii kuona umuhimu wa watoto wenye ulemavu kwenda shule na serikali kuboresha miundombinu ili kuweka mazingira wezeshi ya kujifunzia.

Mtaalamu wa masuala ya elimu jumuishi, Jane Mgidange, anawataka wazazi na walezi wenye watoto wenye ulemavu kuwatoa ili wabainishwe na kupatiwa mahitaji ya msingi.

Anasema, mtoto mwenye ulemavu kama atapatiwa fursa ya kwenda shule na kuwekewa mazingira rafiki anao uwezo kufanya vizuri kama ilivyokuwa wasiyo na ulemavu.

Anazitaja sababu mbalimbali ambazo zinaweza kuchangia ulemavu ikiwa ni pamoja na wajawazito kujifungulia nyumbani badala ya hospitali na kusisitiza kuwa wanapaswa kuhudhuria vituo vya afya wanapojihisi kuwa na mimba, kujifungua na baada ya uzazi wanatakiwa kuwapatia chanjo zote watoto wao ili kuwalinda.

"Chanjo ni suala la muhimu sana kwa watoto ili kujikinga na magonjwa kama polio ambayo yamekuwa yakisababisha ulemavu kwa watoto," anasema Jane.

Kuhusu ulemavu wa akili anasema umekuwa ukisababishwa na matumizi ya dawa za kulevya pamoja na msongo wa mawazo hivyo wazazi na walezi wajitahidi kusimamia watoto wao kujiepusha na janga hilo.

Diwani wa Kata ya Mazae, William Madanya, anasema: "Ulemavu ni jambo linalokuja muda wowote ule hivyo hatupaswi kuwachukulia kama kitu cha ajabu lazima tuwape ushirikiano mfano mapato ya ndani ya halmashauri wapo wenye ulemavu ambao wamekopa kwa ajili ya kuanzisha miradi yao ya kujikwamua kiuchumi."

# Ufugaji kuku Dar unavyozidi kuwa pasua kichwa, magonjwa, vifo balaa

INATOKA UK. 13

nyingine ni kutumia dawa za asili kama mwarobaini, alovera, mchanganyiko wa mlonge na vitunguu saumu, mnyaa au kuwapaka dawa za binadamu kama GV, mafuta ya taa, ya nazi, au dettol kwenye vidonda bado maradhi haya yameendelea kuwa kitisho.

Anashauri kuwapo kwa maelekezo ya kitaalamu ili kufahamu 'dozi' ya dawa asilia zitakazoleta matokeo bora.

Wana wasiwasi kuwa huenda utoaji dawa madukani haufanyiki kwa makini wengine wanasema uweke kwenye macho, uichanganye na chakula au maji, anaeleza Joan.

**KUCHAKACHUA**

Wafugaji wanaonyesha hofu kuwa huenda kuna kuchakachua dawa na kusababisha madhara ndiyo maana maradhi hayaishi wala kupungua na kila mwaka wanapata hasara.

"Dawa inapochanganywa na kitu kingine mfugaji hawezi kujua kama wafugaji watapewa dawa na kuambiwa kuwa ni chanjo hawana la kufanya wataona ipo ndani ya chupa au kwenye kasha au paketi."

Hatuna elimu ya kuzijua chanjo kama ni lazima ziwe vimiminika au zihifadhiwe kwenye chupa, au kuna za poda zinawekwa kwenye pakiti za plastiki yote hayo wanahitaji kuelimishwa.

**MAONI KITAALAMU**

Akitoa maoni ya kitaalamu Kilonzo Festo, ambaye amewahi kufanyakazi katika Chuo cha Kilimo Sokoine-(SUA), anapoulizwa kuhusu matatizo ya ufugaji mijini, anasema mara nyingi kuku wa kisasa wanashambuliwa zaidi na maradhi.

Lakini, akakumbusha kuwa ni lazima kuwatibu na kufuata ratiba ya kuwachanja, akisema kwa mfano kifaranga ni lazima achanjwe ndui baada ya siku saba, 14 na 21.



Kufuga kuku, mradi unaopunguza umaskini mjini lakini unamatatizo hasa maradhi na vifo kwa muda mfupi. **PICHA: MTANDAO**

Baada ya siku 28 apate chanjo ya gomboro kuanzia hapo anatakiwa kuendelea kuchanjwa kila baada ya miezi mitatu.

Kilonzo anazungumzia pia suala la vyakula kuwa nalo ni changamoto kwa ndege hao akishauri kuwa ni vyema kuwapa vyakula na pia virutubisho na dawa za asili kama mlonge, mwarobaini pamoja na aloivera lakini kwa kufuata ushauri wa kitaalamu.

Anawashauri wafugaji kutumia elimu wanazozipata kwa wataalamu wa afya za mifugo, kuchanganya na uzoefu wanaoupata kwa waliofuga muda mrefu na pia kujifunza kupitia elimu mtandaoni kufahamu mambo mapya yanayoibuka kila wakati na namna ya kukabiliana nayo.

"Wenye uzoefu wana ujuzi, elimu wa masuala ya vyakula, dawa, mazingira na wana mifano ya mambo waliyopitia na kuyatatu kwenye mdondo, ndui na gomboro. Wafugaji wawatumie." Anashauri.

Aidha, anazungumzia vyakula na kushauri pia kuwa makini kwenye uandaaji na kwamba wakati mwingine vinaweza kutengenezwa kibiashara zaidi na kushauri kuwashirikisha wafugaji wazoefu ambao wanafahamu kanuni zake, virutubisho vya ziada na mbinu nyingi. Akizungumzia malalamiko ya dawa kuwa hazitibu na magonjwa kujirudia mara kwa mara, anasema maradhi mengi ya kuku yanasambazwa na virusi hivyo ni changamoto lakini ufumbuzi upo kwa kusikiliza wazoefu, watalaamu wa mifugo na kujifunza kwenye maandiko mitandaoni pia.

"Suala la usafi nalo ni muhimu. Kuku na mifugo mingine lazima iishi kwenye mabanda masafi. Ni vyema kuwawekea maranda au mapumba ya mbunga ili wasichafuke na kinyesi. Pia kufagia na kusafisha mara kwa mara ili wadudu wasizaliane," anakumbusha.

Baadhi ya majina ya kuku wa kigeni wanaofugwa Dar es Salaam na miji mingine ni pamoja na 'kuchi' kutoka Zambia na Malawi ambao ni weusi na wekundu, wapo kuroiler wanaotoka Uganda na Kenya.

Kuku hawa wanatajwa na wafugaji kuwa wanashambuliwa na magonjwa kwa kasi kuliko wale wa asilia. Hata hivyo magonjwa ya kuku huambukizwa na virusi hivyo usambaaji huwa wa kasi na vifo ni vya muda mfupi tatizo linalowakuta hata wale wa asilia.

## WANENAVYO MALENGA

### NI KALAMU NA MDOMO

Ni jeshi la pande mbili, kama likijizatiti,
Laweza shinda kuwili, nchi ipate tiketi,
Hata umeme kandili, nchi itapanda chati,
Ni kalamu na mdomo, hivyo vitumike vyema.

Kwa kalamu waandishi, waweza leta mtiti,
Kwa habari za uzushi, tukanaswa kwenye neti,
Likizushwa haliishi, hadi tupigwe vifuti,
Ni kalamu na mdomo, hivyo vitumike vyema.

Ya Rwanda kuyarudia, hayo yanauma eti,
Kalamu liwawangia, hadi likavunjwa geti,
Mdomo ukachangia, zikazagaa maiti,
Ni kalamu na mdomo, hivyo vitumike vyema.

Ona mnayo kalamu, wala haitemi noti,
Muandikayo muhimu, nchi yetu kuwa fiti,
Yanaweza kuwa sumu, yavunjevunje magoti,
Ni kalamu na mdomo, hivyo vitumike vyema.

Mdomo unafunguka, mvuto kama manati,
Kama yakueleweka, nchi inavaa suti,
Kama yake yananuka, yai bovu kwenye koti,
Ni kalamu na mdomo, hivyo vitumike vyema.

Tujengeni kwa mdomo, mnapotoa sauti,
Kosoa bila kikomo, kulisafisha kabati,
Na uvundo usiwemo, sawa na bovu tikiti,
Ni kalamu na mdomo, hivyo vitumike vyema.

Chunguza chunguza sana, jiwekee mikakati,
Yale unayoyaona, ya kuundiwa kamati,
Yasije yakatuvuna, hata kuzamisha boti,
Ni kalamu na mdomo, hivyo vitumike vyema.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Kwa uhaba na ughali huu sokoni ni zamu ya kugeukia mboga asilia

•Kuna 'mashonanguo, mlonge, derega, mkunungu na mlenda'



Kilimo bora cha mboga asilia kinawezekana ili kukabiliana na upungufu na uhaba sokoni. **PICHA: MTANDAO**

SEHEMU nyingi iwe mijini na vijijini kupata mboga ya kutosha familia kumejaa mashaka. Ni kwa sababu ya ukame, joto kali ardhini na mabadiliko ya tabianchi.

Bustani zinazotegemea kumwagiliwa na maji mtoni au kulimwa karibu na mabonde na mikondoni hazizalishi kikamilifu baada ya kukauka.

Jua ni kali, wadudu wanaotoboa mboga ni wengi na wakati mwingine mkulima anakata tamaa ndiyo maana hata hizo kidogo zinazoonekana sokoni zinauzwa ghali ni utafiti wa Nipashe uliofanyika kwenye soko la Mbezi Magufuli jijini Dar es Salaam.

Wakati hayo yakijiri wauza mboga wanaulizwa kwanini wasiuze mboga za majani za asili kama mlonge, mlenda na 'ngogwe' au nyanya chungu zenye ukali, jibu ni kwamba wateja hawajazizoea, pengine waanze kuwazoesha.

Kwa wanaofahamu, unapozitaja mboga za asili ni sawasawa na kuzungumzia shehena ya lishe na virutubisho muhimu kwa binadamu.

Mboga hizo ni rahisi kupatikana tena kwa gharama nafuu ikilinganishwa na mboga za kisasa kama spinachi, kabichi, mchicha lishe, sukuma wiki na bamia.

Uchunguzi unaofanywa na Nipashe kwenye baadhi ya masoko unabaini kuwa mboga za kisasa wakati huu ni ghali na familia yenye watu watano pengine itahitaji takribani Shilingi 3,000 kununua mboga za kutumiwa kwa mlo wa mchana na usiku.

Majani matano mpaka saba ya spinachi huuzwa kwa Shilingi 500 wakati fungu la mchicha lishe, tembele au majani ya maboga yanayoweza kubanwa na mkono mmoja huuzwa kwa gharama hiyo pia.

Fungu hilo ni dogo likitosha kuliwa mara moja na mtu mmoja, jambo linaloongeza tatizo la upatikanaji wa mboga, ndiyo maana ni wakati wa kuanza kula mboga za asilia.

Kwa upande wa mboga za asili ni nyingi ni kwa sababu kila mkoa au jamii ina mboga hizo, kwa mfano kuna majani ya mihogo au kisamvu, mlonge, mnavu, mchunga, mchicha wa asili na mlenda wa aina nyingi.

Mathalani, Wapare kutoka wilaya za Same na Mwanga hutumia mti uitwao 'msele' kupata mlenda unaoweza kuliwa mwaka mzima bila kujali kiangazi wala masika kwa vile huvunwa mtini na kutwangwa na kuchekeshwa na kinachotumika ni majani yake, mboga hizo hupatikana kwenye masoko ya maeneo zinakopatikana.

Kadhalika, kuna mboga za asili kama mashona nguo huitwa vimbara na mbwete, hizi zinapatikana zaidi wakati wa masika.

Zipo mboga kama mgagani ambao asili yake ni Dodoma, derega kutoka Iringa zinazostawi sehemu nyingi hata ukanda wa pwani, bila kusahau majani ya mkunungu na kanyani ambayo nayo hutoka Iringa pia.

Mboga za asili ni nyingi ambazo ni pamoja na mzubo unaoliwa na wakazi wa Mwanza na Shinyanga ambayo ni mchanganyiko wa majani ya maboga ya asili na matango ya asili.

Yanakaushwa na kusagwa na kuhifadhiwa ili kutumika wakati wa ukame kama sasa. Yanapopikwa huungwa na karanga, maziwa au mafuta na viungo vingine, anasema, Queen Geleja mkazi wa Goba, mwenye asili ya Mwanza.

Kadhalika kuna mlenda wa asili ambao wanavijiji wanaweza kuichuma na kuikausha na kuendelea kuutumia.

Bibi Mwajuma Ungando kutoka kijiji cha Nyamwage, mkoani Pwani, anayeishi Mbagala anasema wakazi wa Rufiji wana mboga nyingi za asili kama mwage ambao ni mtu unaostawi karibu na mito au mkondo wa maji.

"Unaweza kuliwa kama majani mabichi au mlenda ukiukaushwa. Kuna matembele maji yanapatikana mabondeni na nyingine nyingi zinazoota maeneo ambayo maji yamekauka," anasema.

Mtandao wa Healthline unakumbusha kuwa mboga hizo za asili huwa na uchungu unaoodhaniwa kuwa ni unatibu, lakini sio matibabu ila ni muhimu kwenye uimarishaji wa afya ili kusaidia mwili kufanya kazi vizuri zaidi.

Unasema mtandao kuwa ni jukumu linaloanzia kwenye utumbo hadi kuimarisha mfumo wa kinga, pia huondoa sumu mwilini na kurekebisha uzalishaji wa kemikali zikiwamo asidi zinazoweza kuusumbua mwili.

Aidha, unaeleza kuwa mboga za asili zimesheheni madini na vitamini nyeti kama, vitamin A, inayoongeza kinga mwilini na nguvu ya macho, folic acid iliyo muhimu kuzalisha damu na kujenga mfumo wa fahamu-ubongo na uti wa mgongo.

Zina vitamin C inayohitajika kutibu na kuponya seli zilizoumia. Ndani ya mboga hizo kuna madini mfano zink ambayo ni muhimu kuimarisha kinga ya mwili, hasa enzi hizi za corona, ebola na VVU na UKIMWI.

Anna Minja, mtaalamu wa lishe wa Shirika la MIICO linalofanyakazi zake mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, likishughulika na masuala ya kuboresha hali za wananchi vijijini kwenye kilimo na lishe bora, uchumi pamoja na usawa wa kijinsia, anasema utafiti uliofanywa na shirika hilo, umebainisha kuwa mboga za asili ni muhimu mno kwenye mlo.

Anaeleza kuwa zina utajiri mkubwa wa virutubisho, pia ni himilivu na zina uwezo wa kukabiliana na madiliko ya tabianchi, ikilinganishwa na mboga zinazozalishwa kwa mbegu za kisasa.

Anataja kwa mfano mchicha wa asili, ngogwe na bamia zimesheheni viini lishe kuliko ilivyo kwa mimea hiyo kutoka mbegu za kisasa.

Anasema ili kusaidia wakulima wadogo wanawake, MIICO inashirikiana na wadau kuwafunza utaalamu wa kuzalisha mbegu za mboga za asili na kuwauzia wakulima wengine vijijini.

Anaiambia Nipashe kuwa wanasambaza utaalamu huo Nyanda za Juu Kusini na kuutaja mkoa wa Songwe katika wilaya ya Mbozi kwenye kata za Mahenge na Igamba.

Anataja mbegu za mboga za asili zinazozalishwa kuwa ni mgagani, mchicha, mnavu na bamia na lengo la mradi ni kuboresha lishe ya wanafamilia vijijini na kupunguza udumavu na maradhi.

### KUTUNZA MBOGA ASILIA

Mabadiliko ya tabianchi yanaathiri mimea ya dawa, mboga asilia kwa kusababisha pengine ukame zinakauka, zinazozuia usambaaji kwenye mapori.

Baadhi ya mboga au mimea hiyo inapatikana kwenye maeneo ya kijiografia au mifumo ya ikolojia ambayo mabadiliko ya tabianchi huyaweka hatarini zaidi.

## HABARI PICHANI



Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Msingi ya Muheza Muslim ambaye ni Diwani wa Kata ya Masuguru, Mohamed Baghoza (kulia), akikagua ujenzi wa vyumba vya madarasa juzi. Kushoto ni Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Athumani Mchechu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Kawawa Kigogo Dar es Salaam, wakibeba mbao kwa matumizi ya shuleni kwao juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**





Viongozi wa Jeshi la Polisi mkoani Manyara wakiwa na Msaidizi wa Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) Tanzania, Dk. Majaliwa Marwa (wa tatu kulia) wakati wa makabidhiano ya jengo la Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi wilayani Simanjiro juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## CHEMSHABONGO NA -00 32 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. tendeka jambo kwa namna nzuri
5. kata, lokesheni
8. tokeza juu ya maji
9. kinyume cha faradhi
10.jambo linalokusudiwa kufanywa
11.sehemu mojawapo ya taasisi
13.madhubuti 18.thabiti
19.mkonge
22.viumbe wote
24.Wanasheria


Chini:
1. bakaya
2. sujudia
3. kasirika
4. kilevi
6. reli inayounganisha Tanzania na Zambia 7. huenda, pengine
12.sadikika 14.sadiki
15.shauku ya jambo
16.ukavu wa nchi
17.walii, sufii
20.walau
21.pengine 23.Uo



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

SAFARI
SOMALIA
MAMBA
FUMBO
LAOSI
BASATA
AMBATANA
ATIFALI
ANITA
AFIKI, IDI,
AMA, MEI, NNE
NDALA
MAKADIRIO

maoni SMS: 0755429240




Majibu toleo lililopita









# TBS yatoa vyeti, leseni 462 kwa wajasiriamali

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limesema katika kipindi cha kuanzia Aprili mpaka Oktoba mwaka huu limetoa vyeti na leseni 462, hatua ambayo imetokana na jitihada za serikali kudhibiti uuzwaji wa bidhaa zisizokidhi viwango vyenye ubora nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Lazaro Msasalaga, alibainisha hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa vyeti na leseni hizo zimetolewa kupitia kanda zake saba.

Alisema kati ya vyeti hivyo, 59 vimetolewa kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini 45 na Kanda ya Magharibi 14.

Alisema kati ya leseni na vyeti hivyo, 39 sawa na asilimia 66 vilitolewa kwa wajasiriamali wadogo vikihusisha bidhaa za vyakula, vipodozi, vifaa vya ujenzi, chaki, gesi, makaa ya mawe na vifungashio.

"Kwa kutambua mchango wa wajasiriamali na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali serikali inatoa huduma za ukaguzi, upimaji na ufuatiliaji wa bidhaa bila malipo ili kuwawezesha wajasiriamali wote kuingiza sokoni bidhaa zinazokidhi vigezo vyenye ubora," alisema.

Katibu Tawala Msaidizi, Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mwajabu Nyamkomola, alisema pamoja na utoaji wa leseni za kutumia alama ya ubora, aliomba TBS kuandaa na kusimamia viwango vya kitaifa, kuthibitisha ubora wa bidhaa zinazozalishwa au kuingizwa nchini.

Aliongeza kuwa TBS wana jukumu la kupima bidhaa za ugezi wa vifaa, kusajili bidhaa za vyakula, vipodozi na majengo ya kutayarishia, kuhifadhia na kuuzia vyakula sambamba na kuthibitisha mifumo ya usimamizi wa bidhaa na huduma.



Katibu Tawala Msaidizi, Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mkoa wa Mbeya, Mwajabu Nyamkomora, akikagua bidhaa za wajasiriamali zinazozalishwa na wafanyabiashara wa mikoa ya Nyanda za Kusini katika hafla ya utoaji vyeti na leseni za kutumia alama ya ubora jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## UVCCM yaomba fedha za mikopo kwa vikundi ziongezwe

Na Grace Mwakalinga, CHUNYA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, umeiomba serikali kuongeza fedha za mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kuwezesha vikundi hivyo kuendesha miradi mikubwa ya kimaendeleo na kujikwamua kiuchumi.

Mwenyekiti wa UVCCM, Wilaya ya Chunya, Leckson Mwakasuluka, alitoa kauli hiyo juzi walipofanya kongamano la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na utendaji kazi wake katika kuliletea maendeleo Taifa.

Alisema licha ya jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali katika kuwawezesha wananchi kiuchumi mwitikio umekuwa mkubwa hali inayosababisha mahitaji kuongezeka.

Alisema wananchi wengi wamejiingiza kwenye shughuli za uzalishaji mali na kujiunga kwenye vikundi na kuibua uhitaji wa mikopo mikubwa kwa ajili ya kuendesha miradi yao.

"Tunaishukuru serikali kwa kuanzisha utaratibu wa kutenga asilimia 10 ya mapato yake kutoa mikopo kwa wananchi hii imesaidia wananchi wengi kujiajiri na kuajiriwa, lakini kwa sasa mikopo inayotolewa haikidhi mahitaji yao tunaomba kiwango cha fedha kiongezeke ili wanaokopa wafanye miradi mikubwa yenye faida," alisema Mwakasuluka.

Alisema wajasirimali wanahitaji kupatiwa mitaji mikubwa ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa wanazozalisha kuliko ilivyo sasa ambapo hupata kiasi kidogo.

Baadhi ya wajasiriamali wilayani Chunya waliishukuru serikali kwa kuwapatia mikopo isiyokuwa na riba ambayo imewasaidia kukuza na kuboresha biashara zao.

Agatha Mwakyoma muuzaji wa mboga na matunda alisema mkopo umemsaidia kukuza biashara yake kutoka kuzungusha mtaani mpaka kufungua genge.

Alisema licha ya kuanzisha genge lakini bado ana ndoto ya kumiliki biashara kubwa ya mboga na matunda ambayo inahitaji mtaji mkubwa ili kufanikisha.

Mwakyoma alisema mpaka sasa kwenye kikundi chake cha watu saba walipatiwa Sh. milioni nne, kiasi ambacho hakitoshi hivyo aliiomba serikali kufanya tathmnini ya utoaji wa mikopo ili iwasaidie kutimiza malengo yao.

## Halmashauri Mbeya yatoa mil.925/- kwa vikundi 49

Na Grace Mwakalinga, MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, amekabidhi hundi ya Sh. milioni 925 kwa vikundi 49 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kufanya shughuli zao za uzalishaji mali.

Fedha hizo ni sehemu ya makusanyo ya mapato ya asilimia 10 katika halmashauri ambazo hutolewa bila riba kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Akizungumza juzi wakati wa kukabidhi fedha hizo kwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Dk .Tulia alisema fedha hizo ni mikopo isiyokuwa na riba kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali ili kuboresha shughuli wanazozifanya kama vile biashara, kilimo na ufugaji.

Hata hivyo aliwataka maofisa maendeleo ya jamii kwenye kata kusaidia vikundi vilivyokosa vigezo vya kupata mikopo hiyo kwa kutoa elimu ya namna ya kuomba mikopo hiyo.

Alisema kwa kufanya hivyo itasaidia wananchi wengi kunufaika, huku akivitaka vikundi vilivyopata fedha hizo kurejesha kwa wakati ili na wengine waweze kukopeshwa.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Triphonia Kisiga, alisema kati ya vikundi 49 vilivyonufaika, wanawake 38, vijana vikundi 10 na wenye walemavu kikundi kimoja na kubainisha kuwa kati ya fedha hizo Sh. milioni 325 zimetokana na mapato ya ndani na Sh. milioni 600 zinatokana na marejesho ya mikopo.

Kisiga alisema vikundi hivyo vimepata mikopo ya aina mbalimbali kama vile utekelezaji wa miradi ya ununuzi vifaa vya kilimo, ufugaji pamoja na usindikaji mazao huku watu 331 wakinufaika na mkopo huo.

Alisema katika kutekeleza utoaji wa mikopo hiyo Halmashauri ya Jiji la Mbeya ilihamasisha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuunda vikundi vya kiuchumi vyenye miradi yenye tija ya pamoja, ambayo itawapatia kipato na kujiletea maendeleo yao wenyewe.

Aliongeza kuwa halmashauri ilitoa elimu kwa vikundi kuhusu utunzaji wa kumbukumbu, matumizi sahihi ya fedha za biashara na kuboresha bidhaa zao ili kuweza kuingia katika soko la ushindani wa kibiashara, pamoja na kuwaunganisha na wataalamu wengine waliowapatia mafunzo ya kilimo na biashara zao.

Mwakilishi wa kikundi cha vijana kilichopata mkopo huo, Rajab Nelson alishukuru kupata fedha hizo ambazo zitawasaidia kuendesha shughuli zao kujiongezea kipato na kuahidi kurejesha kwa wakati ili wakopeshwe tena.





# Tanzania yauza tani 1,423 za nyama nje ya nchi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TANZANIA imeuza tani za nyama 1,423 nje ya nchi zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 5.3 (Sh. bilioni 10) kwa kipindi cha Novemba.

Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania (TMB), Dk. Daniel Mushi, alibainisha hayo jana ofisini kwake jijini hapo wakati akitoa tathmini ya maendeleo ya uuzaji nyama nje ya nchi kwa kipindi cha Novemba mwaka huu.

Dk. Mushi, alisema kiasi hicho ni sawa na ongezeko la asilimia 125, ikilinganishwa na tani 632 zilizouzwa Oktoba mwaka huu.

Alisema kuwa mauzo ya nyama nje ya nchi kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 15 mwaka huu ni tani 5,158.93 sawa na ongezeko la asilimia 21.7 ikilinganishwa na tani 4,239.42 ambazo ziliuzwa kipindi kama hicho mwaka jana.

"Tani 1,423 za nyama zilizouzwa Novemba mwaka huu ni sawa na ongezeko la asilimia 62 ikilinganishwa na tani 878 zilizouzwa Novemba mwaka jana ikiwa ni ongezeko la tani 545," alisema Dk. Mushi.

Kadhalika alisema mchanganuo wa tani hizo za nyama zilizouzwa ni nyama ya mbuzi tani 1,047, nyama ya kondoo tani 343, nyama ya ng'ombe tani 32, nyama ya kuku tani 0.67 nyama ya nguruwe 0.2.

Meneja wa Idara ya Masoko TMB, John Chassama, alisema zaidi ya nchi sita zimeshiriki kununua tani hizo ikiwamo Qatar tani 504, Oman tani 334, UAE tani 267, Saudi Arabia tani 125, Kuwait tani 56, Bahrain tani 50 na China tani 38.

Katika hatua nyingine Chassama alieleza sababu za nyama ya mbuzi kuuzwa zaidi kuliko nyingine ni kutokana na mahitaji yake kuwa juu zaidi sokoni na upatikanaji wa mbuzi kama malighafi kwenye viwanda vya nyama ni rahisi ukilinganisha na mifugo mingine.

Pia alitoa wito kwa vijana kutumia fursa ya kufuga kibiashara kwani soko la uhakika la mifugo lipo.

Alisema kwa namna kiwango cha nyama kinachouzwa nje kinapoendelea kukua ndivyo mahitaji ya mifugo ambayo ndiyo malighafi kwenye viwanda vya nyama nayo yanaongezeka.

Hata hivyo alisema ili kuendelea kuuza zaidi nyama nje ya nchi wananchi wanatakiwa kubadilika na kufuga kisasa ili kupata nyama iliyo bora na itakayoweza kushindana katika masoko ya kimataifa.

Mmoja wa wafugaji ambaye ni mfanyabiashara wa nyama jijini hapo, Emmanuel Stanley aliipongeza TMB, kwa kuwaunganisha na wafanyabiashara kutoka nje ya nchi hali inayosababisha wajikite zaidi katika ufugaji wa kisasa kutokana na uhakika wa soko.

Hata hivyo aliiomba TMB, kuendelea kutoa elimu kwa wafugaji na wafanyabiashara wa nyama juu ya namna bora ya ufugaji wa kisasa ambao gharama yake ni ndogo ukilinganisha na faida itakayopatikana baada ya kuvuna mifugo yake.

## Watu wenye ulemavu washauriwa kujiunga kupata mikopo

**Na Peter Mkwavil,** DODOMA

WATU wenye ulemavu wamehamasishwa kujiunga kwenye vikundi ili kupatiwa mikopo ya asilimia mbili inayotolewa na halmashauri badala ya kukaa nyumbani kusubiri misaada kutoka kwa wahisani.

Wito huo ulitolewa na Ofisa Elimu Maalumu wa Jiji la Dodoma, Issa Kambi alipokuwa akizungumza na wadau wa elimu jumuishi wakiwamo wazazi na walezi wanaoishi na watoto wenye ulemavu kwenye kongamano lililofanyika jijini hapo.

Kambi alisema kuwa badala ya kukaa majumbani na kusubiri misaada hiyo ni wakati wao sasa wa kuchangamkia na kuunda vikundi ili fursa hiyo ya mikopo inayotolewa waweze kuipata.

"Napenda niwaambie wazazi na walezi ambao mnaoishi na familia na watoto wenye ulemavu kuwa fedha zipo kila zinapotolewa bado zinabaki, hivyo niwasihii muunde vikundi ili mpate badala ya kukaa majumbani huko mkisubiri misaada kutoka kwa marafiki.

Pia alizionya familia ambazo zinazofanyiwa ukatili dhidi ya watoto kutokubali kukaa bila kutoa taarifa badala yake washirikiane na serikali kufichua vitendo hivyo kwa ajili ya kuvikomesha.

Mratibu wa Elimu Jumuishi Jiji la Dodoma na Bahi, Jane Mgidange, alisema bado kuna kiwango kidogo cha usajili wa watoto wenye ulemavu, kutokana na miundombinu ya shule kutokuwa rafiki pamoja na idadi ndogo ya walimu wenye utaalamu.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (kulia), akiongoza kikao kazi na viongozi wa idara mbalimbali za mkoa huo jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Machinga wampa kongole Samia ujenzi soko la kisasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wadogo jijini Dodoma (Machinga) wampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwajengea soko la kisasa ambalo limewawezesha kuondokana na adha ya kunyeshewa mvua wakati wa masika.

Walitoa pongezi hizo juzi jijini hapo wakati wakizungumza na waandishi wa habari kuhusu faida za soko hilo la kisasa ambalo ujenzi wake umegharimu Sh. bilioni 9.5.

Mfanyabiashara wa nguo za kike na kiume, Bahati Rajabu maarufu Cheupe, alimpongeza Rais Samia kwa kukubali kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kujenga soko hilo ambalo kwa sasa matunda yameanza kuonekana.

Alisema awali walikuwa hawajaelewa ni ipi dhamira ya serikali lakini sasa wameelewa kwa sababu mitaa mingi ya Jiji la Dodoma inapendeza na machinga wote wapo katika eneo moja.

"Nampongeza Rais Dk. Samia kwa kutupa zawadi ya soko hili la kisasa kiukweli kwa sasa tunafanya biashara zetu kwa uhuru na wateja ni wengi kila unayemuuliza huku ndani atakwambia kwa sasa anauza zaidi ya mara mbili kuliko alivyokuwa mtaani,"alisema.

Mfanyabiashara wa vitu vya urembo, Selemani Mahomba, alisema soko hilo limejengwa kwa viwango lakini kero inayowakumba machinga wengi ni ukosefu wa mitaji ya kueleweka.

Alisema wengi wanatamani kuchukua mikopo inayotolewa na serikali lakini kikwazo ni umri kwasababu wanaweka masharti kuwa mikopo hiyo inatolewa kwa watu walio na umri chini ya miaka 35.

"Tunaishukuru serikali kwa kutujengea soko hili la kisasa lakini kero kubwa ni ukosefu wa mitaji kwa machinga ambapo wengi wamezidi umri wa miaka 35 tunaomba suala hili liangaliwe vizuri ili watu wote wanufaike na mikopo hiyo," alisema.

Mwenyekiti wa machinga Wilaya ya Dodoma Mjini, Shaban Kisamvu, alisema kwa sasa kero iliyoko katika soko hilo ni kutokuwapo kwa kituo kikubwa cha magari ya abiria.

Alisema suala hilo tayari lilishafika kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na akatolea maelekezo, hivyo wanatarajia wakati wowote suala hili litatekelezwa.

"Daladala zikianza kuja hapa kiukweli machinga watakuwa mabilionea kwa sababu watafanya biashara kwa saa 24 na ndiyo dhamira ya serikali ya kuwainua watu wake kiuchumi na kwa sula hili tunampongeza sana Rais Dk. Samia kwa kuacha alama hii ambayo haitafutika," alibainisha.

Ofisa Biashara wa Jiji la Dodoma, Donatila Vedasto, alisema soko hilo limezingatia suala la ulinzi na usalama wa watu na mali zao kwani kuna kituo cha polisi ambacho kinafanya kazi saa 24.

Alisema pia kumefungwa mifumo ya kisasa yaTEHAMA na mfumo wa camera za usalama ili kuhakikisha wafanyabiashara, wateja na mali zao wanakuwa salama wakati wote.



## HABARI ZANZIBAR

# Mifumo biashara kukuza masoko bidhaa kimataifa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, amesema utumiaji wa mifumo ya biashara utasaidia kukuza na kurahisisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa ndani na nje ya nchi.

Aliyasema hayo jana mjini hapo, wakati akifungua mafunzo ya utumiaji wa mifumo ya biashara Zanzibar kwa viongozi wa umma na taasisi binafsi zinazohusu biashara.

Alisema hatua hiyo ni kubwa katika kutimiza azma ya serikali ya kuhakikisha inakwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ya dunia kwa kufuata mfumo wa kibiashara ili kurahisisha kukuza biashara pamoja na kupata masoko kwa urahisi ya ndani na nje ya nchi.

Aidha, alisema mfumo huo utasaidia kupata taarifa mbalimbali ikiwamo za masoko ya biashara za kimataifa kupata vibali, leseni na kujua vigezo vya biashara pamoja na kufanya uamuzi sahihi wa nchi zinazotoa bidhaa bora.

Aliwataka viongozi hao kusimamia mfumo huo na kuwaeleza wafanyabiashara jinsi ya mwenendo wa soko duniani pamoja na kushuka na kupanda kwa bei za bidhaa.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Rashid Ali Salim, alisema mfumo wa uwezeshaji biashara unasimamiwa na mamlaka ya maendeleo ya biashara Tanzania TanTrade.

**Aliyasema hayo jana mjini hapo, wakati akifungua mafunzo ya utumiaji wa mifumo ya biashara Zanzibar kwa viongozi wa umma na taasisi binafsi zinazohusu biashara.**

TanTrade ni chombo cha serikali chenye mamlaka ya udhibiti, utendaji na ushauri wa kuendeleza na kukuza biashara za ndani na nje ya nchi.

Alisema, dhima ya mamlaka hiyo ni kuwezesha ukuaji wa uchumi wa Tanzania kwa kuendeleza na kukuza bidhaa na huduma mbalimbali kwa masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mkufunzi wa mafunzo hayo mshauri wa mfumo wa taarifa za Biashara TanTrade, Gema Mwikoko, alisema iko haja ya wakuu wa taasisi kuwashajihisha wafanyabiashara kujisajili katika mfumo huo ambao utawapatia mbinu za kibiashara pamoja na kupata masoko ya kikanda na kimataifa.

## Wananchi wahakikishiwa huduma ya majisafi na salama

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Serikali ya Zanzibar itaendelea kuwapatia huduma ya majisafi na salama wananchi wake ili kumaliza tatizo la upatikanaji wa huduma hiyo nchini.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya mji wa Zanzibar, alisema upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa Zanzibar umefikia asilimia 66 hali inayoonesha namna serikali ilivyojikita kuwapatia huduma hiyo wananchi wake.

Aliwataka wananchi kuendelea kushirikiana na serikali katika kuitunza miundombinu ya maji ili idumu kwa muda mrefu na kuwafaa wananchi wengi.

"Nachukua nafasi hii kutoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na serikali kuitunza na kuienzi miundombinu inayopita katika maeneo yao wanayoishi ikiwamo miundombinu ya maji," alisema.

Akizungumzia sekta ya afya alisema, serikali imeridhika na ujenzi wa hospitali za wilaya na mkoa ilipofikia na kuagiza uongozi wa Wizara ya Afya kuendelea kuwasimamia makandarasi ili kukamilisha ujenzi huo kwa wakati.

Aidha, alisema serikali imejipanga kuweka vifaa vya kisasa pamoja na kuhakikisha hospitali zote zina madaktari bingwa na wataalamu wote wa afya wanaohitajika katika kuwapatia huduma bora wananchi wake.

Alisema serikali imepunguza gharama za uungwaji wa umeme kwa wananchi wake ili waishi maisha bora kwa kufurahia huduma hiyo.

Alisema serikali itachukua hatua kali za kisheria kwa mtumishi atakayekwenda kinyume na sheria za utumishi na kuwataka wananchi kutojihusisha na masuala ya uvujaji wa mapato wa Shirika la Umeme ikiwamo kuchezea mita kwa kuiba umeme.

Hata hivyo, Hemed aliwataka Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwa mstari wa mbele kusimamia ukusanyaji wa mapato na kuwataka wananchi kushirikiana na mamlaka husika kusaidia suala la ukusanyaji wa mapato.




Mkurugenzi wa Jumuiya ya Wajane Zanzibar, Tabia Makame, akizungumza na wanachama wa jumuiya hiyo (hawapo pichani) Micheweni kisiwani Pemba jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Kamati ya pamoja kupunguza migogoro kwa wavuvi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa kamati ya wavuvi wa vijiji saba vinavyoizunguka huba ya Chwaka, Mkoa wa Kusini Unguja wamesema uamuzi wa serikali kuunda kamati ya pamoja ya usimamizi wa uhifadhi wa rasilimali za bahari utasaidia kupunguza migogoro ya mara kwa mara inayoendelea kujitokeza kwa baadhi ya wavuvi wa vijiji hivyo.

Waliyasema hayo jana katika kikao cha pamoja kilichowashirikisha maofisa kutoka Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, idara ya maeneo ya hifadhi ya mwambao ya bahari pamoja na maofisa uvuvi wa wilaya.

Kikao hicho kilifanyika katika Ofisi za Mkoa wa Kusini Unguja huko Tunguu lengo likiwa ni kuchagua viongozi watakaosimamia kamati hiyo.

Juma Awesu, alisema suala la utunzaji wa rasilimali za bahari lina umuhimu wa kipekee hasa kwa wakati huu ambapo viongozi wa nchi wamejikita kutekeleza sera ya uchumi wa buluu.

Alisema ni vyema kwa jamii na wavuvi wakatoa ushirikiano kwa kamati hiyo mpya iliyoundwa ili kuleta mabadiliko katika sekta ya uvuvi.

"Migogoro mingi ya uvuvi inatokana na kutokuwa na chombo maalum cha kusimamia rasilimali za bahari hivyo imani yetu kuwa kamati hii itakuwa msimamizi mzuri wa wavuvi," alisema.


Ofisa kutoka Idara ya Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari, Thuwaiba Kassim Haji, alisema ameridhishwa na hatua ya wajumbe wa kamati ya uvuvi kwa kuchagua viongozi na hatua hiyo itasaidia kuondokana na changamoto zilizoko hapo awali huku akiendelea kusisitiza kutunza rasilimali za bahari ili kuwanufaisha na kupata maendeleo kwa vizazi vya sasa na baadaye.

Akifungua kikao hicho, Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Kusini Unguja, Yahya Jabir Mwadini, aliwataka wajumbe wa kamati hiyo kuwa na ushirikiano wa pamoja kwa kuitunza rasilimali ya bahari kwa maslahi ya taifa.

Alisema bila ya bahari kulindwa na kuhifadhiwa samaki watakosekana na kuwataka wavuvi hao kuwa mabalozi wazuri wa kulinda rasilimali za bahari.

Aliwataka kuachana na uvuvi haramu ambao ndiyo chanzo cha uharibifu wa mazingira baharini ikiwamo kutoweka kwa matumbawe ambayo ni mazalia ya samaki.

Katika kikao hicho wajumbe wamemchagua Masoud Mohd Abdalla, kuwa Mwenyekiti wa kamati hiyo huku wakipendekeza jina la kamati hiyo iitwe Chwaka Bay (CMG) ikiwa na maana ya kamati ya usimamizi wa pamoja yenye shehia saba ikiwamo Shehia ya Uroa, Marumbi, Chwaka, Charawe, Ukongoroni, Michamvi na Pongwe Pwani.



# Waziri Katambi akoshwa utoaji mikopo halmashauri

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MBUNGE wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, ameridhishwa na utoaji wa fedha za mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri kwenda kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Katambi ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, aliyasema hayo juzi wakati akizindua miradi ya kiuchumi katika Manispaa ya Shinyanga.

Miongoni mwa miradi hiyo ni soko la machinga, kituo cha biashara pamoja na kukabidhi gari la biashara kwa kikundi cha vijana. Alisema anafarijika kuona malengo ya Rais Samia Suluhu Hassan juu ya fedha hizo za mikopo yanatimia kwa kuwa walengwa wanafikiwa.

Alisema fedha hizo zinaviwezesha vikundi mbalimbali vya wajasiriamali kuanzisha miradi mikubwa yenye tija ambayo itawanyanyua kiuchumi na hivyo kupanua wigo wa ajira.

"Napongeza utoaji wa fedha za mikopo asilimia 10 katika Halmashauri ya Shinyanga, mnatoa fedha nyingi na kuanzishwa miradi yenye tija, hii ndiyo adhima ya Rais Samia kuwa fedha hizi ziwafikie walengwa na kuwanyanyua kiuchumi," alisema Katambi.

Aidha, alitoa wito kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuendelea kujiunga kwenye vikundi na kubuni miradi mikubwa yenye tija ili kupanua wigo wa ajira.

Katika hatua nyingine Katambi aliupongeza uongozi wa Manispaa ya Shinyanga kwa kuendelea kuimarisha miundombinu ya kiuchumi katika manispaa hiyo ikiwamo ujenzi wa masoko, stendi za mabasi na barabara.

Pia aliahidi kuendelea kushirikiana nao ili kuubadilisha mji huo kuwa na hadhi ya Jiji.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, John Tesha, alisema kuanzia Januari hadi Desemba mwaka huu wametoa Sh. milioni 273.

Alisema kwa takwimu za kuanzia mwaka 2015 hadi 2022, halmashauri hiyo imeshatoa fedha za mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu zaidi ya Sh. bilioni moja kwa vikundi 175.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Jomaary Satura, alisema kazi ya serikali ni kuboresha mazingira ya biashara kwa wananchi na kwamba wameanza kuimarisha huduma muhimu za kiuchumi ikiwamo ujenzi wa masoko, stendi za mabasi, kuboresha kituo cha urasimishaji, uwekezaji, uendelezaji wa biashara na utoaji wa mikopo kwa miradi yenye tija.



Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, akionyesha vifaa vya Zahanati ya Uyongo katika Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama, ambavyo wamevikamata katika operesheni waliyoifanya. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Jeshi la Polisi lawadaka watuhumiwa dawa za kulevya

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga limesema limekamata vitu mbalimbali vya wizi pamoja na dawa za kulevya, huku baadhi ya watuhumiwa wakitiwa mbaroni.

Kamanda wa Jeshi la Polisi, Janeth Magomi, aliyasema hayo wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari.

Alisema kwa kipindi cha Novemba 22 hadi Desemba 12 mwaka huu wamefanya msako na kukamata vitu mbalimbali vya wizi.

Kamanda Magomi alisema katika msako huo walikamata vifaa tiba vya Zahanati ya Uyongo katika Halmashauri ya Ushetu, bunduki moja aina ya gobore, simu za mkononi 17, pikipiki 10, dawa za kulevya aina ya heroine 10, bangi misokoto 71, televisheni nne, mitungi ya gesi miwili na lita 20 za pombe ya gongo.

Alitaja vitu vingine walivyokamata ni vyuma vya ujenzi wa minara ya Shirika la Umeme Nchini (TANESCO), spika mbili, vitenge doti nne, kompyuta tatu, redio nne, godoro moja, panga moja, shoka moja, makabati mawili ya kuhifadhia chips, pikipiki nane na baiskeli 11.

Kamanda Magomi alisema: "Watuhumiwa ambao wamejihusisha na wizi wa vitu hivi tunawashikilia, wengine tumewafikisha mahakamani na baadhi yao wamehukumiwa kwenda jela."

Katika hatua nyingine Kamanda Magomi alitoa wito kwa madereva wa vyombo vya moto mkoani humo kuwa makini katika kipindi hiki cha sikukuu na kuwataka wazingatie sheria za usalama barabarani ili kuepuka ajali zisizo za lazima.

Aidha, alitaja idadi ya makosa ya usalama barabara ambayo yamepatikana kwa kipindi cha mwezi mmoja ni pamoja na makosa 2,796, pikipiki 937 na wahusika wote walichukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kulipa faini.

Kamanda Magomi aliwataka wananchi wa mkoa huo kuacha kujihusisha na masuala ya vitendo vya uhalifu hususani katika kipindi cha sikukuu za mwisho wa mwaka kwa kuwa Jeshi la Polisi limejipanga kukabiliana na vitendo hivyo.

# Mgogoro wazuka mwekezaji, mmiliki shamba la dhahabu

**Na Alphonce Kabilondo,**
GEITA

MGOGORO umeibuka katika shamba lililogundulika kuwa na madini ya dhahabu katika kitongoji cha Nyamahuna, Kijiji cha Sobola Kata ya Magenge mkoani Geita baada ya mmiliki wa eneo hilo kumkataa mwekezaji, Hussein Nyamanche anayedaiwa kuwa na leseni ndogo ya uchimbaji katika eneo hilo.

Hatua hiyo imetokana na mwekezaji huyo kudaiwa kuwatumia baadhi ya viongozi wa kijiji na tarafa kumshinikiza mwenye shamba akubaliane na mgao wa asilimia moja ya mapato ya dhahabu tofauti na ilivyokuwa awali iliyokuwa asilimia 13 hadi 17.

Akizungumza na Nipashe mgodini hapo mmiliki wa shamba hilo, Batende Mayombo alisema kuwa mwekezaji huyo ameibuka baada ya eneo hilo kugundulika kuwa na madini ya dhahabu Oktoba mwaka huu.

Alisema kuwa Novemba mwaka huu anayedaiwa kuwa mmiliki wa leseni alifika kwenye shamba lake baada ya kugundulika kuwa na madini hayo.

Mayombo alisema eneo hilo ni shamba lake ambalo pia analitumia kama makazi lenye ukubwa wa ekari tano na kwamba mwekezaji huyo alipoibuka kwa mara ya kwanza akiwa na leseni walikubaliana awe anampa asilimia 13 ya mgawo kwa madini yanayochimbwa humo.

Alisema kuwa baada ya kufika eneo hilo waliweka makubaliano ya mgawo wa asilimia 13 hadi 17, lakini alishangaa kuona mtu huyo akimgeuka na kuvunja makubaliano hayo.

Alifafanua kuwa maofisa madini kutoka mkoani Geita, walipotembelea eneo hilo Novemba 26, mwaka huu mwekezaji huyo alipohojiwa kuainisha ukubwa wa eneo lake analomiliki alishindwa kuwaonyesha.

Alisema Novemba 27, mwekezaji huyo alikwenda katika eneo hilo akiwa ameambatana na watu kadhaa kwa lengo la kupima ukubwa wa eneo hilo, lakini walimzuia wakimtaka kufuata sheria, kanuni na utaratibu wa masuala ya uchimbaji wa madini. "Hali hii inanifanya kuwa na mashaka na uhalali wa leseni hiyo kwa kuwa kuna taarifa kwamba eneo hili lina leseni mbili nani mwenye leseni halali, naomba serikali iingilie kati kumaliza mgogoro huu," alisema.

Meneja wa mgodi huo aliyejitambulisha kwa jina la Moris alipotakiwa kuzungumzia mgogoro huo alisema kuwa atafutwe mkurugenzi ambaye ni mmiliki wa leseni ya uchimbaji.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Sobola, Suzana Cherehan, alikiri kuutambua mgororo huo na kusema Novemba 29, mwaka huu, mmiliki wa shamba hilo alipelekwa Kituo cha Polisi Katoro na mmiliki huyo wa leseni.

Alisema: "Ni kweli mgogoro huu naufahamu nilipigiwa simu Novemba 29 na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Magenge nikaambiwa niende na mmiliki wa shamba Kituo cha Polisi Katoro anahitajika nami nilifanya hivyo.

"Tulipofika kituoni hapo tulimkuta Hussein na Ofisa Mtendaji wa Kata na Katibu Tarafa wa Butundwe pamoja na askari polisi mmoja na walifanya mazungumzo, lakini hawakufikia mwafaka."

Akizungumza na Nipashe Kaimu Mtendaji wa Tume ya Madini, Yahaya Samamba alisema hakuna mtu yoyote anayeruhusiwa kufanya shughuli za uchimbaji wa madini ya dhahabu kwenye eneo au shamba la mtu bila makubaliano na mmiliki.

HABARI KIMATAIFA

# Katumbi aibua muungano vyama tawala DRC

**KINSHASA, DRC**

BAADA ya kiongozi wa upinzani nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Moses Katumbi, kutangaza rasmi kuwania urais 2023, muungano wa vyama vilivyo madarakani wametoa wito kwa raia kutochagua mgombea mwenye uraia wenye mashaka.

Kupitia tangazo lake la kugombea urais alilolitoa jana, gavana huyo wa zamani wa mkoa wa Katanga ambaye ni kiongozi wa Chama cha Ensemble pour la République, alihakikisha kujiondoa katika muungano wa vyama vinavyomuunga mkono Rais Félix Tshisekedi. Muungano wa vyama tawala unaodai kuunga mkono demokrasia nchini DRC, umeeleza kuwa hauwezi kutishwa na ugombea wa Moses Katumbi, ila sharti akidhi vigezo vilivyowekwa na sheria ya uchaguzi pamoja na katiba ya nchi hiyo.

Kwa mjibu wa Thierry Monsenepo, mmoja wa viongozi wa muungano huo, Rais Félix Tshisekedi, aliutumia muhula wake wa kwanza ipasavyo kwa kutekeleza aliyoyaahidi na sasa anataka kuendelea kuhudumu tena kwa muhula wa pili.

Monsenepo amewataka Wakongo kuchagua kati yake na Moses Katumbi ambaye uraia wake unabaki wa mashaka na Tshisekedi.

"Kumbukeni kuna wakati Katumbi alijitokeza mbele ya hadhara ya raia wa Kiyahudi akiwaeleza kuwa yeye anachukuliwa hapa Kongo kwani yeye ni mtoto wao," alisema.

Pia alisema baba wa mwanasiasa huyo ni Mtaliano wa asili ya Kiyahudi na mama yake ni Mzambia.

"Hana uhusiano wowote kuhusu uraia wa Kongo kufuatana na yale yanayoelezwa na katiba ili kudai kuwa mgombea wa urais wa Jamhuri," alisema.

Inabainishwa kuwa utawala wa rais wa zamani, Joseph Kabila, uliwahi kumshutumu Katumbi kuwa si raia wa Kongo na hivyo ukamnyang'anya pasipoti yake, Rais Tshisekedi alipoingia madarakani, alimrejeshea pasipoti hiyo na kuthibitisha kwamba Katumbi ni raia wa Kongo.

Ilielezwa kuwa kinachowashangaza wananchi ni kuona utawala huo huo ndio unaeleza sasa kwamba Katumbi ni mgeni.

Licha ya Katumbi kuwa mshirika katika muungano wa Tshisekedi, wawili hao waliishi kwa mashaka makubwa na kutoaminiana kipindi chote cha kuwamo kwenye muungano huo.

Hatua ya kujiondoa kwake kutoka muungano huo ilikuwa kumetarajiwa, na wafuatiliaji wa siasa za nchini humo kutokana na mienendo ya mwanasiasa huyo.

Anselme Kyungu, mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Kolwezi mkoani Lualaba, aliiambia DW kwamba hilo si jambo la kushangaza kwani Moses hajawahi kuwa mshirika wa Tshisekedi isipokuwa tu kwa maslahi. "Wengi wa wanachama wake walieleza kwamba hawawezi kufanya siasa bila kuchukuwa madaraka. Yaani wengi wako katika muungano wa rais pia serikalini kwa maslahi yao tu. Unajua mara nyingi kulikuwa na jaribio la kujitenga," alisema.

Kwa mujibu wa DW, jina la Moses Katumbi limeongezwa kwenye orodha ya wagombea ambao wamejitangaza rasmi kupambana na Rais Félix Tshisekedi mwakani.

Wengine ni mawaziri wakuu wa zamani, Augustin Matata na Adolphe Muzito, pamoja na viongozi wengine wa upinzani, akiwamo Martin Fayulu, Justin Mudekereza na Jean-Marc Kabund. Uchaguzi unatarajiwa kufanyika Desemba 20, 2023.

***DW***




Wanaharakati wakiandamana jijini London kupinga mpango wa serikali ya Uingereza kuwasafirisha wahamiaji haramu nchini Rwanda. **PICHA: AP**

# Mahakama Uingereza kuamua uhalali wahamiaji kusafirishwa

**LONDON, Uingereza**

MAJAJI katika Mahakama Kuu jijini London, wanatarajiwa kufanya uamuzi leo iwapo mpango wa serikali ya Uingereza, kuwasafirisha wahamiaji haramu nchini Rwanda ni halali kisheria.

Kwa mujibu wa ripoti iliyochapishwa jana na RFI, uamuzi huo unatarajiwa, wakati Waziri Mkuu Rishi Sunak, akiapa kukabiliana na wahamiaji haramu wanaowasili nchini humo na kuendelea na mpango wa kuwasafirisha nchini Rwanda, ulianzishwa na mtangulizi wake Liz Truss.

Mkataba uliofikiwa kati ya Uingereza na Rwanda, ni kuwa, itatuma maelfu ya wahamiaji waliofika katika nchi hiyo kinyume cha sheria nchini Rwanda.

Safari ya kwanza, ilikuwa imepangwa kufanyika mwezi Juni, lakini ikasitishwa katika dakika za mwisho na Mahakama ya Haki ya Umoja wa Ulaya baada ya wanaharakati kwenda mahakamani.

Inaelezwa kuwa iwapo mahakama itaamua kuwa, Uingereza iko sahihi kisheria, haimaanishi kuwa safari hizo zitaanza mara moja kwa sababu bado kuna nafasi ya kukata rufani kutoka kwa wanaharakati wa haki za binadamu wanaopinga mpango huo.

Mbali na wanaharakati wa haki za binadamu, mpango huo wa serikali ya Uingereza, unapingwa na Umoja wa Mataifa na Mfalme Charles wa tatu.

***RFI***

**Mkataba uliofikiwa kati ya Uingereza na Rwanda, ni kuwa, itatuma maelfu ya wahamiaji waliofika katika nchi hiyo kinyume cha sheria nchini Rwanda.**

# Ramaphosa achaguliwa tena kuiongoza ANC

**CAPE TOWN, Afrika Kusini**

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, amechaguliwa tena kuwa kiongozi wa Chama tawala cha African National Congress (ANC), na ushindi wake unamweka katika nafasi nzuri ya kuongoza chama hicho katika uchaguzi wa 2024.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na BBC, Ramaphosa alimshinda mpinzani wake Zweli Mkhize kwa kura 2,476 dhidi ya 1,897.

Wakati hayo yakiendelea jopo la wataalamu wa sheria walioteuliwa na spika wa bunge, walisema kuwa kesi za kumfungulia mashtaka juu ya tuhuma zinazomkabili zinapaswa kuanzishwa kwa sababu anaweza kuwa alikiuka katiba na kuvunja sheria ya kupinga ufisadi.

Ilielezwa kuwa azma ya Ramaphosa kuchaguliwa tena iliimarishwa na ukweli kwamba ANC ilitumia wingi wake wa wabunge kupigia kura maoni ya jopo hilo.

Aidha, Rais Ramaphosa alikana kufanya makosa yoyote, na ameanzisha hatua za kisheria kubatilisha ripoti ya jopo hilo, akieleza kuwa dola 580,000 zilitokana na mauzo ya nyati, lakini jopo hilo lilisema kulikuwa na mashaka kama shughuli hiyo iliyofanyika.

Mkhize alikuwa waziri wa afya katika serikali ya Ramaphosa, hadi alipolazimika kujiuzulu mwaka jana kwa madai ya matumizi mabaya ya fedha zilizotengwa kukabiliana na janga la UVIKO-19.

Licha ya madai hayo, ilibainishwa kwamba alikana kuhusika na makosa yoyote, na wafuasi wake waliona madai hayo kama jaribio la kumchafua.

Inaelezwa kwamba Ramaphosa alipewa nafasi kubwa ya kushinda, lakini Mkhize alipata kura nyingi zaidi kuliko ilivyotarajiwa baada ya kutwaa nyadhifa muhimu kwa viongozi wengine wenye nguvu katika mikataba iliyofikiwa kabla ya wajumbe kupiga kura kwenye mkutano huo.

Kura za maoni zinaonyesha kuwa kura yake imepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na kuenea kwa rushwa serikalini, ukosefu mkubwa wa ajira na huduma duni za umma, ikiwa ni pamoja na kukatika kwa umeme kila mara.

***BBC***

# Waziri azuia mkandarasi kutia saini mkataba mpya

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amezuia kampuni ya ETDco kutia saini mkataba wa utekelezaji wa usambazaji wa umeme maeneo ya pembezoni mwa miji kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) baada ya kuonekana kusuasua kwenye kukamilisha mradi wa kwanza iliyopewa mkoani Mbeya miaka kadhaa iliyopita.



Akizungumza jana wakati wa hafla ya utiaji saini wa mkataba wa utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme maeneo ya pembezoni mwa miji, waziri huyo alisema makandarasi wamepata jeuri kwa sababu wanajua hakuna watakachofanywa hata wakichelewa kukamilisha miradi.

Alisema kampuni ya ETDco wanalalamikiwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwa kuchelewa kukamilisha kazi waliyopewa ambayo hadi sasa wamefikia asilimia 28 na kwa mujibu wa ratiba, walipaswa wawe wamefikia asilimia 85, hivyo hawatapatiwa mkataba mwingine hadi wakamilishe kazi ya awali.

"Wanajua wakichelewa hata ukiwaambia ondoka mpaka upate mwingine itachukua muda, unakuta kapeleka vitu lakini anasuasua, ukisema upeleke mwingine gharama zitakuwa kubwa zaidi, imekuwa ni kubembelezana, serikali hatuwezi kuvumilia hilo.

"Sasa hivi mnataka kazi ya mikoa miwili ya Sh. bilioni 18 wakati kazi ya Mbeya ni miaka kadhaa sasa hamjakamilisha na kandarasi nyingine mtasaini, lakini kama kasi ndio hii inawezekana kabisa hizi zikawa kazi zenu za mwisho hapa Tanzania na ninaomba ujumbe huu uwafikie makandarasi wote wa REA," alionya.

Waandishi wa habari walipotaka kujua kwanini walishindwa kutekeleza kazi kwa mujibu wa mkataba, viongozi wa kampuni hiyo hawakutoa ushirikiano.

January alisema kuanzia sasa watabadilisha masharti katika utekelezaji wa miradi ya REA, akibainisha kwamba kama mkandarasi yeyote yuko nyuma ya muda wa kukamilisha kazi aliyopewa, hatapatiwa mkataba mwingine.

Sharti la pili, alisema kama mkandarasi yeyote alipewa kazi na katika utekelezaji wake akawasumbua na kuchelewa kukamilisha mradi ndani ya muda wa makubaliano, hatapatiwa tena mkataba mwingine.

"Afadhali tubaki na makandarasi watatu, wanne wanaotimiza wajibu wao kuliko kuwa na 50 ambao wanaingia kujaribisha, tunahitajika kuzingatia historia na uwezo wa mkandarasi kabla hajapata kazi nyingine, sisi tuko tayari kuwa na mkandarasi mmoja mkubwa huko duniani aje afanye hii kazi na nyie mbaki bila kazi," alisema.

Alisisitiza kwamba msingi wao ni kuona kazi inafanyika na umeme ufike vijijini na siyo kuwajengea watu uwezo, huku akiwataka makandarasi hao kukaa pembeni kama hawawezi kazi.

January alisema wizara itaelekeza nguvu nyingi katika ufuatiliaji wa miradi hiyo kutokana na kuna kusuasua kwa utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme vijijini licha ya kutumia fedha nyingi za mashirika ya maendeleo kutafuta makandarasi ili kupeleka umeme maeneo yenye uhitaji.

Alisema katika sehemu nyingi wanaona makandarasi wamechimba mashimo, wamesimika nguzo, wengine wameweka nyaya na kuondoka huku ikiwachukua muda mrefu kukamilisha miradi hiyo.

Alisema kuanzia sasa serikali itaajiri waratibu 130 wa miradi ya REA katika kila mkoa na wilaya ambao watawasimamia makandarasi na kutoa taarifa serikalini kuhusu maendeleo ya miradi.

"Kama mkandarasi amechelewa kuleta waya au nguzo, tutajua siku hiyo hiyo, na tutaweka mfumo wa mawasiliano kati ya waratibu hao na sisi ili ichukue siku moja kujua nini kinaendelea katika mikoa miradi inapofanyika.

"Sasa hivi mambo yanaenda huko unakuja kuambiwa baadaye wakati yameshachelewa, hilo hatutaki litokee, na baada ya Krismasi kutakuwa na usaili na mwakani tutatangaza kila mtu na wilaya yake," alisema.Ilibainishwa kwamba mradi huo wa usambazaji wa umeme awamu ya tatu utanufaisha maeneo 416 kwenye mikoa minane ambayo ni Geita, Kagera, Kigoma, Mbeya, Mtwara, Singida, Tabora na Tanga.

Mkandarasi kutoka Kampuni ya O.K Electrical, Mrisho Masud, aliyezungumza kwa niaba ya makandarasi wengine, aliahidi wataongeza bidii na nguvu katika kutekeleza miradi hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa REA, Hassan Saidy, alisema miradi hiyo ina lengo maalum kwa wananchi, hivyo aliwasisitiza makandarasi waliotia saini mkataba, kufanya kazi kwa karibu na viongozi wa maeneo husika.

"Hakikisheni mnafanya kazi kwa kuzingatia viwango na ubora unaokubalika, kwa viwango vilevile vya njia za umeme za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), itawasaidia kupunguza kuchelewesha mradi, mkitumia vifaa visivyokuwa na ubora, tukivibaini mtavibadili kwa gharama zenu," alisisitiza Saidy.

# Nape alikabidhi Jeshi la Polisi vifaa vya TEHAMA

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, ameziagiza Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS) na Jeshi la Polisi kutumia vifaa vya kuendesha mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi makosa ya mtandao bila urasimu ili washtakiwa wapate haki kwa muda sahihi.

Amezitaka kuhakikisha vifaa hivyo vinaelekezwa katika matumizi ya moduli ya makosa ya mtandaoni na kuwezesha mfumo huo kufanya kazi kwa ufanisi ili kuwapo na takwimu za ushughulikiwaji wa matukio hayo zinazoshabihiana.

Wanaosimamia sheria za makosa ya mtandao wawezeshwe kiteknolojia ili wawe na uwezo wa kuzisimamia sheria zitekelezewe kwa urahisi na anga la mtandao liendelee kuwa salama.

Waziri Nape aliyasema hayo wakati akikabidhi vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa Jeshi la Polisi na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa ajili ya moduli ya makosa ya mtandao jana jijini Dar es Salaam katika kuboresha huduma hiyo kwa jamii.

"Dunia imeenda mtandaoni, ongezeko la watu kwenda huko ni kubwa mno, katika idadi yetu ya watu milioni 61, karibia milioni 40 wanafanya miamala kupitia mitandao, kwa hiyo ni asilimia zaidi ya 50, nia ya serikali ni kuhakikisha huko kupo salama," alisema Nape.

Alisema wizara hiyo imeendelea kushirikiana na wadau kudhibiti matumizi mabaya ya huduma za mawasiliano nchini kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo utungwaji wa sheria kama makosa ya mtandao ya mwaka 2015 na sheria ya miamala ya kielektroniki ya 2015.

"Lakini hatua zingine ni pamoja na uundaji wa mkakati wa taifa wa usalama wa mtandao, uanzishwaji wa vitengo maalum vya kusimamia usalama wa mtandao na uundwaji wa kamati ya kitaifa ya kusimamia utatuzi wa matumizi mabaya ya huduma za bidhaa za mawasiliano," alisema.

Pamoja na juhudi kubwa zinazofanya na kamati ya kitaifa ya kusimamia matumizi mazuri ya huduma na bidhaa za mawasiliano, alisema bado kumekuwa na ongezeko la matumizi mabaya ya simu za mkononi hususani wizi wa fedha kupitia mitandao na kutaka hatua za ziada zichukuliwe.

"Wizara yangu ipo tayari kuendelea kuongeza nguvu katika kuleta vifaa vya kisasa vitakavyokidhi mahitaji kwa sababu ni agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, tuwezeshe upatikanaji wa haki kwa urahisi na kwa wakati kupitia TEHAMA na sisi tupo tayari kwa ajili hiyo," alisema.

Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Joseph Pande, alisema kukamilika kwa mfumo huo kutatatua changamoto ya kutokuwapo na takwimu za kina zinazohusu makosa ya mtandao kwa taasisi zinazoshughulikia makosa hayo kuharakisha upelelezi wa makosa hayo na kurahisisha upatikanaji wa haki kwa watuhumiwa wa makosa hayo.

Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini IGP, Camillus Wambura, alisema vifaa hivyo vitakwenda kufanya kazi iliyotarajiwa ikiwamo kusimamia maadili, nidhamu na weledi mitandaoni.

Jumla ya kompyuta 170, mpakato 10 na modem za TTCL 170 ziligawiwa kwa Jeshi la Polisi, huku Ofisi ya Mashtaka ya Taifa ikikabidhiwa kompyuta mpakato 180, 'scanner' 45 na 'modem' za TTCL 30 vitavyotumika kuboresha huduma hiyo.


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANDREA YAKOBO KIFARU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 219 CZR – TOYOTA VITZ.** Chassis namba **SCP100286149. Engine namba 1SZ2020080.** Yeyote atakayeiona atoe **taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: DAR/URA/RB/472986/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FESTO RICHARD SWAI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 705 CYP- TVS STAR.** Chassis namba **MD625AF46M1D02883.** Engine namba **DF4DM1802290.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CHU/RB/463840/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SANLG WORD WIDE INVESTMENT LTD** inatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 617 DLT.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **TAR/RB/147/2022.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**ASYA S. SLEIMAN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index number **S.1918-0503** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **FALAAH MUSLIM** Secondary School February, 2010. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MUH/RB/307/2021.**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 142 OF 2022**
In the Matter of the Estate of the Late:
**NEEMA BONIFACE HATIBU**
**BY 1.FRIDA JOSEPHATI**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the **23TH JANUARY.........2023**
Dated at **MOROGO** this 16ST day of **DECEMBER.........2022**

RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P.O. Box 660, Morogoro

BURUDANI

# MAMA HAJUI ZUCHU, DIAMOND NI WAPENZI



GWIJI wa muziki wa Taarab nchini, Khadija Kopa, ameweka wazi kwamba hajui kama binti yake Zuchu yuko kwenye uhusiano wa kimapenzi na Diamond Platnumz.

Kopa pia amebainisha kuwa hajui kama wawili hao ambao wanadaiwa kuchumbiana wanapanga kufunga pingu za maisha.

"Sijui, Mungu ndiye anajua. Hiyo ni mipango ya Mungu. Mungu ndiye anajua kama nitapata mkwe au la," alisema katika mahojiano na wanahabari.

"Mimi sijui uhusiano wake."

Wakati alipohojiwa kuhusu video za kimapenzi za binti yake na Diamond ambazo zimekuwa zikivuma kwenye mitandao ya kijamii siku za hivi majuzi, alidai kuwa hana habari na hajapata nafasi ya kuzitazama.

Hata hivyo, aliweka wazi kuwa ikitokea Zuchu aolewe na bosi wake, hana tatizo na wao kuwa pamoja kama mke na mume.

"Mimi sijali nini wala nini, yeyote atakayebeba mizigo kama amempenda atamuoa tu," alisema.

Pia alibainisha kuwa yuko sawa na aina ya muziki ambao binti yake anafanya akiwa katika Lebo ya Diamond, WCB.

Tetesi za mahusiano kati ya Diamond na msanii wake, Zuchu zimefufuliwa tena katika siku za hivi majuzi kufuatia matendo yao pamoja ambayo yamekuwa yakishirikishwa kwenye mitandao mbalimbali.

Kumekuwa na video na picha kadhaa ambazo zimeibua maswali chungu nzima kuhusu uhusiano wao halisi.

## WASANII WANG'ARA TUZO ZA FILAMU



TUZO za filamu mwaka 2022, zimefikia ukingoni ambapo kwa upande wa wasanii wa kiume bora, Nkwabi Ng'wanamala maarufu kwa jina la Mzee Kikala wa tamthiliya ya Kombolela ameibuka mshindi.

Sambamba na hilo kwa upande wa msanii bora wa kike, Tunu Mbegu, wa filamu ya 'Still Ok to Date' ameibuka kidedea.

Tuzo hizo ambazo hii ni mara yake ya pili kutolewa tangu kuanzishwa kwake, zilitolewa usiku wa juzi jijini Arusha ambapo wasanii 169 walikuwa wakichuana na filamu 39 zilikuwa zikishindanishwa.

Aidha, upande wa muongozaji bora, Leah Mwendamseke maarufu 'Lamata' aliondoka na ushindi.

Lamata ambaye ni muongozaji wa filamu ya Jua Kali, alikuwa akishindanishwa na waongozaji wengine akiwamo Neema Ndepanya, Honeymoon Aljabri na Florence Mkinga na Christina Pande.

Aidha, msanii Jacob Steven'JB' alitangazwa kuwa mshindi katika kipengele cha chaguo la watazamaji kipengele kilichukuwa kinashindaniwa na wasanii 19.

## DIMPOZ AELEZEA MASAHIBU YAKE




NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, Omary Nyembo 'Ommy Dimpoz', amefunguka alivyougua koo miaka michache iliyopita hali iliyosababisha kufanyiwa upasuaji mara mbili.

"Kama mnavyokumbuka nilipata changamoto ya kiafya. Sikuwa na kansa bali nilikuwa nashindwa kula chakula. Kilikuwa hakishuki.

"Nilifuatilia vipimo hapa nyumbani lakini tatizo halikupatiwa ufumbuzi. Ilihitaji vipimo vya ziada. Ilihitajika kwenda nje ya nchi. Vipimo vikasema kwamba nilikula sumu.

"Hiyo hali ilinisumbua sana. Nilikuwa najiuliza nilikula wapi sumu? Niliamua niendelee na matibabu. Changamoto ilikuwa inakuja wakati wa upasuaji ilikuwa ni kupoteza sauti.

"Hiyo hali ilinifanya niwe kimya kufanya muziki na pia sitaki presha ya muziki." Aliandika Dimpoz kwenye ukurasa wake wa Instagram.

## HABARI MICHEZO

# JESHI KUIBUA VIPAJI KUSAIDIA TAIFA

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

WIZARA ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), wanakusudia kushirikiana na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo katika kuibua vipaji vya michezo mbalimbali vilivyopo jeshini ili kuweza kusaidie kupeperusha vema Bendera ya nchi katika mashindano ya kimataifa, imeelezwa.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa(JKT), Innocent Bashungwa, wakati akipokea vikombe na kuwapongeza wanamichezo wa Shirika la Mzinga waliopata ushindi wa jumla wa michezo yote ya Shirikisho la Michezo ya Mashirika ya Umma Tanzania(SHIMMUTA).

Waziri Bashungwa, alisema maamuzi ya kushirikiana na Wizara ya Michezo inatokana na vipaji vingi vya michezo mbalimbali kutoka katika Majeshi ya Ulinzi, jambo ambalo aliweka wazi kuwa ni bora vikaboreshwa ili kuweza kulisaidia taifa kufanya vizuri katika michezo ya kimataifa.

"Wakati nikiwa Waziri wa Michezo, nilianzisha mpango huo na nakumbuka niliwaunganisha na wanamichezo kutoka timu ya Jeshi ya Ngome na Baraza la Michezo (BMT), sikujua kama nitakuja wizara hii, sasa nitashirikiana na Wizara ya Michezo ili tuendeleze vipaji ndani ya jeshi viweze kuliletea tija Taifa" alisema Waziri Bashungwa.

Naye Meneja Mkuu wa Shirika la Mzinga, Brigedia Jenerali Hamis Seif, alisema wanamichezo hao wamefanya kazi kubwa ya kuitangaza vema Wizara ya Ulinzi kwa kunyakuwa ushindi katika michezo mbalimbali ya SHIMIWI.

Brigedia Jenerali Seif, alisema kutokana na mafanikio hayo, shirika hilo limeona ni vema kuwatambua wanamichezo hao kutokana na mchango wao kwa kuwazawadia ili kuleta chachu katika mashindano yajayo waweze kufanya vizuri zaidi.

Mwenyekiti wa Michezo wa Shirika la Mzinga, David Msabi, alisema wamefanikiwa kupata jumla ya vikombe 10 katika mashindano hayo na meneja wa Mzinga aliona si vema ushindi huo ukaishia hapo na kuamua kufikisha kwa Waziri wa wizara hiyo ili uweze kutambulika.




Meneja Mkuu wa Shirika la Mzinga, Brigedia Jenerali Hamis Seif, akibeba Kombe la Ushindi wa Jumla la Michezo ya SHIMMUTA, kumkabidhi Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Innocent Bashungwa (kulia). Aliyevaa kofia ni Mwenyekiti wa Michezo Mzinga, David Msabi. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

## Yanga, Coastal mtihani mzito

INATOKA UK. 32

Frank Msese, alisema wamefanya maandalizi baada ya kupoteza dhidi ya Ihefu FC na wameyafanyia kazi mapungufu yao kuelekea mchezo wao dhidi ya Mtibwa Sugar.

"Haitakuwa mechi rahisi kwa sababu Mtibwa Sugar ni timu yenye wachezaji mchanganyiko wa damu changa na nyota wazoefu, lakini tumejipanga kwa ajili ya kutafuta pointi tatu katika mchezo wa kesho (leo)," alisema Msese.

Kocha Msaidizi wa Mtibwa Sugar, Awadhi Juma, alisema wamefanya maandalizi mazuri na kikosi chao kipo tayari kwa ajili ya kutafuta pointi muhimu katika mchezo wao wa leo dhidi ya Ruvu Shooting.

"Tumeangalia baadhi ya michezo yao kwa kufanyia kazi ubora wao na madhaifu yao katika kuhakikisha tunapata pointi muhimu katika mchezo wetu, tutacheza kwa nidhamu ya hali ya juu kwa kuwaheshimu Ruvu Shooting," alisema kocha huyo.

## Simba: Vipigo zaidi vinakuja

INATOKA UK. 32

rahisi, haijalishi matokeo, tulijipanga vizuri kucheza mechi ngumu kwa sababu Geita Gold ni timu nzuri na mwalimu wake Minziro (Fred Felix) ni kocha mzuri na mshindani tangu anacheza soka, kwa hiyo hata anavyofundisha soka anafundisha lile la kushindana. Soka ni mchezo wa nafasi, mkipata nafasi na kuzitumia vema basi inakuwa siku nzuri kwenu, Geita Gold wamefanya makosa mengi tumewaadhibu.

"Nawashukuru wachezaji wangu, wanaonekana kadri muda unavyozidi kwenda wanazidi kubadilika, inanipa moyo wa kupambana kutaka kufanya vizuri na kutaka kufunga magoli unaonekana ni mkubwa sana," alisema Mgunda.

Mchezaji Kibu Denis ambaye juzi alifunga bao lake la kwanza msimu huu, alisema anaamini atakuwa na mwendelezo mzuri kwenye ufungaji baada ya kufungua akaunti.

"Ulikuwa mchezo mgumu, mechi haikuwa rahisi, binafsi nimetokea benchi na kufunga bao, nishukuru wachezaji wenzangu, benchi la ufundi, wanachama na mashabiki wa Simba ni kweli nilipofunga bao nilifurahi sana kwa sababu ndiyo bao langu la kwanza msimu huu, ukiangalia msimu uliopita nilifunga mabao manane, mashabiki walitegemea makubwa msimu huu kutoka kwangu, lakini hawakuyaona mzunguko wa kwanza. Kila kitu kina muda wake, nimeanza kwa kufunga bao leo, naamini huu ni mwanzo mzuri kuelekea mechi zinazofuata," alisema.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema kipigo hicho ni ujumbe tosha kwa timu zingine zote, huku akitoa onyo kuwa vipigo vinene kama hivyo vitaendelea.

"Hii ni kutoa ujumbe kuwa sisi tuna timu bora sana, kutoa kipigo cha mabao 5-0 tena timu ikiwa ugenini haijawahi kutokea kwenye Ligi Kuu msimu huu na sisi ndiyo tuna rekodi ya kufunga mabao mengi kwenye ligi, tulishinda pia kwa idadi hiyo dhidi ya Mtibwa Sugar, kuna watu walimbeza Clatous Chama kuelekea kwenye mechi hii, lakini amewafunga midomo, amefunga bao zuri sana, unajua wakati Argentina inajivunia fundi wa mpira, Messi (Lionel), sisi Simba tunajivunia mtu anaitwa Chama," alisema.

## Mbeya Kwanza yaitaka Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbeya Kwanza ambayo iliteremka daraja msimu uliopita, inaonekana kupambana kutaka kurejea tena Ligi Kuu, baada ya juzi kuishindilia Pan African mabao 3-1, katika mechi ya Ligi ya Championship iliyopigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Ushindi huo umeifanya timu hiyo kukwea hadi nafasi ya nne ya msimamo wa ligi hiyo ikiwa imefikisha pointi 24 baada ya kucheza mechi 13.

Timu mbili za juu kwenye ligi hiyo zitapanda moja kwa moja Ligi Kuu, huku zitakazomaliza nafasi ya tatu na ya nne zikielekea kucheza mechi za mchujo.

Ligi hiyo bado inaongozwa na JKT Tanzania licha ya Jumamosi iliyopita kuchapwa mabao 2-1 dhidi ya Mashujaa, mechi ikichezwa Uwanja wa Lake Tanganyika, mjini Kigoma.

Pamoja na kupoteza , maafande hao bado wanaendelea kuongoza ligi wakiwa na pointi 31 kwa michezo 13 ambayo wamecheza mpaka sasa, wakishinda 10, sare moja na kupoteza mbili. JKT Tanzania ilicheza mechi nane bila kupoteza, ikishinda michezo saba na kutoa sare moja.

## Pluijm kusajili majembe ma3

**Na Hadija Mngwai**

KATIKA kuhakikisha anakiboresha kikosi chake ipasavyo, Kocha wa Singida Big Stars, Hans Pluijm, amesema anaitaji majembe matatu kwa ajili ya kuziba mapengo yaliyojitokeza katika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Bara.

Dirisha dogo la usajili kwa timu za Ligi Kuu Bara, Ligi ya Championship na First League, limefunguliwa Desemba 16 na linatarajiwa kufungwa Januari 15, mwakani.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Singida Big Star, Hussein Massanza amesema kuwa, wanatarajia kuongeza wachezaji katika nafasi tatu kulingana na matakwa ya kocha Hans ili kuimalisha kikosi chake.

"Dirisha dogo la usajili limefunguliwa, hivyo tunajipanga kufanya maboresho katika kikosi chetu kadri benchi la ufundi litakavyotaka kuboreshwa katika baadhi ya safu.

"Maeneo ambayo tunahitaji kuboresha ni ushambuliaji, ulinzi na winga, tutafanya usajili wa kimkakati kuhakikisha tuna boresha kikosi chetu vizuri.

"Tutaziba mapengo yote yajitokeza katika mzunguko wa kwanza ambayo mwalimu Hans Pluijm, ameweza kuona mapungufu yaliyojitokeza na dirisha limefunguliwa, hivyo ni wakati sahihi," alisema Massanza.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DE JONG HUYO MAN
KIUNGO wa Kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong, mwenye umri wa miaka 25, ameripotiwa kumwambia Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag, kuwa atafurahi kuungana naye Old Trafford. ***(Mirror)***

### WAN-BISSAKA NA WEST HAM
KLABU ya West Ham United ina nia ya kumsajili beki wa kulia wa Manchester United, Aaron Wan-Bissaka mwenye umri wa miaka 24 kwa mkopo katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Manchester Evening News)***

### AMRABAT AITAKA LIVERPOOL
KIUNGO wa kati wa Fiorentina na Morocco, Sofyan Amrabat, mwenye umri wa miaka 26, angependelea kujiunga na Liverpool licha ya Tottenham kuonyesha nia ya kumtaka. ***(Foot Mercato kupitia Inside Futbol)***

### LIVERPOOL KWA AMRABAT
MKATABA wa kumnunua Sofyan Amrabat katika dirisha la Januari ndio matokeo yanayotarajiwa zaidi na Liverpool, kwani uhamisho wa kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19 na kiungo wa kati wa Benfica na Argentina, Enzo Fernandez, 21, bado unafanyiwa kazi. ***(Teamtalk)***

### CAICEDO AWINDWA CHELSEA
CHELSEA na Liverpool zina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Brighton mwenye umri wa miaka 21 raia wa Ecuador, Moises Caicedo. ***(Sky Sports)***

### MOUKOKO ATAKIWA BARCA
BARCELONA wana nia ya kumsajili mshambuliaji wa Ujerumani, Youssoufa Moukoko, mwenye umri wa miaka 18, kutoka Borussia Dortmund, lakini wanakataa kulipa ada kwa mchezaji anayepatikana bure Juni. ***(Football Transfers)***

### GVARDIOL ANUKIA CHELSEA
CHELSEA wanatumaini kuzishinda Real Madrid na Manchester City katika mbio za kumsajili mlinzi wa RB Leipzig na Croatia, Josko Gvardiol, mwenye umri wa miaka 20, kwa kuhama kwa pauni milioni 45 Januari. ***(Sun)***

### THURMAN ATAKIWA UNITED
KLABU ya Manchester United imeripotiwa kutaka kumsajili mshambuliaji wa Borussia Monchengladbach na Ufaransa, Marcus Thuram, mwenye umri wa miaka 25 wakati dirisha la uhamisho la Januari litakapofunguliwa. ***(Sport Bild via Sun)***

### SIMEONE KUIMARISHA ULINZI
KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone, anapania kuimarisha safu yake ya ulinzi Januari na anafikiria kumnunua beki wa Leicester City na Uturuki Caglar Soyuncu, 26. ***(Team Talk)***

### RONALDO MAJANGA ARSENAL
MLINZI wa zamani wa Arsenal, Nigel Winterburn, amesema kumnunua mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo, mwenye umri wa miaka 37, kutakuwa "janga kubwa" kwa 'Washikabunduki' hao. ***(Metro)***

### UNITED YAKARIBIA KUUZWA
MMILIKI mwenza wa Manchester United, Avram Glazer, amefanya mazungumzo na wawekezaji watarajiwa wakati wa safari yake ya kuelekea Doha kwa ajili ya Kombe la Dunia, wakiwamo kutoka Saudi Arabia na Qatar. ***(Athletics)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI AWEKA KANDO KUSTAAFU ARGENTINA

●●● Ninafurahia kuwa katika timu ya taifa na ninataka kuendelea kwa kushuhudia michezo michache zaidi kama...

**DOHA, Qatar**

LIONEL Messi amesema hatastaafu soka la kimataifa baada ya kuiongoza Argentina kunyakua Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 36.

Mshambulizi huyo wa Paris St-Germain aliulizwa kuhusu mustakabali wake na Kituo cha Televisheni cha Argentina, TyC Sports, baada ya taifa hilo la Amerika Kusini kuilaza Ufaransa kwa mikwaju ya penalti 4-2 kutokana na sare ya mabao 3-3.

Messi ambaye atafikisha miaka 36 mwakani, alijibu kwa kusema bado anaamini ana mengi ya kulipatia taifa lake.

"Ninapenda soka, ndivyo ninavyofanya," alisema.

"Ninafurahia kuwa katika timu ya taifa na ninataka kuendelea kwa kushuhudia michezo michache zaidi kama bingwa wa dunia.

"Aliongeza: "Ni wazi nilitaka kumaliza kazi yangu na hii na siwezi kuuliza chochote zaidi.

"Messi, akicheza kombe lake la tano la dunia, alifunga mara mbili kwenye fainali na pia alifunga penalti kwenye mikwaju ya penalti.

Alishinda Mpira wa Dhahabu wa mashindano hayo - uliotunukiwa mchezaji bora wa mashindano, lakini akifunga mabao saba.

Messi atakuwa na umri wa miaka 39, wakati wa Kombe la Dunia lijalo na alikuwa amedokeza hapo awali kwamba michuano hii ya Qatar ingekuwa ya mwisho kwake.

Hata hivyo, Kocha Lionel Scaloni, amesema anamtaka Messi katika kikosi chake kwa ajili ya michuano ya 2026, itakayofanyika kwa ushirikiano wa Marekani, Canada na Mexico.

"Kwanza kabisa, tunahitaji kumwekea nafasi katika kikosi chake cha Kombe la Dunia 2026," alisema.

"Ikiwa anataka kuendelea kucheza, atakuwa nasi.

"Nafikiri ana haki zaidi ya kuamua kama anataka kuendelea kuichezea Argentina au la, au anachotaka kufanya katika maisha yake ya soka.

"Ni furaha kubwa kwetu kumfundisha yeye na wachezaji wenzake.

"Kila kitu anachokutana nacho hadi wachezaji wenzake ni kitu kisicho na kifani, kitu ambacho sijawahi kuona. Mchezaji, mtu anayetoa sana kwa wenzake."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,059,8

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 21,22 NA 23 DISEMBA 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 21/12/22 | 22:00 | MSK Deinze vs Zulte Waregem | 2.67 | 3.41 | 2.39 |
| 02. 21/12/22 | 23:00 | UD Logrones vs Albacete Balompie | 2.93 | 3.23 | 2.36 |
| 03. 22/12/22 | 17:00 | Jamshedpur vs FC Goa | 2.52 | 3.25 | 2.52 |
| 04. 22/12/22 | 18:00 | OFI Crete vs Atromitos | 2.47 | 3.35 | 2.75 |
| 05. 22/12/22 | 20:00 | Aris Limassol vs Apoel Nicosia | 2.81 | 3.21 | 2.49 |
| 06. 22/12/22 | 20:00 | Omonia Nicosia vs Apollon Limassol | 2.42 | 3.15 | 2.95 |
| 07. 22/12/22 | 21:00 | CD Linares vs Racing Santander | 2.98 | 3.23 | 2.33 |
| 08. 22/12/22 | 21:00 | CD Eldense vs Burgos | 2.63 | 3.18 | 2.63 |
| 09. 22/12/22 | 23:00 | Gimnastic Tarragona vs Malaga | 3.09 | 3.18 | 2.29 |
| 10. 22/12/22 | 23:00 | Real Oviedo vs Granada | 2.83 | 2.98 | 2.59 |
| 11. 22/12/22 | 23:15 | Moreirense vs FC Arouca | 2.41 | 3.15 | 2.71 |
| 12. 23/12/22 | 11:45 | Brisbane Roar vs Western Sydney | 2.35 | 3.32 | 2.87 |
| 13. 23/12/22 | 14:30 | Perth Glory vs Wellington Phoenix | 2.78 | 3.38 | 2.38 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# PELE AIPIGIA SALUTI ARGENTINA, AMHURUMIA MBAPPE



**SAO PAULO, Brazil**

GWIJI wa Brazil, Pele alituma pongezi kwa Argentina baada ya ushindi wao wa ajabu wa fainali ya Kombe la Dunia, akielezea mafanikio ya Lionel Messi kama "wakati wake aliostahili".

Huku akionyesha huruma kwa Kylian Mbappe, ambaye aiibuka kuwa mfungaji bora wa michuano hiyo kwa mabao yake nane.

Pele, ambaye amelazwa hospitalini hivi karibuni, amekuwa akifuatilia matukio ya Kombe la Dunia nchini Qatar na kusema ushindi huo wa Argentina umemfurahisha sana marehemu Diego Maradona huko aliko.

Kipindi kikubwa kwa Messi mwenye umri wa miaka 35, kinamaanisha kwamba hatimaye amepata ushindi wa Kombe la Dunia kwa jina lake, akilingana na Maradona ambaye ndiye aliyeongoza Argentina kutwaa ubingwa huo mwaka 1986 nchini Mexico.

Maradona alifariki dunia Novemba 2020 akiwa na umri wa miaka 60.

"Hongera Argentina! Hakika Diego anatabasamu sasa," aliandika Pele kwenye Instagram.

Pia Pele mwenye umri wa miaka 82, alimhurumia Mbappe, ambaye alimaliza kwa timu iliyopoteza licha ya kufunga penalti mbili na kumaliza kwa hat-trick ya pili katika historia ya michuano hiyo, baada ya Geoff Hurst kuifungia England mwaka 1966 dhidi ya Ujerumani Magharibi.

Argentina ilinyanyua taji hilo baada ya sare ya 3-3 Jumapili, na kushinda kwa mikwaju ya penalti 4-2 baada ya Kingsley Coman na Aurelien Tchouameni kukosa penalti zao.

Mshindi mara tatu wa Kombe la Dunia Pele, alisifu kazi ya Mbappe ya kutinga wavuni mara nne, ikiwa ni pamoja na mkwaju wa penalti, na pia alipongeza Morocco, iliyomaliza nafasi ya nne baada ya kuwa timu ya kwanza kutoka Afrika kutinga nusu fainali.

"Leo, soka inaendelea kusimulia hadithi yake, kama kawaida, kwa njia ya kusisimua," alisema Pele.

"Messi ameshinda Kombe lake la kwanza la Dunia, kama historia yake inavyostahili.

"Rafiki yangu mpendwa, Mbappe, akifunga mabao manne kwenye fainali. Ilikuwa ni zawadi gani kutazama tamasha hili la mustakabali wa mchezo wetu.

"Na nisingeweza kushindwa kuipongeza Morocco kwa kampeni ya ajabu. Ni vyema kuona Afrika iking'ara."

# Deschamps kuamua mustakabali Ufaransa

**DOHA, Qatar**

DIDIER Deschamps atafanya uamuzi kuhusu mustakabali wake wa kuendelea kuinoa Ufaransa katika mwaka mpya baada ya kushuhudia 'Les Bleus' hao wakipoteza kwa mikwaju ya penalti dhidi ya Argentina katika fainali ya Kombe la Dunia, Jumapili.

Hat-trick ya Kylian Mbappe - ya pili pekee kufungwa kwenye fainali ya Kombe la Dunia kwa wanaume - iliifanya Ufaransa kutoka nyuma mara mbili katika sare ya 3-3 ya kusisimua baada ya muda wa ziada kwenye Uwanja wa Lusail.

Hata hivyo, ni mchezaji mwenzake na Mbappe wa Paris Saint-Germain, Lionel Messi ambaye alinyakua taji hilo maarufu, huku Kingsley Coman na Aurelien Tchouameni wakikosa mikwaju yao ya penalti. Kipigo hicho kinaweza kufufua uvumi kuhusu mustakabali wa Deschamps, huku nguli wa Ufaransa, Zinedine Zidane, akitajwa kwa muda mrefu kama mrithi anayetarajiwa.

Hata hivyo, Deschamps atachukua muda wake kupima iwapo ataongeza muda wa kukaa kwa miaka 10 na mabingwa hao mara mbili wa dunia.

"Wewe si wa kwanza kuuliza. Hata kama tungeshinda, nisingeweza kujibu hilo usiku wa leo," alisema Deschamps baada ya kuulizwa na waandishi wa habari kuhusu mustakabali wake.

"Kwa kweli, nina huzuni sana kwa wachezaji na wafanyakazi, lakini nitakuwa na mkutano na rais wa Shirikisho la Soka la Ufaransa mwanzoni mwa mwaka ujao na ndipo mtajua."

Deschamps aliweka wazi kusikitishwa kwake na uchezeshaji wa mwamuzi Szymon Marciniak baada ya mchezo, ingawa pia alitoa pongezi zake kwa Argentina.

"Nahitaji kuwa makini ninachosema. Mliona vizuri kama nilivyoona. Inaweza kuwa mbaya zaidi, ingekuwa bora," alisema.

"Kuna baadhi ya maamuzi yalizua mjadala, lakini ndivyo ilivyo katika kila mchezo, nilisema kabla ya mchezo kuwa Argentina walikuwa na bahati, si kwamba walisaidiwa na maamuzi.

"Sitaki kuwanyang'anya chochote, wanastahili ubingwa kabisa. Sio kwa sababu ya maamuzi waliibuka washindi na nilizungumza tu na mwamuzi.

"Sitaki kuingia katika kile kilichosemwa, nataka tu kuwapongeza Argentina."

Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, ambaye alihudhuria fainali hiyo alionekana akizungumza na Deschamps baada ya mchezo huo na aliiambia RMC Sport kuwa amemtia moyo kocha huyo mwenye umri wa miaka 54, kubakia kwenye nafasi yake.

"Bila shaka, nilimwomba Didier Deschamps aendelee, nataka aendelee! Nilimwambia alipaswa kutulia," alisema Macron.

344,733/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/12/22 | 18:00 | Everton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.31 | 3.25 | 3.05 |
| 02. 26/12/22 | 18:00 | Bristol City vs West Bromwich Albion | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 03. 26/12/22 | 18:00 | Rotherham United vs Stoke City | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 04. 26/12/22 | 18:00 | Burton Albion vs Lincoln City | 2.37 | 3.30 | 2.90 |
| 05. 26/12/22 | 18:00 | Cambridge United vs Shrewsbury Town | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 06. 26/12/22 | 18:00 | Charlton Athletic vs Peterborough United | 2.70 | 3.30 | 2.55 |
| 07. 26/12/22 | 18:00 | Exeter City vs Portsmouth FC | 2.65 | 3.35 | 2.55 |
| 08. 26/12/22 | 19:00 | FC Annecy vs AS Saint-Etienne | 2.90 | 3.25 | 2.37 |
| 09. 26/12/22 | 20:00 | Goztepe Izmir vs BB Bodrumspor | 2.50 | 3.35 | 2.65 |
| 10. 26/12/22 | 20:15 | Cardiff City vs Queens Park Rangers | 2.48 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 26/12/22 | 22:45 | Royal Charleroi SC vs RSC Anderlecht | 2.80 | 3.45 | 2.38 |
| 12. 26/12/22 | 22:45 | Luton Town vs Norwich City | 2.75 | 3.30 | 2.50 |
| 13. 26/12/22 | 23:00 | Valenciennes FC vs Amiens SC | 2.46 | 3.20 | 2.85 |
| 14. 26/12/22 | 23:00 | Pau FC vs Paris FC | 2.95 | 3.20 | 2.38 |
| 15. 26/12/22 | 23:00 | Quevilly-Rouen Metropole vs Grenoble Foot | 2.46 | 3.05 | 2.95 |
| 16. 26/12/22 | 23:00 | SC Bastia vs SM Caen | 3.05 | 3.10 | 2.38 |
| 17. 26/12/22 | 23:00 | Nimes Olympique vs EA Guingamp | 2.90 | 3.25 | 2.40 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 20/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2563 | Kasimpasa vs Umraniyespor | 1.80 | 3.65 | 3.70 |
| 13:00 | 3534 | Cambodia vs Philippines | 3.64 | 3.69 | 1.81 |
| 14:00 | 1132 | Churchill Brothers vs Tiddim Road Athlectic Club | 2.04 | 3.21 | 3.36 |
| 15:00 | 1681 | Sivasspor vs Kasimpasa Erokspor | 1.44 | 4.36 | 5.62 |
| 15:45 | 5819 | Enppi Club vs Ismaily SC | 2.83 | 2.63 | 2.93 |
| 16:00 | 4144 | Ruvu Shooting vs Mtibwa Sugar | 2.49 | 2.84 | 2.89 |
| 16:00 | 5328 | Fasil Kenema vs Wolkite City FC | 1.59 | 3.55 | 5.25 |
| 16:15 | 3625 | Persija Jakarta vs Dewa United | 1.62 | 3.80 | 5.20 |
| 16:30 | 3609 | Rajasthan United vs Aizawl FC | 2.10 | 3.20 | 3.20 |
| 17:00 | 5113 | Antalyaspor vs Manisa Futbol Kulubu | 1.51 | 4.17 | 5.04 |
| 17:30 | 4441 | Al Hala Muharraq vs Riffa Club | 5.40 | 3.90 | 1.58 |
| 17:30 | 5944 | AL Sahel SC vs AL Riyadh | 2.26 | 2.95 | 3.50 |
| 18:00 | 2393 | Talaea El Gaish vs National Bank | 2.68 | 2.78 | 2.93 |
| 18:00 | 2983 | Farco FC vs Al Ahly Cairo | 7.59 | 4.20 | 1.42 |
| 18:00 | 4525 | Neftchi Baku vs Zira | 1.67 | 3.60 | 4.47 |
| 18:15 | 5887 | Young Africans vs Coastal Union | 1.14 | 5.02 | 12.08 |
| 18:30 | 2081 | Al Ain vs Baniyas | 1.37 | 4.76 | 6.22 |
| 19:00 | 1237 | Basaksehir vs Goeztepe | 1.31 | 5.05 | 7.19 |
| 20:00 | 5658 | Zamalek vs Haras EL Hodood | 1.34 | 4.58 | 8.95 |
| 21:00 | 2317 | CD Guadalajara vs Elche | 8.55 | 4.47 | 1.36 |
| 21:00 | 3710 | Fenerbahce vs Istanbulspor | 1.24 | 5.64 | 8.36 |
| 21:00 | 3931 | CD Diocesano vs Getafe | 9.99 | 5.19 | 1.28 |
| 21:00 | 4735 | CF Intercity vs Mirandes | 3.23 | 3.23 | 2.20 |
| 21:00 | 5785 | CFR Cluj vs Hermanstadt | 1.61 | 3.51 | 5.73 |
| 22:00 | 1138 | KAA Gent vs Cercle Brugge | 1.77 | 3.74 | 3.94 |
| 22:00 | 1998 | OH Leuven vs Kortrijk | 1.74 | 3.83 | 4.03 |
| 22:00 | 5550 | Mechelen vs RFC Seraing | 1.64 | 3.94 | 4.54 |
| 22:00 | 5921 | Union Saint Gilloise vs Oostende | 1.30 | 5.33 | 7.70 |
| 22:45 | 1055 | Altrincham vs Curzon | 1.51 | 4.17 | 5.04 |
| 22:45 | 1592 | Notts County vs Chorley | 1.31 | 5.60 | 7.60 |
| 22:45 | 2302 | Chesterfield vs Coalville Town | 1.54 | 4.18 | 4.76 |
| 22:45 | 2414 | Northampton vs Carlisle | 2.24 | 3.21 | 3.11 |
| 22:45 | 2435 | Southend vs Boreham Wood | 2.00 | 3.21 | 3.45 |
| 22:45 | 2669 | Guiseley vs Halifax | 3.99 | 3.85 | 1.70 |
| 22:45 | 2968 | Cliftonville Belfast vs Glentoran Belfast | 2.69 | 3.32 | 2.34 |
| 22:45 | 3124 | Gap Connahs Quay vs Aberystwyth Town | 1.16 | 6.45 | 11.73 |
| 22:45 | 3222 | Newcastle vs Bournemouth | 1.45 | 4.37 | 6.36 |
| 22:45 | 3229 | MK Dons vs Leicester | 7.60 | 4.80 | 1.36 |
| 22:45 | 3433 | Royal Antwerp vs Standard Liege | 1.85 | 3.65 | 3.69 |
| 22:45 | 3775 | Aldershot vs Welling | 1.67 | 3.74 | 4.27 |
| 22:45 | 3920 | Oldham vs Peterborough Sports | 1.85 | 3.60 | 3.55 |
| 22:45 | 4176 | Woking vs Eastleigh | 1.93 | 3.60 | 3.65 |
| 22:45 | 5422 | Southampton vs Lincoln | 1.26 | 5.57 | 9.56 |
| 22:45 | 5653 | Wolverhampton vs Gillingham | 1.12 | 7.56 | 18.90 |
| 23:00 | 1758 | Alcorcon vs FC Cartagena | 2.63 | 3.03 | 2.73 |
| 23:00 | 2528 | Guijuelo vs Villarreal | 15.87 | 6.35 | 1.17 |
| 23:00 | 3683 | Aberdeen vs Rangers | 5.18 | 3.99 | 1.58 |
| 23:00 | 5180 | Sestao vs Athletic Bilbao | 10.95 | 5.37 | 1.25 |
| 23:00 | 5473 | Real Union Irun vs Mallorca | 5.78 | 3.99 | 1.54 |
| 23:15 | 4797 | Viseu vs Boavista | 2.87 | 3.12 | 2.32 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# LALJI, ROTARY WAANDAA MBIO KUSAIDIA MATIBABU MACHO

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Lalji kwa kushirikiana na Klabu za Rotary ya Masaki pamoja na Klabu ya Lions-District 411C, wameandaa mbio kwa ajili ya kutoa huduma ya matibabu ya macho kwa Watanzania wenye matatizo hayo.

Mbio hizo zinatarajiwa kufanyika Januari 15, mwakani katika viwanja vya The Green Masaki, lengo likiwa ni kukusanya fedha zitakazotumika katika kutoa huduma ya matibabu ya macho kwa Watanzania wenye matatizo hayo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Taasisi ya Lalji Foundation, Imtiaz Lalji, alisema mbio hizo ni muhimu sana kwa washiriki kiafya, lakini fedha zitakazopatikana zitasaidia kuendesha kambi ya upasuaji wa macho bure hapa nchini.

"Tulipata fursa hii kutoka kwa ndugu zetu Rotary Club na Lions, tukaona ni nzuri kwetu sisi Lalji Foundation kuwafikia Watanzania wasiojiweza kama kinamama na watoto yatima. Hivyo kwetu sisi tumefurahia kushiriki katika kuwahudumia Watanzania wenye uhitaji ambao kwa namna moja au nyingine wameshindwa kupata matibabu ya macho kutokana na hali zao kiuchumi," alisema Imtiaz.

Kwa upande wa Gavana wa Klabu ya Lions, Mustansir Gulamhussein, alisema mbio hizo zinatarajiwa kukusanya fedha zitakazoweza kuwafikia Watanzania zaidi ya 1,000 wenye matatizo ya macho kutoka sehemu mbalimbali nchini na matibabu hayo yatahusisha upasuaji wa mtoto wa jicho, pamoja matibabu mengine ya macho.

Naye Rais wa Klabu ya Rotary, Akash Shah, alisema zawadi maalumu zitatolewa kwa baadhi ya washiriki, ambapo washindi wa tatu wa mwanzo watakaoweka rekodi kwa wanawake na wanaume katika mbio za kilometa 21, watapatiwa zawadi.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Lalji, Imtiaz Lalji (kushoto), Boniface Manko, Gavana wa Klabu ya Lions District 411C, Mustansir Gulamhussein, Rais wa E-club Rotary ya Masaki, Akash Shah na (kulia) ni Samwel Makundi kutoka TravelPort, wakizungumza na waandishi wa habari kuhusu mbio za macho kwa ajili ya kukusanya fedha zitakazotumika kutoa huduma ya macho bure kwa Watanzania wenye matatizo hayo. Waliosimama kutoka kushoto ni Ali Aseem, Reena Pandya, Fatma Lalji na Vikash Shah. **MPIGAPICHA WETU**

# DAUDA AGONGA MWAMBA TFF

**Na Saada Akida**

KAMATI ya Maadili ya Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), chini ya Mwenyekiti wake, Mwita Waissaka, imetupilia mbali maombi ya Mjumbe wa Chama cha Soka Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA), Shafiih Dauda, na kumtaka kuendelea na adhabu yake ya kifungo cha kutojihusisha na soka kwa miaka mitano.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Dauda kupeleka maombi yake ya kutaka kamati hiyo kurejea shauri mama kupitia kikao cha Februari 14 na 15, mwaka huu kwa kumfungia kifungo cha miaka mitano na faini ya shilingi milioni sita.

Kamati hiyo ilimtia hatiani Dauda kutokana na chapisho lake kupitia mtandao wa kijamii wa Instagram kinyume cha 73 (4)(a) na 75 (5) vya kanuni za maadili za TFF toleo la 2021, pia kwa kukiuka kifungu cha 3 (1) cha Kanuni za Utii za TFF toleo la 2021.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti huyo, alisema Desemba 9, mwaka huu walipokea barua ya Dauda akiomba Kamati ya Maadili kusikiliza tena shauri lake mama kwa ajili ya kumuondolea adhabu na faini.

Alisema Desemba 15, mwaka huu, Dauda alikumbushwa kuhusu kikao cha kamati hiyo, lakini aliomba kupangiwa tarehe nyingine kwa sababu ya udhuru.

"Kamati ilimtaka atume mwakilishi wake au mwanasheria katika kikao hicho kilichofanyika juzi Desemba 17, mwaka huu, hakufanya hivyo kwa kutuma mtu wala maandishi yoyote kuhusu kutofika kwake katika kikao hicho alichoomba kwa ajili ya marejeo.

"Kamati ilirejea TFF kuhusu maombi ya marejeo hayo kwa Dauda, shirikisho limetoa majibu kuwa mjumbe huyo hastahili kupewa msamahama aliomba kwa sababu tangu alipopewa adhabu hakuwahi kutumikia adhabu hiyo," alisema Waissaka.

Alisema pia walipokea baadhi ya ushahidi wa mjumbe huyo kuendelea kutumia mitandao yao ya kijamii kurudia makosa yale yale ya kuyasema mambo ya mpira katika mitandao.

"Kwa maamuzi hayo kanuni na sheria iko wazi, anaruhusiwa kukata rufaa kwa Kamati ya TFF, lakini pia adhabu hizo zinapotolewa haziishii kwa TFF tu, bali kwenda hadi ngazi za juu," alisema.

Michezo
Jumanne Desemba 20, 2022
Nipashe



UKURASA 30

## Pele amhurumia Mbappe



### 'SITUNDIKI DALUGA'

"Ni wazi nilitaka kumaliza kazi yangu na hili, siwezi kuuliza chochote zaidi, lakini nitaendelea kucheza kama bingwa wa dunia."

### KOCHA ARGENTINA

"Tunahitaji kumwekea nafasi katika kikosi chake cha Kombe la Dunia 2026, ikiwa anataka kuendelea kucheza, atakuwa nasi."

HABARI KAMILI UK. 29

# YANGA SC, COASTAL MTIHANI MZITO LEO

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Yanga kinashuka dimbani leo kikitaka kuendeleza kampeni yao ya kusaka pointi tatu kwenye Ligi Kuu Bara, lakini kuvuna alama zote sita kutoka kwa Coastal Union msimu huu, wakati 'Wagosi wa Kaya' hao wenyewe wakiwa na mtihani mzito wa kutaka kujibu mapigano na kujinasua katika mstari wa chini kwenye ligi hiyo.

Miamba hiyo, itavaana leo usiku katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ikitaka kuendeleza kasi yao ya ushindi baada ya mchezo uliopita kushinda mabao 3-0 dhidi ya Polisi Tanzania, lakini ikitaka kuondoka tena na alama tatu dhidi ya Coastal Union baada ya mechi ya raundi ya kwanza kuichapa 2-0 katika Dimba la Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Kwa upande wa Coastal Union ambayo inashika nafasi ya nne kutoka mkiani ikiwa na alama 15, mbali na kutaka kulipa kisasi dhidi ya Yanga, inashuka uwanjani katika mchezo huo ikitoka kujeruhiwa na KMC FC kwa bao 1-0 katika mechi ya ligi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam Alhamisi iliyopita.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema wanaamini wako vizuri kiakili na kiufundi kwa ajili ya kutafuta pointi tatu leo.

Alisema wachezaji wako tayari kuendelea na kasi yao ya kutafuta matokeo chanya kwa sababu wanahitaji kufikia malengo yao.

"Mechi ya kesho (leo), tunatakiwa kuwa makini na haitakuwa rahisi kwa sababu ya Coastal Union kwa sasa wana vijana wazuri pale mbele, wanakasi na wanapiga mashuti, lazima tunatakiwa kuwa makini kuwachunga wachezaji hao," alisema Kaze.

Kocha Msaidizi wa Coastal Union, Joseph Lazaro, yeye alisema wamejiandaa vizuri kwa sababu nafasi yao ni ngumu sana na wanatakiwa kushinda katika mchezo wa leo.

"Mechi itakuwa ngumu kwa sababu mchezo uliopita hatukufanya vizuri, tutacheza kwa heshima kubwa na tahadhari kubwa kwa ajili ya kusaka pointi muhimu na kutoka katika nafasi ya chini ya kucheza 'Play off' (mechi ya mchujo)," alisema Lazaro.

Yanga ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 41, nne zaidi ya Simba iliyopo nafasi ya pili ikiizidi Azam FC kwa pointi moja katika nafasi ya tatu.

Mchezo mwingine utakaopigwa leo ni kati ya Ruvu Shooting dhidi ya Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, ambao utaanza majira ya saa 10:00 alasiri.

Kocha Msaidizi wa Ruvu Shooting,

INAENDELEA UK. 28

## Simba: Vipigo zaidi vinakuja

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya ushindi mnono wa mabao 5-0 dhidi ya Geita Gold kwenye mechi ya kwanza ya mzunguko wa pili ya Ligi Kuu, katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza juzi, Klabu ya Simba imetamba kuendeleza dozi nene kwa timu zingine huku Kaimu Kocha Mkuu, Juma Mgunda, akiwashukuru na kuwasifu wachezaji wake kwa kubadilika kadri siku zinavyosonga mbele.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Mgunda alisema wachezaji wa timu yake kwa siku za karibuni wamekuwa wakicheza kwa kupambana na kutaka kufanya vema, pamoja na uchu wa kufunga mabao kitu ambacho kinampa faraja.

"Nilisema hakuna mechi

INAENDELEA UK. 28

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002